


UNIVERSITY OF NAIROBI  
LIBRARY

KILIO CHA WANYONGE KATIKA RIWAYA ZA SAID AHMED  
MOHAMED

Na: MUGAMBI E. KAMUNDE


"Tasnifu hii imetolewa ili kutosheleza baadhi ya  
mahitaji ya shahada ya 'Master of Arts' katika  
Chuo Kikuu cha Nairobi"

1983



U N G A M O

"Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na  
haijatolewa kwa mahitaji ya digrii katika  
Chuo Kikuu kingine cho chote."



MUGAMBI E. KAMUNDE

(Mtahiniwa)

"Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini  
yangu kama msimamizi wa kazi hii wa Chuo Kikuu."



PROF. M. H. ABDULAZIZ

Y A L I Y O M O

UKURASA

Yaliyomo .....	i
Shukrani .....	iv
Muhtasari .....	vi

SURA YA KWANZA

1:1	Utangulizi .....	1
1:2	Somo la Utafiti .....	1
1:3	Madhumuni ya Tasnifu .....	3
✓ 1:4	Mipaka ya Tasnifu .....	4
✗ 1:5	Msingi wa nadharia wa Tasnifu ...	7 *
1:6	Sababu za kulichagua somo hili ..	10
1:7	Kazi zilizotangulia .....	12
1:8	Njia za utafiti .....	14
1:9	Tanbihi .....	15

SURA YA PILI ✓

2:0	UTENGANO ✓	18
2:1	Utangulizi✓	18
2:2	Maudhui✓	19
2:3	Wahusika ✓	27
2:3:1	Maksuudi✓	30
2:3:2	Kazija✓	35
2:3:3	Maimuna✓	40
2:4	Muundo wa jamii katika Utengano ✓	47
2:4:1	Tabaka la kikabaila .....	48

2:4:2	Tabaka la makabwela .....	54
2:5	Kimalizio .....	65
2:6	Tanbihi .....	67

SURA YA TATU

3:0	DUNIA MTI MKAVU .....	71
3:1	Utangulizi .....	71
3:2	Maudhui .....	73
3:3	Ufupisho .....	74
3:4	Wahusika .....	76
3:4:1	Fumu Jaku, Mzee Gae .....	77
3:4:2	Bakari Jaku .....	82
3:4:3	Pandu Jaku .....	88
3:4:4	Fauz, Farouk Hilal .....	92
✓ 3:5	Hali ya uchumi na hisia za mwamko za wanyonge .....	98
3:6	Kimalizio .....	104
3:7	Tanbihi .....	106

SURA YA NNE ✓

✓ 4:0	ASALI CHUNGU .....	108
✓ 4:1	Utangulizi .....	108
✓ 4:2	Maudhui .....	109
✓ 4:3	Hali ya kisiasa katika Asali Chungu .....	110
✓ 4:4	Maisha ya jamii katika Asali Chungu .....	113

4:5	Wahusika .....	117
4:5:1	Zuberi .....	118
4:5:2	Dude .....	120
4:5:3	Kimalizio .....	121
4:6	Tanbihi .....	122

SURA YA TANO

5:0	HITIMISHO .....	124
	MAREJEO .....	127

122  
128  
11

108  
14  
122

67  
18  
11

122  
108  
14

### S H U K R A N I

Napenda kutoa shukrani zangu kwa wale wote waliohusika kwa usaidizi wa namna mbali mbali ili kuifanya kazi hii ifanikiwe.

Kwanza kabisa nampa shukrani zangu za dhati Profesa M. H. Abdulaziz, aliye mkuu wa Idara ya Isimu na Lugha za Kiafrika katika Chuo Kikuu cha Nairobi, sio tu kwa kuisimamia kazi yangu vyema bali pia kwa kunipa shime na mawaidha bora ya kitaaluma.

Nawashukuru pia wahadhiri wote wa Idara ya Isimu na Lugha za Kiafrika kwa maoni yao bora waliyonipa mara kwa mara. Maoni yao yamenifadhili vikubwa katika kuisanifisha na kuisawirisha kazi yangu. Hasa yafaa nimitaje Dkt. Kitsao niliyeanza kazi hii naye akiwa msimamizi wangu. Yeye alinipa msingi dhabiti ambao umekuwa wa manufaa sana.

Namshukuru sana Bw. Said Ahmed Mohamed kwa maoni aliyonipa kuhusu riwaya zake na fasihi kwa ujumla - alipozuru hapa nchini - na vile vile kwa njia ya posta akiwa katika Jamhuri ya Ujerumanî.

Singependa kuwaszau wanafunzi wa M.A. mwaka wa kwanza - akina Lukobwa, Mungania, Ali Wasi, Musau na wengineo. Ndugu hawa walinipa moyo na vile vile kuniondolea upweke, maadam nilikuwa peke yangu katika

mwaka wangu wa masomo.

Nawashukuru akina Peter Mugambi, King'ei na Mbaabu, wote kutoka Chuo Kikuu cha Kenyatta kwa kujitolea kunisaidia pale nilipohitaji msaada wao.

Nakishukuru pia Chuo Kikuu cha Kenyatta kwa kuyagharimia masomo yangu na vile vile kwa kuigharimia kazi ya utafiti, uchapishaji na mahitaji mengine ya kifedha kuihusu tasnifu hii.

Mwisho, lakini si haba, namshukuru sana Bi Agnes Njeri sio tu kwa kuipiga taipu tasnifu hii bali pia kwa kuifanya kazi hiyo kwa uangalifu mwangi. Kwa kuikamilisha kazi hii ameonyesha stahamala na mapenzi katika lugha ya Kiswahili ambayo wapiga-taipu wengi huchelea kuwa ni ngumu na hupoteza wakati.

Kwenu nyote nasema - Ahsante |sana.

## M U H T A S A R I

Tasnifu hii ni kazi ya kifasihi inayoitafiti na kuinakidi fani ya mwandishi mmoja wa kisasa (S. A. Mohamed) katika riwaya zake tatu: Utengano, Dunia Mti Mkavu na Asali Chungu.

Katika uhakiki wake, kazi hii itazingatia kipengele kimoja - nacho ni "wanyonge" wanavyojitokeza na kuyatetea maslahi yao katika ile jamii aliyoichora S. A. Mohamed.

Kila sura itajadili jambo maalum ambalo litakuwa na changizo fulani katika kuyasawirisha maudhui. Mbinu tatu muhimu zitakazotumiwa na kutafitiwa ili kuyatekeleza maudhui ni za "kisiasa", "kiuchumi" na "kijamii". Mbinu nyingine zitakazotumiwa ni kama vile "wahusika", "matabaka" mbali mbali n.k. Kila Sura itaitafiti riwaya moja.

Sura ya kwanza ambayo ni utangulizi haina budi kuutoa ufanuzi kuhusu mada ya tasnifu. Ufanuzi huu hasa utajikita katika neno "wanyonge" ambalo lina utata mwingi, maadam kuna "wanyonge" au "unyonge" wa daraja na viwango mbali mbali - mathalani, kuna unyonge wa kitabia, kiuchumi, kiakili, kimwili n.k.

Sura hii pia itafafanua kuhusu maana ya "riwaya" na wajibu wa fasihi na mwandishi kwa madhumuni ya kumaizi kundi (tabaka) mwandishi analojitambulisha nalo.

Jambo hili litaisaidia sana tasnifu hii maadam mwandishi anayejitambulisha na walio wengi, bila shaka atayatilia maanani maslahi yao na atajitambulisha nao katika ukombozi.

Sura ya pili itaihakiki riwaya ya Utengano hususa katika mbinu ya kijamii. Katika sura hii, tutaigawa jamii katika matabaka mawili - tabaka la matajiri na lile la maskini kwa madhumuni ya kubainisha uhusiano ulioko baina ya makundi hayo na jinsi uhusiano huo unavyoathiriana. Ili kufikilia lengo hili hatuna budi kuchunguza jinsi wahusika wa daraja mbali mbali walivyochorwa katika riwaya ya Utengano.

Sura ya tatu ni uhakiki wa riwaya ya Dunia Mti Mkavu. Mtindo utakaotumiwa katika uchambuzi wa riwaya hii ni kama uliotumiwa katika sura ya pili - lakini sura hii itakita kwa upande wa "uchumi". Tumedhamiria kuonyesha jinsi hali ya uchumi iliviyowasakama watu wa kiwango cha chini katika jamii aliyo tupu S. A. Mohamed. Lengo kuu ni kudhihirisha jinsi kundi la watu walioonewa na kudhulumiwa wanavyowaza udhalimu unaowakabili.

Sura ya nne itakuwa fupi kuliko ile ya pili na ya tatu. Tumeifanya iwe fupi ili kujiepusha na kuyarudia yaliyotajwa katika sura zilizotangulia.

Sura hii ni utafiti wa Asali Chungu. Mbinu itakayozingatiwa ni siasa na jinsi mamlaka yanavyogawa, hasa katika jamii za kinaizi na kibwanyenye ambazo zimejaa anasa na ulimbwende. Tutachunguza athari za maisha ya namna hiyo na jinsi yanavyowaathiri wanyonge katika jamii tunayoitafiti.

Sura ya mwisho itakuwa ni "Hitimisho". Itakuwa ni kiungo cha kuyaunga mawazo na maoni yaliyoko katika sura nne za mwanzo. Itatoa pia msimamo na imani kuhusu suala la "wanyonge" katika jamii.

## S U R A Y A K W A N Z A

### 1:1 UTANGULIZI

### 1:2 SOMO LA UTAFITI

Tasnifu hii itajishughulisha na uhakiki wa riwaya tatu za Said Ahmed Mohamed, katika kipengele kimoja - 'Wanyonge'.

Riwaya ni mojawapo ya tanzu (nyanja) tatu (nyigine zikiwa ni tamthilia na ushairi) za fasihi ya Kiswahili.

Maana ya riwaya ni hadithi iliyo ndefu kutosha kufanya kitabu kimoja au zaidi. Habari iliyomo ni ya kubuniwa tu na imejengwa juu ya tukio la historia. Yaweza kuandikwa kwa maelezo ya ujazo (au nathari).<sup>1</sup>

Maoni zaidi kuhusu riwaya ni kuwa ni hadithi iendayo mfululizo kwa kinaganaga;

Hueleza maisha ya mtu au kikundi cha watu katika jumuiya yao au vipengee fulani vya maisha yao.<sup>2</sup>

Kuna madhumuni mbali mbali ya kutunga riwaya. Mathalani, kustarehesha, kuburudisha (kujiburudisha), kufundisha au kuhimiza ujasiri katika maisha, kuufunulia umma migogoro na mwenendo wake, kusahihisha makosa na kasoro za umma na watu binafsi kwa lugha ya msisitizo au kejeli.

Msanii wa riwaya tatu tunazozihakiki ameutumia usanii wake kuwahimiza wanyonge na kuwapa hisia za mwamko wa kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni na kuwafanya sio tu watambue haki zao bali pia wazipiganie.

Neno "Wanyonge" au "Unyonge" kama lilivyoelezwa katika kamusi ya Kiswahili Sanifu lina maana ya;

"Hali ya kuwa dhaifu".<sup>3</sup>

Udhaifu huu unaweza kuwa wa hali nyingi. Lakini kwa vyo vyote vile, kuwa katika hali dhaifu ni kuwa na upungufu wa kitu fulani. Mtu anaweza kuwa dhaifu kwa kupungukiwa na nguvu za mwili. Upungufu wa namna hiyo waweza ukatokana na hali nyingi, kama vile maradhi, njaa N.K. Vile vile, mtu aweza kuwa na unyonge (udhaifu) kwa kupungukiwa na mali, akili au afya.

Tasnifu hii haidhamirii kuzungumzia juu ya unyonge (wanyonge) kwa ujumla. Tutajifunga katika namna ya unyonge unaojitokeza katika riwaya tatu tunazozihakiki.

Unyonge katika riwaya hizo watokana hususa na mifumo mbali mbali katika mazingira anayoyachora msanii. Mifumo hii ni kama vile; siasa, uchumi, jamii na utamaduni. Mifumo hii pia inaigawa jamii kitabaka, ambapo tabaka la juu linatumia mamlaka na nguvu zake kulinyanyasa na kulikandamiza tabaka la chini. Hili

45  
12  
62  
B

tabaka la chini ndilo ambalo tunaweza tukaliita tabaka la "wanyonge", waliokandamizwa, ambao hawana sauti na ni dhaifu (wapungufu wa nguvu) kwa vile hawawezi kuusimamia au kuutawala uchumi.

Kwa upande mwingine, tunatumaini kuwa tasnifu hii itaonyesha kuwa katika jamii anayoizungumzia S. A. Mohamed, unyonge haupo tu katika tabaka la chini. Kuna unyonge mwingine unaodhihiri (hasa unyonge wa tabia) mionganoni mwa matabaka yenye uwezo na madaraka. Hali hii itaonekana waziwazi tutakapoingilia uhakiki wa wahusika mbali mbali riwayani. Kuwepo kwa unyonge katika viwango kadhaa kwatuonyesha kuwa hakuna kiumbe aliyekamilika na vile vile kuwa wanyonge ni wa aina mbali mbali. Wazo hili lautilia nguvu msemo usemao kuwa "Hujafa hujaumbika", na linatoa waadhi kwa waliobarikiwa kupata cheo, hadhi, mali na utukufu kuwa, hivi ni vitu vya hapa duniani na havidumu daima dawamu.

### 1:3 MADHUMUNI YA TASNIFU

Vari  
malku  
wanavu  
upyo

Madhumuni ya tasnifu hii ni kuhakiki hali ya wanyonge kama wanavyojitokeza katika riwaya tatu za Said Ahmed Mohamed - yaani; Utengano; Dunia Mti Mkavu na Asali Chungu.

Lengo hili litafikiliwa kwa njia kadhaa. Kwanza ni kuhakiki jinsi wahusika kadhaa walivyochorwa riwayani na kutoa ufanuzi kuhusu "wanyonge" kwa kueleza aina mbali mbali za wanyonge na hali zao. Licha ya hayo,

kazi hii itajaribu kueleza na kubainisha juhudi zinazofanywa na wanyonge hao ili kujiinua na kujikomboa kutokana na hali yao dhaifu katika mazingira na jamii ambamo msanii anawachora.

Katika riwaya zake, Said Ahmed Mohamed amewachora wanyonge kama kundi la watu katika matabaka ya jamii, ambalo linaonewa, linadhulumiwa na linanyanyaswa. Uonevu huu umetokana na mifumo ya kisiasa, kiuchumi na kijamii, ambayo inajitokeza kinaganaga katika jamii fulani finyu ambayo msanii anaishughulikia.

Ingawa ni tatizo lisilo haba kuipambanua mifumo hii, pale ambapo uwezekano utapatikana, basi upambanuzi utatolewa.

Katika kuihakiki mbinu hii ya "wanyonge", vile vile, tutajaribu kuipata ithibati kuwa "wanyonge" wameonewa na ni kwa kiasi gani - kama inavyodhihirika riwayani. Kisha tuchunguze ari na shime zinazofanywa na baadhi ya wahusika waliodhalilishwa ili kuikata minyororo ya kiutumwa.

Ni' dhamira yangu kuwa kwa kuhakiki kipengele cha wanyonge kama walivyowasilishwa riwayani, ukweli wa maisha ya uhalisi ya jamii, kwa mujibu wa historia utabainika.

#### 1:4 MIPAKA YA TASNIFU

Kazi hii kwa kiwango kikubwa itakuwa kazi ya

uhakiki wa kifasihi. Uhakiki wa kifasihi ndio ambao umesadifu zaidi maadam imeelezwa kuwa;

Fasihi hutokana na vitendo vya kihisia vya watu katika jamii ----- Fasihi ni zao la kipawa cha watu kimaarifa linalowasilishwa kwa maandishi (maneno) kuonyesha ukinzani na migogoro katika jamii.<sup>4</sup> (tafsiri ~~yangu~~) *Huu si naomibwana.*  
<sup>yangu</sup>

Aidha, wataalam wengine kama vile Coser wamesema kuwa fasihi ni;

Kauli hai kuhusu maisha na mapambano ya kujihami kwa hali na mali kwa watu wa jamii fulani.<sup>5</sup> (tafsiri ~~yangu~~).

Kwa vyo vyote vile fasihi imeelezwa kama kioo cha kuiangalilia jamii fulani. Ni kwa mujibu huu (ambapo fasihi haiwezi kutengwa na jamii) ambapo katika kuhakiki "wanyonge" katika jamii aliyotuchorea msanii riwayani tumeamua kuzingatia uhakiki wa kifasihi.

Tasnifu hii haidhamirii <sup>Ku</sup>kiuka mipaka ya jamii anayozungumzia Said Ahmed Mohamed.

Ni Tutajifunga katika nyakati na mazingira tunayopewa na mwandishi. Ingawaje si jambo rahisi kuweka mpaka tukasema mwandishi aandika baina ya mwaka huu na huu, tasnifu hii itakuwa na wajibu wa kubainisha nyakati tofauti tofauti katika kila riwaya.

Jambo maalum ni kuwa tutajishughulisha na maisha halisi kama yalivyolengwa katika jamii aliyoikusudia mwandishi.

Lakini, ingawaje tutajifunga katika riwaya za mwandishi mmoja, haimaanishi kuwa tukiyapata mawazo ya waandishi wengine wanaolandana kimaudhui na msanii wetu tusiyachukue. Tutayachukua, lakini ni kwa madhumuni ya kutilia nguvu maoni au fikra za msanii yule mmoja tunayemhakiki. Aidha, maoni tutakayoyachukua kutoka "nje" hayana budi yatusaidie katika kulifikilia lengo la tasnifu kwa jumla.

Ingawa Said Ahmed Mohamed ameziandika riwaya zake baina ya mwaka 1977 na 1980 (Asali Chungu - 1977; Utengano - 1980, Dunia Mti Mkavu - 1980), ameweza kuranda kwa usanii mwangi katika nyakati za nyuma ya miaka hiyo. Kwa mfano, ametuchorea (sio katika riwaya zote) jamii fulani ambayo iliishi katika utawala wa Kinaizi. Jamii ya aina hiyo itachunguzwa katika tasnifu hii hususan kwa muktadha wa jinsi walio wanyonge walivyojitahidi na kujikakamua ili kupambana na hali ile wakati ule.

Katika jamii nyingine (ya riwayani), tutakuwa na jukumu la kutafiti hali ya wanyonge hasa baada ya jamii ile kujikomboa kutokana na udhalimu wa wakoloni - yaani baada ya kujipatia "Uhuru wa bendera".<sup>6</sup>

### 1:5 MSINGI WA NADHARIA WA TASNIFU

Katika tasnifu hii, ambayo imejikita katika kipengele kimoja katika jamii, hatuna budi kuuchukua mtazamo wa kijamii kuwa ndio msingi wetu wa nadharia. Madhumuni ya kuichagua nadharia hii ni kuwa fasihi, kama ilivyosemwa hapo juu, sio tu zao la jamii, bali pia mizizi na misingi yake imēkita katika jamii hiyo.

Kutokana na dhana ya fasihi katika muktadha wa jamii, wametokea wahakiki chungu nzima ambao wamejizatiti kutoa maelezo yao kuhusu fasihi na jamii - Mathalani Ngugi (1978) Literature and Society.

Kazi hii pia itatumia msingi wa nadharia wa Ki-Marx ili jamii iweze kueleweka kikamilifu. Dhamira ya kuutumia mfumo huu ni kuwa jamii tunayoihakiki imejengeka katika matabaka mbali mbali.

Katika The Communist Manifesto, maoni ya Marx kuhusu jamii zote ni kuwa;

Historia ya jamii zote zilizoko ni historia ya mapambano ya kitabaka -----.

Wakandamizaji na wale wanaokandamizwa wako katika kambi mbili za ukinzani.<sup>7</sup> (Tafsiri yetu yangu). *Marx*  
*yenu* *Marx*

Akiendelea na maudhui yake kuhusu tabaka katika jamii, Marx anatuambia;

Jamii nzima inaendelea kugawanyika katika kambi mbili zinazopingana; inagawanyika katika matabaka mawili ambayo yanapingana kiwazi; Bwanyenye na Proletarii.<sup>8</sup> *fasabhi wasichonecho  
wakata au mafalaki* (Tafsiri yangu).

Mojawapo ya jukumu la Marx lilikuwa ni kuuboomoa na kuuangamiza ubebera na ubepari, mifumo ambayo ilielekea kuiangamiza na kuiteketeza jamii. Mifumo hii imekuwa kama ugonjwa ambao hauna budi kuchangiwa dawa kwa hali na mali.

Marx hutoa maoni kuwa tabaka zima la watu wanaodhulumiwa na kuonewa hawana budi kuungana kwa umoja ili kumng'oa adui anayewakabili. Adui huyu ndiye anayehodhi uchumi, rasilmali na amemhini mnyonge angalau nafasi ya kupumua.

Marx aonelea kuwa njia ya kujikomboa na kurejesha hali za kiutu, haki, usawa na utangamano ni moja tu. Nayo ni kuchukua ala na kujiandaa kwa mapambano.

Anahimiza kwamba inawapasa wanaonyanyaswa wawe na hisia za mwamko na wafahamu dhahiri kuwa wameonewa. Kisha kufanya hivyo, ni jukumu lao kuzua mbinu za kujikomboa hususa kutokana na kasumba waliyoivuta ikawaingia katika akili, mawazo na fikra.

Katika kitabu cha Swingewood, Marx and Modern Social Theory, mwandishi atuambia kuwa;

Nadharia ya Marx ya kijamii husisitiza  
uhusiano wa kiuchumi baina ya njia za <sup>mawazo si  
jina lao</sup>  
uzalishaji na utambuaji wa uhuru kwa  
wafanyakazi - uhusiano wake na watu wa  
tabaka lake huleta mwamko wa kitabaka.<sup>9</sup>  
(Tafsiri yangu).

Dhana ya Marx ni kuwa migogoro, migongano na  
ukinzani wa kitabaka unatokana na uchumi - jinsi  
unavyosimamiwa na jinsi unavyogawa kwa kila kundi.

Kutokana na hali hii, itikadi ya Marx na ya  
wahakiki wengine katika jamii (akiwepo S. A. Mohamed -  
mwandishi wa riwaya tunazozihakiki) ni kuwa ni muhali  
amani kupatikana mahali pasipokuwepo haki, usawa na  
ukweli. Itikadi hii yaelekea kuupa nguvu msemo wa  
Kiswahili usemao kuwa; "Amani haiji ila kwa ncha ya  
upanga".

Ili kuwe na jamii inayostahiki, mapinduzi ni  
jambo la lazima. Njia ya pekee ya kuyaleta haya  
mapinduzi (ya kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni)  
ni mapambano tu. Na hapa ndipo wafanyakazi (wanyonge)  
wanapohimizwa waungane na wachukue ala ili wapigane  
na "mabwana zao".

Katika unasibishaji wa nadharia ya Ki-Marx na  
kiini cha tasnifu hii, Said A. Mohamed na waandishi  
wengine anaooana nao kimaudhui amejaribu kuibainisha

wazi mifumo inayosababisha "kilio cha wanyonge" na kutoridhika kwao, na jinsi wanavyojiandaa ili kuuleta ukombozi.

1:6 SABABU ZA KULICHAGUA SOMO HILI

Hadi kufikia sasa, hakujawahi kutokea tahakiki zilizoshughulikia riwaya tatu za Said Ahmed Mohamed.

Isitoshe, hakuna hata mhakiki mmoja aliyejitokeza uwanjani kuutambua au hata kuukejeli umbuji wa S. A. Mohamed katika fani hii ya kuziunda riwaya.

Jambo maalum lililon<sup>ku</sup>vuta kama sumaku katika kulichagua somo la kazi hii ni ile itikadi ya mwandishi mwenyewe. Itikadi yake maalum ni kuwa ijapokuwa dhuluma na uhaini vitaendelezwa kiasi gani, hatimaye haki na utu vitatawala katika jamii. Aidha, mahali pasipo haki, amani haiwezi kuwepo. Imani hii ya walio 'wanyonge' inadhihirika katika riwaya na itajitokeza katika sura zifuatazo ambapo wanyonge wanazusha mtafaruku dhidi ya wenye 'nguvu'.

Mwandishi aitumia itikadi yake kama kigezo cha kuundia riwaya. Anajitambulisha na walio wengi ambao kwa sadfa ndio wanaonyanyaswa.

Katika itikadi yake, S. A. Mohamed aamini kwamba;

Lazima mwandishi awe na mtazamo madhubuti juu ya jambo au mambo mbali mbali ya maisha. Kwa mfano, suala la umaskini,

unyonge na uonevu kati ya mwanadamu na  
mwanadamu analionaje mwandishi -----?<sup>10</sup>

Anaendelea S. A. Mohamed;

Na mwandishi anapaswa kufuata itikadi  
ipi? Bila shaka ile itikadi inayotetea  
wengi; wazee na ndugu zetu ambao maisha  
yao yafanana na maisha ya wanyama -----.<sup>11</sup>

Somo hili la "wanyonge" limechaguliwa kwa kutilia  
maanani wajibu wa fasihi na wajibu wa msanii katika  
jamii. Tukichukulia kuwa wajibu wa fasihi ni kuimulika  
na kuielimisha jamii, na kuwa msanii ana wajibu wa  
kuiambia jamii ukweli, basi, itaonekana kuwa ni  
unafiki mkubwa kwa waandishi kuandika ili kuwafurahisha  
watawala au "mabwana zao".

Mwandishi anayestahiki jina hilo hana budi  
ayaeleze maisha ya watu katika jamii kihalisi ili  
jamii ile iweze kujisahihisha.

Katika riwaya zake, S. A. Mohamed amefaulu  
kutuchorea picha ya maisha ya uhalisi bila kuchelea  
jambo lolote. Amefanya hivi kwa kutumulikia wanyonge,  
hali zao, maslahi yao, hisi zao, malalamiko na  
harakati nyingine katika maisha yao ya kila siku.

Inatumainiwa kuwa somo hili litaamsha hamu na  
shime kwa wasomi ili wachukue ala za kitaaluma na  
kutafiti zaidi kuhusu fani mbali mbali zinazojitokeza

katika riwaya za S. A. Mohamed.

1:7 KAZI ZILIZOTANGULIA

Mpaka sasa hakujatokea tahakiki zozote zenyewe kutajika zilizozichambua riwaya za S. A. Mohamed.

Ni makala mawili tu yaliyoweza kupatikana ambayo yalishughulikia kazi hiyo. Licha ya hayo, kuna pia kazi moja ya tasnifu.

S. A. Mohamed mwenyewe ameyaandika makala akayaita;

"Kupatana na riwaya zangu",  
aliyoyatayarisha kwa madhumuni ya kuyatoa katika kongamano iliyofanyika katika ukumbi wa "Kenya Polytechnic" mnamo Agosti - 1981.

Ingawa makala haya yamekita zaidi katika nadharia kuliko katika uhakiki, bali yana fungu lake la kuchangiza katika tasnifu hii. Katika makala hayo, msanii asema kuwa ni vigumu sana mwandishi kuweza kujihakiki mwenyewe. Hivyo hatuwezi kuyaita makala hayo uhakiki wa riwaya za mwandishi. Dhamira yake (mwandishi) kuu ni kuonyesha uhusiano wake na riwaya zake na jinsi (riwaya) zinavyojengeka.

~~+ Makala haya yazungumzia umbuji wa msanii wa riwaya kwa jumla bali hayashughulikii kipengele kimoja kama ilivyo madhumuni ya tasnifu hii. Kwa hivyo, huenda yasitufae kiasi kikubwa maadam yamekita zaidi~~

katika muundo na mtindo wa riwaya.

Sehemu moja tu ambayo ina uwiano na madhumuni ya tasnifu hii ni sehemu ambapo makala haya yanaeleza kuhusu wajibu wa msanii katika sanaa ya uandishi. Hapa, S. A. Mohamed anajitambulisha na walio wengi katika jamii, na kutupa dhana kuwa mwandishi ye yote anayesadifu hana budi kujitambulisha na kundi la watu ambao wanakandamizwa, kunyanyaswa na kudhulumiwa na tabaka la juu lenye uwezo na nguvu.

Makala ya pili ni yale yaliyoandikwa na Dkt. Al-Amin Mazrui, "Dunia Mti Mkavu" (A literary treatise on Marxism).

Mazrui, katika uhakiki wake, ametumia Nidhamu ya mfumo wa Ki-Marx na sanaa - jamii kuitazama Dunia Mti Mkavu.

Ametumia uhakiki wa kijamii kuukejeli na kuubeua ubwanyenye na unaizi ulioenea Unguja.

Tasnifu hii itanufaika sana kutokana na maoni ya Mazrui ingawaje itajifunga tu katika "wanyonge" wanavyojitokeza katika mazingira iliyoelezewa.

Tasnifu ya Kazungu (1983) ya M. A. pia imeingilia riwaya moja ya Said Ahmed Mohamed - Asali Chungu. <sup>Na ukaini kuri mwaya imeshui!</sup> <sup>12</sup>

\* Ingawaje Kazungu amechunguza riwaya hiyo hasa kwa upande wa lugha na matumizi yake katika kuendeleza maudhui, kazi hii itatusaidia kuimaizi riwaya hiyo kwa mujibu wa uhakiki.

*wenye kazi  
kutoka kwa mafano*  
Jambo muhimu alilolitafiti Kazungu kwa mfano,  
ni ule ulimwende uliotapaka Unguja. Watu wa tabaka  
fulani walishiriki katika mambo ya anasa na starehe -  
vitu ambavyo vilipatikana kutohana na jasho la wakulima  
(wafanyakazi wa kiwango cha chini cha maisha).

1:8 NJIA ZA UTAFITI

Tasnifu hii itatumia njia kadha kama mwongozo  
wa utafiti.

Kwanza kabisa ni kuzisoma kwa mapana na kwa  
kuchimba riwaya tatu za Said A. Mohamed; Utengano,  
Dunia Mti Mkavu na Asali Chungu.

Kisha tutachunguza baadhi ya mienendo ya wahusika  
hususa nguli na wakinzani kwa kusudi la kuelewa jinsi  
wanavyosaidia katika kuiendeleza maudhui. Tutajaribu  
pia kuubainisha ukinzani au migogoro iliyopo baina  
ya makundi mbali mbali ya wahusika - au katika jamii  
iliyoelezwa riwayani ambayo inawakilishwa na wahusika  
mbali mbali. Ubainishaji wa namna hii ni muhimu ili  
tuweze kuitazama mazingira ambamo unyonge unaibuka.

Pili, tutavisoma vitabu vinginevyo vyenye  
kuiendeleza maudhui inayolandana au hata kukurubiana  
na ile ya "kilio cha wanyonge" inayoendelezwa katika  
riwaya za S. A. Mohamed. Vitabu vitakavyosomwa ni  
kama vile; S. A. Mohamed - Sikate Tamaa (mashairi);  
M. S. Mohamed - Nyota ya Rehema, Kiu (riwaya);

Hussein - Mashetani, Arusi (tamthilia); Mazrui - Kilio Cha Haki (tamthilia); Ngugi na Micere - Mzalendo Kimathi (tamthilia), na vinginevyo vyenye kuinufaisha kazi hii.

Ingefaa ifahamike kuwa vitabu hivyo vitatumia  
kwa madhumuni ya kupanua mawazo tu katika kuliendeleza  
somo hili. Hivyo, tutayachuja yale ambayo yatatuwauni  
na kuurutubisha uhakiki wetu wa "wanyonge".

Tatu, litakuwa jambo aula kukutana ana kwa ana  
na S. A. Mohamed (mwandishi wa zile riwaya tatu) ili  
kupata mawaidha machache kutoka kwake, hasa juu ya  
maisha yake, mazingira, itikadi na kadhalika. Naamini  
kwamba kwa kukutana na mbuji huyu nitanufaika zaidi  
katika jukumu la kuzinakidi na kuziratili riwaya  
zake.

Mwisho, nitazungumza na wanavyuoni kadha na  
wataalam wengine wo wote wale wanaoweza kutoa mawaidha  
muafaka.

Nina imani kubwa mno kuwa taaluma, maoni na  
fikra za watu mbali mbali zitaniauni vikubwa katika  
kuisanifisha na kuikamilisha tasnifu hii.

1:9 TANBIHI

1. Nkwera, F.M; Sarufi na Fasihi Sekondari na Vyuo, Tanzania Publishing House,  
Dar-es-Salaam, 1978 u.k. 109.

2. Kama nambari 1, juu.
3. Kamusi ya Kiswahili Sanifu, Oxford University Press, 1981, u.k. 302.
4. Ngugi, "Literature and Society" in E. Gachukia's Teaching of African Literature in Schools, Kenya Literature Bureau, Nairobi, 1978 uk. 3.
5. Coser, L.A., Sociology Through Literature, Prentice Hall, International Inc. London, 1963, uk. 1 - 2.
6. Kama nambari 4, juu.
7. Marx K., & Engels F., The Communist Manifesto, Penguin Books, 1978, uk. 79.
8. Kama nambari 7, juu.
9. Swingewood, A., Marx and Modern Social Theory, The Macmillan Press Ltd., London, 1975, uk. 114.
10. Mohamed, S.A., "Kupatana na riwaya zangu". Makala yaliyotolewa kwa kongamano katika ukumbi wa "Kenya Polytechnic" Agosti, 1981 uk 4 - 7.

11. Kama nambari 10, juu.

12. Kazungu, K., Tasnifu ya Digrii ya M.A. (1983),  
Chuo Kikuu Cha Nairobi.

## S U R A Y A P I L I

2:0 UTENGANO

2:1 UTANGULIZI

Mohamed Said  
Mohamed

Utengano ni riwaya ya pili aliyoiaandika Said Ahmed Mohamed. Ya kwanza ni Asali Chungu.

Katika Utengano, mwandishi, kwa kuutumia ufundi wake ameweza kutuchorea picha na kutupa mandhari ya jinsi mambo yanavyotokea katika maisha ya kila siku ya jamii fulani.

Amefinilia lengo hili kwa mbinu kadha. Mathalani anawatumia wahusika ambao ni viumbe wa hadithini, kwa kuwapa kila mmoja wao nafasi au fungu fulani la kuchangiza katika uendelezaji wa maudhui.<sup>1</sup>

Katika riwaya hii wamewasilishwa wahusika wa viwango na namna mbali mbali. Kuna nguli na vile vile kuna wakinzani. <sup>particular</sup> <sup>as far as</sup> Aidha, kuna wahusika wengine ambao wametumiwa tu kama viungo au viwakilisho vya kuunga vitushi mbali mbali vya riwaya.

Wahusika wanajitokeza katika jamii ambapo;

Maisha hugawiwa mapande katika kile tukiitacho siasa, uchumi, ma-sala ya kijamii, ya kiutamaduni, ya kidini ----- n.k.<sup>2</sup>

Ingawa mifumo hiyo yote imejitokeza katika

Utengano, lakini si jambo rahisi kuweza kupambanua au kuchanganua kwa mfano siasa kutoka katika uchumi, maadam mambo haya yamechangamana na ndiyo hasa misingi ya jamii katika Utengano. Lakini, kwa kuwatumia wahusika kama vyombo au viōo vya kuiangalilia jamii tutaihakiki na kuinakidi nifumo hii ~~moja~~ moja au yote kwa pamoja ili kuweza kutambua jinsi inavyoathiri jamii anayoizungumzia Said Ahmed Mohamed.

2:2 MAUDHUI

Dkt. Kitsao amekariri katika mihadhara yake kuwa Utengano ni mojawapo ya riwaya za Kiswahili zinazoendeaza maudhui ya "Kilio Cha Wanyonge".<sup>3</sup> Tasnifu hii inaliunga <sup>inaliunga</sup> mkono wazo la Kitsao, na kuongeza kuwa, ingawaje yaweza kusemwa kuwa "kilio cha wanyonge" ndiyo maudhui <sup>na</sup> kuu, kuna maudhui <sup>me</sup> nydingine ndogo ambayo <sup>na</sup> inasaidia katika <sup>kutendeze</sup> <sup>maudhui</sup> kuu. <sup>Vijana!</sup> <sup>Jipunze</sup> <sup>Kiswahili.</sup> <sup>Whubalano</sup> <sup>wa</sup> <sup>ngeli</sup> <sup>Shule</sup> <sup>ye</sup> <sup>misig</sup> <sup>SP</sup> <sup>Kay</sup>.

Katika jalada la Utengano, tunayapata maneno yafuatayo;

Ilikuwaje hata Maimuna - mwari ~~Mwafrika~~, mwana wa nyumba kubwa - kubadilika kiasi hicho? ----- Ni nini hasa kilicholeta utengano nyumbani mwa Bwana Maksuudi?<sup>4</sup>

Maneno haya yanatuashiria kuwa kuna utengano "nyumbani mwa Bwana Maksuudi". Vile vile yanamkabidhi

mhakiki jukumu la kukitafuta kiini cha utengano huo.

Ni jambo aula iwapo utengano uliopo utabainishwa kabla ya kuingilia suala la kukitafuta kiini chake.

Maksuudi ametengana na dunia, wadhifa (kazi),  
bibiye Tamima, wanawe Maimuna na Mussa, Mwanasururu  
n.k. Rashidi ametengana na kazi, Maimuna na mji  
(akaenda Futoni) na vile vile Mama Jeni na Biti Sururu.  
Mwanasururu naye ametengana na dunia.

— Kwa maoni yangu, utengano huu huletwa na hali au  
taratibu za jamii na utamaduni wake. Hali hizi ni kama  
vile ubwanyenye, uliotokana na athari ya Uarabu/Uajemi  
na Uislamu (hata kabla ya ukoloni wa Waarabu kuanza)  
na Ubepari, uliotokana na uzungu na Ukristo katika  
muda wa ukoloni wa Waingereza na Wazungu wengine.<sup>5</sup>

Utengano huu vile watokana na ubinafsi,  
uroho, uafriti na dhuluma, mambo ambayo husababishwa  
na athari za pesa — katika muktadha wa jamii za kikabaila  
na kibwanyenye. Hali hii hasa imetokana na athari za  
mapinduzi ya viwandani ambayo yalisababisha hali ya  
'ubwana' na 'utumwa', masala ya wafanyakazi na ile ya  
wasimamizi (mabwana zao) n.k. Ni katika muktadha huu  
ambapo tunamuona Maksuudi akiwa mwenye takaburi, tadi  
na inda. Amejitosa katika kinamasi cha anasa kiasi cha  
kuwa ameuasi utu wake. Haoni karaha kufanya mambo ya  
kiunyama (hata kwa mke wake) kwa vile cheo, mamlaka na

pesa zimempokonya utu - na kumfanya asitambue halali wala haramu.

Kasumba hii ya hadhi, cheo na pesa imewaingia viongozi wengi akilini Chambilecho Hussein katika Mashetani.<sup>6</sup> Imewapumbaza na kuwahadaa mpaka wakasahau msemu wa wahenga usemao kuwa, "Mpanda ngazi hushuka". Maudhui hii ya hadaa na pumbao la dunia imezingatiwa katika utenzi wa Al-Inkishafi, ambapo mshairi anaunasihi moyo wake kwa kunaswa na "ghururi" za dunia. Anaunasihi moyo wake ili uzinduke katika usingizi, kwa mfano, mshairi ausaili moyo wake;

Moyo wangu nini huitabiri!

Twambe u mwerevu wa kukhitari,

Huyui dunia ina ghururi?

Ndia za tatasi huzandamaye?<sup>7</sup>

Ubeti huu unapiga mwangwi katika Utengano, kwa vile wanaoshiriki katika vitendo vya dhuluma na vya uhaini wanadhani kuwa wataishi hapa duniani milele. Wametekwa bakunja na mali na utajiri hata hawatambui kuwa vitu hivyo havidumu hapa duniani. Wameasi haki na utangamano pasipo kufahamu kuwa hatimaye, haki itatawala na walio maadui wa haki watatumbukia kwenye kaburi la sahau.

au Wazo <sup>liver</sup> <sub>me</sub> (-½ <sup>utengano</sup>)

Maudhui nyingine ambayo yajitokeza wazi wazi ni ile ya, "Taasubi ya kiume" au "udhalilishaji wa kike

10,000

8,000

5380

(uke)". Dhana hii yamfanya mwanamke aonekane dhaifu na mnyonge mbele ya mwanamume. Katika Utengano, msimu na hadhi ya mwanamke ~~imepuuzwa~~ na (mwanamke) akafanywa kuwa kama chombo au kifaa cha kukinaishia haja za mwanamume. Hakuna usawa wala haki baina ya mume na mke. Wanawake nao hawalali. Wanatoa malalamiko yao kinaganaga bila ya kuchelea nguvu za wanaume. Wanawake wamepata hisia za mwamko za kujitetea na kupigania maslahi yao. Kwa mfano, kumetokea waandishi wa Kiswahili wenye kuiandikia maudhui ya kupigania maslahi ya wanawake.<sup>8</sup>

S. A. Mohamed amtumia mhusika wake Kazija, (ambaye ameonewa sio tu na dunia bali pia na Bw. Maksuudi) kama chombo au sauti ya kuyatetea maslahi ya wanawake.

Mwanzo kabisa wa sura ya kwanza mwandishi atueleza;

Kuna mengi ambayo Kazija anayachukia. Ndiyo, anachukia ----- . Kwanza anamchukia mwanamume. Mwanamume anamchukia kwa sababu dhahiri, nayo ni kuwa ameekwa mbele, ingawa Kazija hajui na nani. Pili, anaichukia nafsi yake - nafsi iliyolemaa na kuridhi siku zote kumpembejea mwanamume ambaye ni kiumbe kama yeye. Anachukia hali yake, anachukia jamii yake, anachukia, anachukia kila kitu, kila kitu ----- . (uk. 1)

Kazija si mwanamke wa kwanza kulalamika kuhusu

*Iabia ya  
mchumvi na h*  
 msimu wa wanawake na maslahi yao katika jamii. Katika kazi kadha za Kiswahili na vile vile Kiingereza, tumewaona wanawake wakijitokeza kupigania haki zao.

Maandishi hayo ni kama vile, Tambueni Haki Zetu,

Wimbo Wa Lawino n.k.

Kazi moja ya Kiingereza ya Mutiso G. C. (1947)

imetueleza kuhusu mhusika mmoja (mwanamke) ambaye amekataa kuamka asubuhi na mapema kumtayarishia mumewe

chai, akidai kuwa wote wana haki sawa. *Upuzi!*

*Chungu! Upuzi? Haki gani? - Haki ya usawa baina ya mwanamke na mwanamume;*

*tijeceli* ----- elimu bora kwa mwanamume, kazi

bora kwa mwanamume, haki zote kwa mwanamume.

Mwanamke ni nani mbele ya mwanamume? (uk. 7).

*= ni kwanza cha kifurahisha na kifurahisha mwanamume.*

Malalamiko haya yaonyesha sio tu kudhulumiwa kwa wanawake, bali pia yaonyesha udunishaji wao. Twaweza kuwaainisha katika kundi la wanyonge - watu ambao wamenyimwa sauti na wenye nguvu. Wazo hili ladhihirika pia kwa kuutazama uhusiano ulioko baina ya Bw. Maksuudi na mkewe Tamima. Bi Tamima hana haki wala uwezo wo wote wa kujitetea dhidi ya uonevu na dhuluma za mumewe.

Lake tu ni kuufyata mkia simba angurumapo.

*BLURURUUI! foris-KENYA!  
MORAN Nyayo hujatihin Katwa  
funa*  
 Maudhui nyingine inayojitokeza ni ya malezi.

Atiijumie  
Samaki.

Inhilita

Wamesema wahenga kuwa "Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo".

Aidha, wakasema wahenga <sup>hao</sup> ~~wao~~ hao kuwa "Mtoto akililia wembe mpe".

Katika jukumu la malezi, Maksuudi ni mzazi aliyeitawala nyumba yake kwa "ufito wa chuma" (in fist) Aliitawisha jamii yake katika "Kasri la watawa". Aliwanyima watu wa nyumba yake (hasa mwanawewe Maimuna na mkewe Bi Tamima) uhuru angalau wa "kutoka" nje na kufahamu jinsi ulimwengu (wa nje) ulivyo. Unyimwaji huu wa haki (hasa kwa vijana wanaokua) huleta madhara makubwa hatimaye maadam sharti mtu ajifunze mema na mabaya na ajue kujiamulia chungu na tamu kutokana na tajriba ya kilimwengu. Kwa mfano, tunamuona Kazija anaweza kuimudu dunia kwa kutumia ujanja na ujeuri-mambo ambayo yatokana na tajriba yake. Tajriba hii imempevusha na anaelewa vizuri jinsi ya kukabiliana na kupambana na Bw. Maksuudi;

Sikiliza, dunia hii hayendi bila ya pesa.

Unapokuwa ukii ----- Unapokuwa kiongozi piga kelele. Taja kila kitu lakini unapopata nafasi ya kula kula! Na mwanamke mwepesi wa kuliwa. (uk. 12). <sup>ujani usi</sup> <sup>to</sup> <sup>edible</sup> <sup>kusus</sup> Kazija anaendelea na kusema kwa kejeli na ubeuzi;

Na huyu ndiye mtetezi anayetazamiwa kugombea uchaguzi. Huyu ndiye atakayechukua maisha

ya wanyonge mikononi mwake. (uk. 12)

Maneno haya na mengine mengi ayasemayo Kazija yatuonyesha dhahiri shahiri kuwa mwandishi anamtumia kama sauti ya kuwatetea wanyonge; lakini jambo hili litachunguzwa kwa tafsili zaidi katika sura ifuatayo ambayo itahusu wahusika.

Maimuna, "Mwari Mwafrika, mwana wa nyumba kubwa" amekosa maarifa aliyonayo Kazija. Ndiposa msanii atueleza kuwa Maimuna;

Alitaka azaliwe upya, alelewe upya, akuwe upya, asomeshwe upya, aishi upya katika ulimwengu aliokuwa kanyimwa kuishi. Alitaka aguse, ashike, avamie, aonje, ale, anywe, akoge, avae, atembee katika dunia mpya. (uk. 39)

Hamu ya "uhuru" huu imemshawishi Maimuna kuufikia uamuzi fulani. Amekata kauli kwamba ~~ana~~ budi kutoroka nyumbani ili muradi akawewe kukizima kiu ~~alichonacho~~ ~~cha~~ kutaka "uhuru". ng! *Kuch! To Kuch! J. Meserve, reas of mabn*

Maimuna si binti wa kwanza Mwafrika kudai uhuru na kutaka kuivunja minyororo ya wazazi. Msichana Tatu katika Wakati Ukuta vile vile aliudai uhuru huo huo. Wengine ni kama vile Cheja katika Hatia; Pili katika Doa La Mauti; Rosa katika Rosa Mistika; Riziki katika Uasi; n.k.

Unyakuaji wa "uhuru" wa namna hii huleta sio tu utengano, bali pia migogoro na migongano baina ya kambi hizi mbili - jadi na leo.

Swali kubwa katika kazi hii ni iwapo Maimuna aliasi kwa Maksuudi au iwapo hakuwa na jingine la kufanya. Je, nani mwenye hatia, ni Maimuna au babake? Ikiwa ni Maimuna, je, alirudi zizini kuutaka msaada kama alivyofanya Tatu?

Katika kesi baina ya Rosa Mistika na babake Zakaria, inayoendeshwa na hakimu (Mungu), kila mmoja anamulaumu mwenzake kuwa ndiye mwenye hatia. Mpaka sasa hatujui ni nani mwenye hatia. Tungali twangoja uamuzi wake hakimu mwenye busara (Mungu). *"escapist theories"* <sup>twamble basi wewo</sup>

*sana Jamii* <sup>note</sup> *Jisu-ni Rosa Njekosa* <sup>itzg</sup> Tatizo hili la malezi lingaliko mpaka sasa, na <sup>zakaria</sup> <sup>naye?</sup> uamuzi haujatolewa iwapo mtoto ahitaji uhuru au ahitaji kutawishwa na kufungiwa ndani chini ya sheria kali za wazazi wake.

Maudhui nyingine ndogo ndogo ni kama vile siasa, <sup>ku baya</sup> <sup>lito wos</sup> <sup>timaudhui</sup> <sup>mibinyi</sup> <sup>kidogo kid</sup> dhuluma, uonevu, mabadiliko, hadaa za dunia, mvutano baina ya ulimwengu (maisha na mnyonge), n.k.

Baadhi ya maudhui haya yanaingiliana, kwa hivyo itakuwa ni kujirudia kuichukua kila mojawapo na kuijadili.

2:3 WAHUSIKA

Wahusika ni viumbe ~~vya hadithini~~ <sup>is this intellectual honest</sup> <sup>state where</sup> <sup>forget this</sup> <sup>Yale University</sup> <sup>Umbi</sup> <sup>wa kipekee katika kuiendeleza maudhui ya msanii.</sup> <sup>Yamia lugha pevu imtu wa m.a. mima</sup> <sup>na lugha ni Kama ya undergraduate Kwanza</sup> <sup>umaarufu mwingi iwapo wahusika hao watasadifu kwa yale</sup> <sup>yaliyodhamiriwa na mwandishi. Kumchora au kumuumba</sup> <sup>mhusika ni kumjenga kutoka mwanzo hadi mwisho kwa</sup> <sup>kumpa umbo, wasifu, tabia n.k.</sup>

Kuwepo kwa wahusika kwategemea sana jinsi msanii aezavyo kuwa umbi. Huweza kuwa ~~na~~ wasilisho la watu awajua ambao amevutiwa na umbile na tabia zao ngeni au za kutatanisha; mbaya au nzuri, zenye kuvutia au kukirihi. Huweza kuwa viumbe ambavyo anewasikia wenzake wakiwasimulia na kwa hivyo huwaumba katika mawazo ya kusimuliwa. Huweza kuwa ni watu ambao kuwepo kwao pamoja na hulka zao amesoma katika vitabu au majarida fulani. Pia huweza kuwa hata watu wasio sura maalum, watu wasiopata au wasioishi katika dunia hii kwa sura wala umbo; watu wasio na majina Ali na Asha, bali ni watu anaowabuni msanii katika kipawa chake cha kubuni kwa mchanganyiko wa maarifa na uzowefu wa maisha na matukio yake.

Lakini mara zote, mhusika kama Dude na Zuberi wa Asali Chungu, <sup>had</sup> <sup>ambao wa</sup> ni mhusika ambaye amehusishwa kwa maisha halisi ya jamii aichorayo msanii. Kama ni mnyonge

anayeonewa, basi anawakilisha wanyonge wanaoonewa; kama ni bwana - mkubwa mwonevu anayeonea basi anawakilisha waonevu wanaoonea.

Msanii aweza akawachora wahusika kwa kutumia majina ya majazi. Mtindo huu umezingatiwa sana na Shaaban Robert katika maandishi yake. Kwa mfano, tunapata wahusika ambao majina yao yanaoana na tabia na mienendo yao. Wahusika hao ni kama vile; Karama (mwenye ukarimü), Utubora (mwenye sifa za utu na hulka njema), Makuu (mwenye kujitakia makuu), Radhia (mwenye tabia za kuridhia), Majivuno (mwenye majivuno) n.k.

Dude anayeelezewa katika Asali Chungu si Dude maalum kwa maana ya Dude ye yote tunayemjua; wala si Dude aishiye Unguja, bali ~~ni~~ Dude wa hadithini ~~Kuniga?~~ <sup>Kul COPY</sup> anayejaribu kukopi tabia ya mtu au watu wanaopatikana <sup>Wacha utoto (our guy! we we)</sup> ~~kukopi~~ <sup>shere</sup> katika jamii ya mwandishi.

Juu ya wahusika, S. A. Mohamed yuasema;

Wahusika wangu mara nyingi hutokana na lile kundi linalonyimwa ambao huonyeshwa wana mvutano na lile kundi linalonyim<sup>a</sup>.

----- Wahusika wangu katika riwaya ni vivuli au masanamu yanayosema na <sup>z</sup> kujibishana katika maandishi. Hutenda mambo na kutendana na kuisukuma riwaya



kuendelea mbele katika kutendana kwao.

Viumbe hivi huvinu na kuvizaa na  
kuviachia vikue kimwili, kiroho, kimawazo,  
kijamii, kiutamaduni, kisiasa, kielimu na  
kisaikolojia.<sup>10</sup>

Wahusika ni wa namna mbali mbali. Kuna "nguli"  
ambao ni wahusika wakuu na ambao huwakilisha "values"  
(ujumi za jamii).

Pili kuna "wakinzani" ambao ni wahusika katika  
fasihi ambao wanapingana na "nguli" kwa vitendo,  
mawazo, tabia n.k.

Tatu kuna wahusika wengine ~~wadogo~~ wadogo ambao  
pia ingawaje hawazungumziwi sana riwayani wana umuhimu  
wao katika jukumu la kiumba riwaya. Wahusika wa  
kiwango hiki hutumika kama viungo vya matukio na vitushi  
mbali mbali vya riwaya.

Katika riwaya ya Utengano, ingawa kuna wahusika  
wengi sana muhimu, tutawachukua wahusika watatu kama  
vielelezo katika kuiendeleza maudhui. Wahusika hao ni  
Bw. Maksuudi, Kazija na Maimuna. Yaaminika kuwa katika  
kuwashakiki na kuwanakidi wahusika hawa, bila shaka  
tutaweza pia kuwashunguza baadhi ya wengine. Mhusika  
mmoja hawezi kukuzwa kikamilifu pasipo kuhusishwa na  
wengine.

Kabla ya kuwaingilia wahusika hawa, mmoja baada

ya mwingine ingefaa kutajwa kuwa zipo njia nne muhimu zinazotuongoza katika kuzijua sifa za wahusika. Njia ya kwanza ni jinsi mwandishi anavyosema <sup>m Sakini</sup> juu yake. Pili, jinsi watu wengine wasemavyo kumhusu, tatu, jinsi anavyosema yeye mwenyewe na mwisho, twaweza kuzifahamu sifa za mhusika kutokana na vitendo vyake.

Kazi hii itazingatia mbinu hizo nne katika uchambuzi wa wahusika.

2:3:1 MAKSUUDI *(Intentionally? Silly!  
purposely)*

1 Jina lenyewe latuonyesha kuwa ni la majazi.

Katika Kamusi, neno "Maksuudi" lina maana;

*Mawenzi* Kwa kutilia nia; kwa kudhamiria: k.m.

*Mawenzi* (Amenipiga kumbo maksuudi).<sup>11</sup>

Lina maana hasa ya kulifanya jambo siyo kwa sadfa bali kwa kukusudia na kwa kuwa na nia na dhamira ya kulifanya.

Katika ma-sala ya jamii, Maksuudi anawakilisha jamii za kikabaila na kibwanyenye. Ni wakilisho pia la uovu wa jamii na vile vile jamii ya wanyonyaji na ya "mwenye nguvu mpishe".

*Nanooja fizi*

Kutokana na pato lake cheo na mamlaka, Maksuudi ametumbukia katika lindi la ubinafsi, uafriti, uroho na dhuluma. Anamhini na kumhaini mkewe, bintiye <sup>(Maimuna)</sup> Kazija, Mwanasururu, Bitikocho na vile vile ametengana

na nduguye Fadhili. Amefarakana takriban na kila kitu, dunia, nafsi yake, jamii yake n.k.

Bila shaka msomaji ashangazwa na mabadiliko yanayomkumba Maksuudi ambaye twaambiwa kuwa;

Kweli Maksuudi alikuwa mchochole na ni wazi kwamba anatokana na ukoo wa kifanyakazi na kikulima. Ni kweli kwamba hapo kale imani yake ilikuwa thabiti. Alikuwa mtetezi wa haki na kiongozi shupavu, mpaka dakika ya mwisho. Yeye ndiye aliyekuwa miongoni mwa waasisi wa Chama Cha Mwafrika. Naye alijitolea kwa nia, mvua na juu, panda shuka, nenda rudi. Kifungo, vitisho na visasi vya watawala, vyote havikumsh tua wala kumrejesha nyuma. Alitaka kuona kwamba nchi yake inajigomboa, na wanyonge, wafanyakazi na wakulima wanajitawala. (uk. 17).

Baada ya harakati za kupigania uhuru, Maksuudi alifadhiliwa kwa kupewa madaraka na wanyonge. Alichaguliwa kuwa mkuu wa wilaya na vile vile wa chama.

Na hapa ndipo alipata fursa ya kupaa mbinguni pasipo kutafakari na kufahamu kuwa, "angenda juu kipungu hafikilii mbinguni".  
[Y] Silly!

Alianza kuota mabawa na kuibadili mienendo yake. Alianza kuwa mchoyo na kutaka kumiliki kila kitu

duniani. Hizi neema za raha, starehe, anasa, cheo, madaraka na wadhifa ndizo chanzo cha uovu wake.

/Alianza kuutumia wadhifa na mamlaka yake kwa kuwanyanyasa watu kama vile Kazija ambaye anamtumia kama chombo cha ~~kukinaishia~~ shauku na uchu wake wa kimwili.

TV Nyati h  
oh no-not again!

Maksuudi si kiumbe wa pekee mwenye sifa za namna hii. Wako viongozi wengi ambao wakishapata bahati ya kupanda ngazi huwapa kisogo kabisa wale waliowasaidia kwa kuzishikilia padio za ngazi zilizokuwa zateleza.

Kenya soon  
not yet  
not yet  
not yet  
not yet  
not yet  
not yet

Mifano ya viongozi kama hao imezagaa sio tu katika

maandishi bali pia katika maisha ya uhalisi, hasa katika mataifa mengi ya bara la Afrika. Twaweza hata tukawaona viongozi arba <sup>wa sababu hewa ni</sup> wamejitwalia madaraka mengi na nguvu zisizo kikomo. Watu hawa wanapofanya vitimbi

(KANU government) vyao hivi hawakumbuki kuwa kila lililo na mwanzo, sharti liwe na mwisho wake. Wanaendelea kujilimbikizia mali huku wanyonge wanaowatawala wakizidi kuungulika katika lindi la umaskini. Katika serikali za Afrika, uonevu huu umewanda tangu viongozi wa daraja za chini kama vile machifu hadi marais. Viongozi wengine hata huvuka

viwango vya uanadamu na kuwa <sup>kama</sup> nduli kwa ukatili wao.

12 min w/w UK. Binot the killer! - total man + the bull.  
From mere teacher to president - mpi

Katika upande wa fasihi tunao wahusika ambao sifa zao zimelandana na zile za Maksuudi. Katika Dunia Mti Mkavu kwa mfano, tunakumbana na Fauz ambaye sifa zake

→ from a U.T to presidency - surely!  
Yet Prof's have no place.

ni za "Mzungu mweusi". Tunashuhudia jinsi anavyoiteketeza jamaa ya Jaku kwa sababu anataka kuyalinda maslahi yake. Anawanyonya nguvu zao na kuwaacha wakiwa dhalili katika dunia ambayo pia ni uwanja wa fujo.<sup>13</sup>

*1300re Kutumie maneno yako mwongozo ala "Uwesasi" - S<sup>1</sup>n, mtakatifu Sikosha Kito.*

Katika Nyota Ya Rehema, M. S. Mohamed amemchora <sup>Ny  
wachia  
ukabila</sup> Fuad kama wakilisho la ukabaila na ubwanyenye katika <sup>from  
a duror  
warped  
mind</sup> jamii za Kinaizi. Licha ya kumdhulumu Rehema <sup>Respect  
individual  
entities</sup> kisaikologia, kihisia na kiakili, <sup>Fuad au Karim?</sup> anampokonya kishamba chake ambacho ndicho tegemeo lake la kipekee baada ya kuponyokwa na wazazi na wafadhili wake. Ameachiwa dunia imwongoze kwa jaha yake.

Zuberi ni katili mwingine anayelisukuma gurudumu la dhuluma. Ushari wake umeelezewa kinagaubaga katika riwaya ya Asali Chungu.

Baadhi ya wahusika walotajwa hapa watashughulikiwa kikamilifu katika sura nyingine. Wametajwa hapa tu kwa minajili ya kuzitilia nguvu sifa za Maksuudi.

✓ Kwa kiasi kikubwa, mwandishi amemtumia Kazija kutumulikia na kuzinadi hizaya za Bw. Maksuudi. Analibeua tabaka la viongozi ambalo haki laigeuza kuwa haramu, na tamu walifanya chungu. Maksuudi, anayetarajiwa kuwaongoza watu katika haki na maadili mema anawaongoza katika maangamizi.

Aibu ya kwanza anayoipata ni ile ya kumfumania  
Kazija akichezewa na mwanawe Mussa. Hapa yaonyesha  
kuwa Mussa pia ameanza kuingia katika mkondo wa nyayo  
za babake. (Repetition)

Njama ya baba kumfumania mwanawe, iliyopangwa na  
Kazija ilikusudiwa kuonyesha kuwa Maksuudi ni mtu asiye  
mwaminifu kwa mkewe na vile vile ni kiongozi asiye na  
hulka njema. Tamaa zake zamuegemeza katika ulimwengu  
wa anasa, na ni katika hali hii anaposababisha utengano  
nyumbani kwake. Ameshiriki anasa kiasi cha kuwa  
amewasahau raia waliompa madaraka akawa mkuu wa wilaya,  
kiongozi wa chama, mkurugenzi wa shirika la Bima la  
Taifa. Anaishi katika jumba la fahari lenye "kimo",  
"heba", "uzuri" na lenye "taa za thurea".

Isitoshe, amekuwa mla rushwa, hatua ambayo  
inasababisha mporomoko wake.

Maksuudi ana uovu usio mwisho. Nyumbani kwake ni  
katili mkubwa. Hili laonyeshwa na jinsi anavyomtesa  
mkewe akiwa katika hali ya ujauzito na vile vile baada  
ya kujifungua. Amesababisha kufarakana kwake na Bi  
Tamima, Maimuna, Mussa, Mwanasururu na wengineo. (Kina nani?) Eba  
Somu

Kama asemavyo Muyaka, "Usione kwenda mbele, kurudi  
nyuma si kazi".<sup>14</sup> Maisha ya Maksuudi yalianza kuingia  
mushkili pale alipoanza kushiriki katika mambo ya  
magendo na rushwa. Alikuwa ajichimbia kaburi na kujitakia

msiba ambao hauna matanga. Kutokana na ushari huu,

S. A. Mohamed atufunza kuwa hakuna refu lisilokuwa na ncha. Aidha anaiendeleza itikadi yake kuwa mahali pasipo na haki, hata amani haipatikani. — *mamdiso* — *ameridoo* — *wape runi* *wewe?*

Kutokana na kesi ya jinai inayomkibili Maksuudi, anashikwa, kutiwa pingu na kuhukumiwa kifungo. *Ole* — *Hakuna haj* *Kuleta* *hisia* *Zalio haj*  
*wake Mheshimiwa Bw. Maksuudi!* Maisha yake baada ya kutoka jela yafanana na ya Mchochole. Mamlaka hana tena, utukufu umemtoka na hali yake ni ya kusikitisha. Amekonda kama unyasi kwa vile nafsi yake iliendelea *Kerani* *Tumaoa q?* kumchimba.

Juhudi zake za kuujenga ukuta hazikufanikiwa kwa vile alishindwa kuziba ufa awali. Imekuwa ni vigumu kuipatanisha tena jamaa yake na anakufa kifo cha fedheha ingawaje anafanya juu chini apate ghofira kutoka kwa jamaa na marafiki zake.

Wakati maisha na neema za Bw. Maksuudi zaendelea kutumbukia nyongo, wanyonge waendelea kupata hisia mpya za mwamko, kama asemavyo mwandishi;

Penye unyonje mapambano hayeshi, na unapomnyamazisha mnyonge mmoja, ni kama kuwapalilia wengine. (uk. 51).

2:3:2 KAZIJA

Kazija ni mhusika muhimu sana katika riwaya ya Utengendo kwa vile anatumwiwa kama chombo cha kuufichua

uovu ulioko katika jamii - unaoendelezwa kwa kiwango  
kikubwa zaidi na Bw. Maksuudi.

Yeye (Kazija) ni msichana wa kisasa ambaye,  
kutokana na tajriba yake ya kilimwengu amefahamu wazi  
wazi kuwa katika jamii anamoishi upo uovu mwangi sana  
unaoendelezwa hasa na matajiri dhidi ya maskini.

Ameshafahamu pia kuwa wanawake wanakandamizwa  
vikubwa na wanaume. Kazija ni mtetezi wa maslahi ya  
wanawake. Aidha ni mkinzani wa Bw. Maksuudi kwa sababu  
matendo, mawazo na tabia za huyu wa pili zinapingana  
na kile anachokisimamia yule wa kwanza. Kazija auchukia  
uonevu, dhuluma na vile vile unyonge alionao wa kukubali  
kunyanyaswa. Sifa za Kazija zajidhihiri mwanzoni  
mwanzoni mwa riwaya ambapo hisia zake zaelezewa;

Kuna mengi ambayo Kazija anayachukia. Ndiyo,  
anachukia ----- . Kwanza, anamchukia  
mwanamme ----- . (uk. 1).

Kwa mara nyingi, Kazija amejitokeza dhahiri kumpasulia  
mbarika Bw. Maksuudi. Ujasiri huu wa "mnyonge"  
kujitokeza bila uoga kuifichua aibu ya kiongozi mwenye  
cheo na mamlaka watuonyesha ukakamavu na dhamira ya  
dhati ya Kazija kuipigania haki yake. Ni nadra sana  
kumsikia maskini akitoa malalamiko yake kinaganaga  
(mbele ya anayemdhulumu). Lakini kwa Kazija, shauri  
limekatwa na yu tayari kupigana kwa hali na mali mpaka

mnyonge arejeshewe utu na heshima yake.

Kazija ameizua mbinu ya ujanja na ulaghai ili  
aweze kufaulu katika jukumu lake - kumtweza Bw. Maksuudi.  
Ujanja huu anautumia pale anapomfumanisha Mussa <sup>ne</sup> babake.

Amepevushwa na dunia na anauelewa unyonge wa  
Maksuudi wa nafsi. Hivyo apanga kulipiza kisasi;

Leo itatosha kwa hilo aliloliandaa. Kulipa  
kisasi cha ndugu na shoga yake, Farashuu.  
(uk. 12).

Vile vile, Kazija anaufahamu udhaifu wa Bw. Maksuudi  
katika kuwaongoza watu;

Kazija aliwaza madagany<sup>a</sup>, ya viongozi kama  
hawa, viongozi ambao nje hujionyesha kuwa  
wana hisia na wananchi, na kumbe ndani kwa  
ndani ni mahaini. Na huyu ndiye mtetezi  
anayetazamiwa kugombea uchaguzi. Huyu ndiye  
atakayechukua maisha ya wanyonge mikononi  
mwake. (uk. 12).

Aghalabu, viongozi wengi watafutapo uongozi kwa  
njia ya kura hujinyenyekеза na kuipendekeza kwa raia.  
Wanatumia maneno matamu ya kurairai - ambayo hata  
yaweza kumtoa nyoka pangoni. Jambo linaloshangaza  
<sup>clinché cleric</sup>  
<sup>imechakazi (eli)</sup> ~~toa singia wasi~~  
wengi ni kuwa baada ya kuchaguliwa na kukabidhiwa  
madaraka, viongozi hawa wanawapa wananchi kisogo. Jambo

hili ni dhahiri na mifano maridhawa yaweza kupatikana katika serikali nyingi hapa barani Afrika.

M.Y. KENYA  
-KAMOTHO-  
(AINAYA FISI JIKE) Lelik  
Uche

Katika sura ya saba ya Utengano wagombea uchaguzi kadha wanajitokeza uwanjani na kila mmoja wao anajaribu kutoa sifa zake na kutoa miadi mbali mbali ili kuwashawishi wapiga kura.

Katika uwanja wa siasa, tunafahamikiwa vyema kuwa raia si wapumbavu. Wanafahamu viongozi ambao wanatafuta kura ili waende wakayajaze matumbo yao. Kwa hamasa na hasira, baadhi ya raia kama vile Mzee Japu wanawaza;

Maksuudi ----- aaa, alipokuwa mkuu wa Wilaya alikula pesa ngapi za mke wangu alipotaka kununua kiwanja cha kujenga nyumba.

.. Sahihi yake tu Mkuu wa Wilaya aliiuza shilingi mia mbili. Leo anataka mimi na mke wangu tumpe kura. Ainuke zaidi maana yake, azidi kutukalia vichwani. Tumechoka kuchezewa na watu namna hawa. Kura yangu nitampa Siwa, kijana huyu amepata sifa mionganini mwa wananchi. Sifa zake zimeenea. Kijana mkakamavu, siye yule dhalimu Maksuudi au Zanga ----- . (uk. 78)

Wanyonge ni wenye simanzi na majonzi lakini hawana wa kuwaliwaza. Inawabidi wawe wakakamavu na wazue mbinu zao za kujikomboa kutokana na dhuluma na maonevu.

Kazija, ambaye amekula yamini kumtweza na kumbeua  
Bw. Maksuudi anampaka matope mbele ya hadhara - katika  
jukwaa la siasa;

Huyu Maksuudi ambaye ameshindwa kuiendesha  
nyumba yake atawea kuangalia maslahi yetu?

----- Maksuudi aliyemwacha mkewe kwa  
kisa cha kumtorosha mwanawe ati. Mbali na  
mali aliyojilimbikia, Mnyengine ya unyang'anyi  
kwa wake zake. Amemnyang'anya mkewe mmoja,  
Mwanasururu, mali yake na mwisho akamwacha  
na kusababisha kifo chake. Mengi mengi  
----- (uk. 81)

Kujitokeza kwa Kazija kumshambulia Maksuudi  
hadnarani kwaeleza mambo mawili. Kwanza ni ujasiri na  
ushupavu wa wanawake ingawaje wanagandamizwa na wanaume.  
Pili kwaonyesha kuwa ingawaje wenye nguvu wamekazana  
kuwanyamazisha walio dhalili, hawa wa pili hawawezi  
kamwe kuzikubali dhuluma na uonevu.

Kazija ametumiwa na mwandishi kama chombo cha  
kuwazindua wanyonge katika usingizi wa ujinga. Awahimiza  
wasimame wima na wapiganie haki zao bila kukata tamaa.  
Himizo hili laendelezwa zaidi na S. A. Mohamed katika  
shairi lake (Sikate Tamaa) ambapo anahimiza mnyonge;

Umeanguka, inuka, simama kama mnazi  
Umechunika, inuka, tia dawa kwa ujuzi

Sasa <sup>inuka</sup>, kijana ianze kazi  
Sikate Tamaa. (Ubeti 1)

Una nguvu, simama, wewe upambane nao  
Una werevu, simama, uzepuke njama zao  
Usiche kovu, simama, ujifunze vumilio  
Sikate tamaa. (Ubeti 4).<sup>15</sup>

Kwa kumalizia (katika sifa za Kazija) twaweza kusema kuwa Kazija ni mhusika wa kike mwenye wajibu maalum wa kutekeleza katika kuiendeleza maudhui ya riwaya. Ni jasiri, mkakamavu na mwenye udhati katika jukumu lake. Kiumbe huyu amepewa nguvu na msanii na hachelei cho chote. Amejitolea mhanga apiganie maslahi ya wanaodhulumiwa wakiwemo wanawake akiwa yeye ni mmoja wao.

Ingawaje Kazija aonekana mwanamke (msichana) aliye na maadili yaliyolegealegea, maoni ya tasnifu hii ni kwamba, mwandishi anampa sifa zile kwa maksudi ili aweze kuubainisha zaidi uchoyo, uroho, uovu na uonevu wa Bwana Maksuudi. *Nanna gani?*

*2:3:3 MAIMUNA*

Maimuna na mamaye - Bi Tamima walikula chungu kwa pamoja pale nyumbani. Walitawaliwa kwa "ufito wa chuma" na Bw. Maksuudi katika "Kasri la watawa" kama liitwavyo jumba la Bw. Maksuudi. Jumba hilo liliitwa *na neni? na yelee!* *no mwandishi (SB Kay).*

"kasri" kwa sababu ya kimo chake, heba na uzuri uliolistahili. Watawa (<sup>si kwezi</sup> ~~watumwa~~) hawa kamwe hawakuruhusiwa kutoka nje angalau (<sup>kupunguza</sup> ~~kubadili~~) hewa. Watumishi ndio tu walioruhusiwa kuingia na kutoka.

Haieleweki vyema ni kwa nini Maksuudi aliwatenda hivi mkewe na mwanawe. Lakini yaaminika kuwa msanii amempa Maksuudi sifa za ukatili ili kudhihirisha zaidi ukatili, hiana na ubinafsi wake. Pengine vile vile, alichelea kuwa hawa wawili (Bi Tamima na Maimuna) wakitoka nje wataweza kujifunza mengi na pengine wapevushwe nayo kiasi cha kuwa wanaweza wakauasi utawala na maagizo yake. Pia, yawezekana kuwa hataki wapate maarifa kuhusu mienendo yake huko nje ambayo imejaa uovu. \* Hull ni uzuri tu. Hukungu haja <sup>to</sup> katumis <sup>Inawezelensi</sup> <sup>Lousy live.</sup> <sup>hapa!</sup>, speak out your mind, man!

Tukirejea katika sifa za Maimuna, mhusika huyu, kama tuambiwavyo katika <sup>hivimbi</sup> jalada la Utengano, ni "Mwari Mwafrika, mwana wa nyumba kubwa". Amezaliwa katika familia yenye uwezo na mamlaka. Malezi aliyoypata Maimuna utotoni yaweza yakamithilishwa na malezi ya watoto wengine kama vile Rosa, katika Rosa Mistika, Njeri katika "The Minister's Daughter", <sup>Xerax</sup> <sup>"Danayé Shemasi!"</sup> <sup>my friend</sup>. Wakati Ukuta, Cheja katika Hatia na wengineo. Wahusika hawa walilelewa katika hali ambapo ilikuwa ni mwiko msichana kutembea na mvulana. Wazazi wao (hasa baba) waliwafungia ndani katika kutaka kudumisha kaida za kiutamaduni. Lakini, aghalabu malengo yao hayakutimia

kwa vile yalikumbwa na migogoro kwa vile nyakati ziliwa zimebadilika. Jambo hili limedhihirishwa vyema katika Wakati Ukuta ambapo baba Tatu aeleza kimantiki kuwa;

A  
E-Hussein

Hakuna mtu anaweza kushindana na wakati.

WAKATI UKUTA, UKIPIGANA NAO UTAUMIA

MWENYEWE. Tutagombana na watoto wetu bure.<sup>16</sup>

Maimuna pia ni kama Tatu na ni bure babaye amfungie.

Mara ya kwanza Maimuna anapopata wazo la kuvunja minyororo ya kiutumwa (nyumbani) ni pale, kwa simanzi, anamshauri mamaye aliyepatwa na uchungu wa kuzaa.

Maimuna anatoa shauri;

Mama usifanye mchezo 'vyo. Ikiwa kuogopa

kuvunja miko ya nyumba hii, tusiogope.

Naivunjwe leo hiyo miko. (uk. 21)

Wazo hili latuonyesha kuwa Maimuna yu tayari kupinga miko ya babake ili mama yake asalimike. Vile vile latuonyesha mwanzo wa Maimuna kuanza kupata mwamko kuwa baba yake ni haini asiyejali hulka na maslahi ya wengine.

Maimuna, kwa kushawishiwa na Biti Kocho amejasiri kwenda kumtafuta mkunga atakayemsaidia mamaye katika uzazi, jambo ambalo ni kinyume cha matakwa ya babaye.

Yadhihirika pia jinsi nyumba nzima ya Bwana Maksuudi

ilivyoishi kwa hofu na wahaka kwa kuchelea hasira na vitimbi vya bwana wao. Ukatili wa Maksuudi watuonyesha shahiri dhuluma, ubinafsi, uroho na uhaini wake. (Marudw)  
Amewanyima 'watawa' wa 'Kasri' yake uhuru wa;

Anatalia had  
Kuingia na kazi  
yake inyuzi  
mwenzi.

----- Kuogelea katika hewa ya maumbile,  
----- uhuru wa kuingia na kutoka nje,  
uhuru wa mapenzi, uhuru wa kufanya kazi na  
kupata riziki n.k. (uk. 23)

Yampatayo Maimuna baadaye (baada ya kutoroka nyumbani) yatokana na taathira ya malezi mabaya tangu utotoni hadi siku ile alipotoroka. "Uhuru" aliupata, nao uhuru ule ulikuwa na madhara yake. Kule *Purni* Madongoporomoka alikotorokea kulikuwa na maisha tofauti na ya pale nyumbani. Maimuna, aliyeokuwa limbukeni katika maisha ya kilimwengu aliyaona na kujifunza mengi. Alijifunza kutokana na mienendo ya akina Biti Kocho, Bi Farashuu, na hatimaye, Mama Jeni.

Baadhi ya maisha mapya aliyokumbana nayo Maimuna ni kama vile kutumiwa kama chombo cha kufanyiwa biashara ya kimwili cha mfadhili wake - Mama Jeni. Baada ya kupokea noti, Mama Jeni amuachia mwanamume (James) apambane na Maimuna;

'Come on', James alikemea. Alikuwa taabani na Maimuna kamkosa. 'Come on', aliita James sasa kwa upole, huku akiyumbayumba. 'Sitaki', Maimuna alijikwapua na kuepa mikono ya James.

Alikimbilia kipembe chengine cha chumba.

Chozi lilikuwa kifua tele. (uk. 56)

*Kinuwa* Naam huu ndio 'uhuru' alioutaka Maimuna. Lakini hatuwezi kumlaumu bila kwanza kuchunguza kisa chake kama isemavyo katika shairi la "Wanambia Mchafu" katika Sikate Tamaa.<sup>17</sup>

*Kite Kimoja* *Kuleto ulamu wa lugha ni yeye binaa*  
Huku Maimuna alipoendelea kutopea na kuboea <sup>?</sup> katika kinamasi cha anasa, maisha ya babake yaliendelea kubadilika maadam dunia ilianza kumfunza kuwa "Mpanda ngazi hushuka". Hiki kilikuwa ni kinaya cha hali ya juu baina ya baba na bintiye. Katika zile raha zake, Maimuna ameamua kuwa kitu cha kwanza cha kutilia maanani ni pesa. Iwapo itakuwa kwa halali au haramu, pesa lazima azitafute. Ameufikia uamuzi huu baada ya kutambua kuwa ameshajisaga na kujitumbukiza katika shimo chafu asimoweza kutoka - Dunia. Anasafiri katika mtumbwi mmoja na Dora - msichana mifikiye aliyeendewa kombo na maisha baada ya kuachwa katika hali ya upweke na ulitima wazazi wake walipoiaga dunia. *Monyo - mmoja - alimka bidhi - mimi jeni - no lantoloneko*

*2*  
Ulitima unaoonyeshwa na wahusika hawa ni kielelezoo cha jinsi watu wasiokuwa na uwezo (wa kiuchumi au wa kisiasa) wanavyodhalilishwa. Maimuna ni mnyonge kwa kule kutokuwa na maarifa ya kutosha kuweza kuimudu dunia na kujikimu mwenyewe. Bi Sururu, Biti Kocho, na Farashuu nao wanakutumia kule kutopevuka kwa Maimuna

ili kujilipizia kisasi kutokana na kifo cha Mwanasururu, mwanawe Farashuu. Basi hapa, twaona kuwa Maimuna anajikuta katika ulimbo ulioandaliwa kutokana na maovu aliyoyatenda Maksuudi babaye. Kwa hivyo, licha ya kusema kuwa Maksuudi ndiye aliyesababisha utengano nyumbani kwake, imedhihirika kutoka riwayani kuwa kuna kisasi ambacho kundi fulani wamekula yaamini kukilipiza dhidi ya Bwana Maksuudi na jamii yake nzima. Maimuna, kama mamaye na nduguye Mussa, anaangukia katika mtego huu.

Mtu wa kwanza kuuchochea utengano huu ni Kazija - pale anapomfanya Mussa akosane na kufarakana na babaye Maksuudi. Wengine ni Bi Farashuu, Biti Kocho na Mama Jeni ambao wanahakikisha kuwa utengano umetokea baina ya Maksuudi, Bi Tamima na Maimuna.

Utengano huu wamfanya Maimuna aipoteze hadhi yake na kuwa mtu wa hali ya chini ambaye ajipatia riziki kwa njia yo yote ile. Amekuwa mtu wa kuwatumbuiza watu vilabuni na mahotelini, kama inavyodhihirika katika tangazo lifuatato;

#### RUMBALOLA HOTEL

----- Fika, fika, fika ujionee, msakato wa Maimuna. Maimuna Maksuudi, Gwiji wa Nataki na nyimbo ----- (uk. 109)

Vitendo vya Maimuna kwa ujumla vyatuonyesha jinsi

kiumble (mwanadamu) ajikutapo katika hali ambapo hana uhakika kuhusu maisha ya baadaye hutia kani na kujiandaa kupambana na mazingira, muradi aweze kuishi kama wengine. Lazima azizue mbinu mpya za kuweza kujikimu ~~kwa~~ malazi, mavazi, chakula na starehe nyingine azihitajizo binadamu.

Maisha ya namna hii humpa mtu roho ngumu ya ukatili na huwa hajali litakalotokea atendapo baadhi ya mambo.

Maimuna amekataa katakata kumghofiri babaye ambaye kufikia kifo chake (Maksuudi) maisha yake yalitumbukia katika simanzi na kiherehere.

Mabadiliko katika maisha ya Maimuna na ugumu wa moyo wake waonekana dhahiri shahiri katika maneno yake anapomfokea babake mzazi;

Miiimi, mimi mwanaao? <sup>Nini</sup> Mimi unanihitajia?

Wewe nani? Miiimi, mimi nirudi -----.

Hata nikirudi ----- hata nikirudi -----

----- tokeni, tokeeeeeeni. ----- Sogea

hatua moja tu, kama huitaki roho yako.

Utanijua sasa hivi kuwa mimi siye tena  
Maimuna boza. Nyinyi ndio mlionibadilisha  
hivi. Nyinyi na dunia. Tokeni. Nasema  
tokeni. Tokeeeeeeni.

Mapambano ya Maimuna dhidi ya Maksuudi babaye ni taashira, dhihirisho na wakilisho la mapambano dhidi

ya uonevu wa wenye nguvu. Walioonewa wana imani kuwa wataikata minyororo ya utumwa na kuzimaliza nguvu za wadhalimu.

Kitendo hiki cha Maimuna vile vile kimeoana muafaka na matendo ya wafanyakazi na wakulima wa kiwango cha chini wanaonyanyaswa ambao wameshikana kwa umaja kuzipinga dhuluma za wazi. Yatumainiwa kuwa mapambano haya yataweza kuiletta haki na usawa kamili miongoni mwa binadamu katika jamii.

#### 2:4 MUUNDO WA JAMII KATIKA UTENGANO

Ngugi wa Thiong'o amesema katika makala yake yaitwayo "Literature and Society" kuwa kiini cha jamii yo yote ile ya wanadamu ni uchumi, siasa, utamaduni na hali yake ya kijamii,<sup>18</sup> Ameendeleza maoni yake kwa kusema kuwa jamii nzima imejigawa katika "mataifa" mawili makuu - wanaonyanyaswa na wanaonyanyasa. Maoni haya yanakuubiana sana na ya Karl Marx aliyesema kuwa jamii nzima imegawanyika katika makundi mawili ambayo aghalabu yanapingana; yaani - mabwanyenye na <sup>have notes</sup> <sup>lou workers</sup> <sup>has</sup> <sup>proletari</sup> <sup>Peasants</sup> <sup>mafalaki</sup> <sup>Kenya</sup>.<sup>19</sup>

Tunapoongea juu ya mabwanyenye tunamaanisha lile kundi la watu katika jamii lililo na uwezo wa kiuchumi, kisiasa na kijamii. Kama tuambiwavyo na Hussein (1971), watu hawa wana uwezo, ubaya na wema. Vile vile wana uwezo wa kujenga, kubomoa na kutukuza.<sup>20</sup> Kwa mfano, mhusika mmoja katika Mashetani anajitapia mhusika mwingine, aliye duni kwa kusema;

yaf. Louis XII

Mimi ni nguvu na nguvu ni mimi. Mimi ni  
uwezo na uwezo ni mimi.<sup>21</sup>

Hawa watu wenye uwezo ndio waliomiliki mali,  
ras~~imali~~, ardhi n.k. Kwa hivyo, wanyonge hulazimika  
kuwanyenyekia ili wao pia waweze kupata angalau  
mahitaji muhimu - ya kila siku.

Lakini ingawaje wanyonge wanaonewa na kudhalilishwa,  
wao wana imani kuwa hatimaye wataushinda uonevu na  
ukandamizaji katika jamii. Kwa mfano, katika Wema  
Hawajazaliwa, mhusika mmoja yuasema;

Wale waliobarikiwa mamlaka na mwendo wa  
kasi wa tai na wapeperuke mwanzo. Waache  
waende.. Nitatembea polepole na nitafika  
pia.<sup>22</sup>

Katika jamii ya Utengano, msanii atuchorea jamii  
mbili kuu zinazopingana, Jamii zenyewe ni za kikabaila  
(kibwanyenye) na za kikabwela (maskini). Jamii ya  
kikabaila imewakilishwa na Bwana Maksuudi hali ile ya  
kikabwela imewakilishwa na wahusika wengine kama vile  
Kazija, Biti Kocho, Bi Farashuu n.k.

Ili kutoa ithibati zaidi tutaigawa sehemu hii  
katika jamii au tabaka mbili.

2:4:1 TABAKA LA KIKABAILLA

Kama ilivyosemwa hapo juu, tabaka hili ndilo

limemiliki rasilmali na aghalabu huishi katika starehe na anasa - kutokana na jasho la lile kundi jingine la maskini ambalo ndilo hushughulika katika uzalishaji wa rasilmali hiyo. Kwa kuyachunguza na kuyanakidi maisha ya Maksuudi, hali na mienendo ya tabaka hili itabainika.

Kabla ya maisha ya Maksuudi kutumbukia nyongo, inadhihirika kuwa aliishi maisha ya ulimbwende <sup>romanticism?</sup> alipokuwa kiongozi wa chama na vile vile mkuu wa wilaya. Vile vile, aliwahi kuwa mkurugenzi wa Shirika la Bima la Taifa. Alikuwa na magari, watumishi, mashamba n.k. Twaonyeshwa haya na maneno ya mwandishi;

Gari la aina ya Cortina lilikuwa likingojea mbele ya mlango wa jumba moja kubwa la ghorofa. (uk. 18)

Maneno haya tayari yatuonyesha kuwa Maksuudi alikuwa tajiri mwenye mali na majumba ya ghorofa.

Dereva wake aendelea kueleza jinsi alivyoshughulika kumhudumia Bwana. Alienda marikiti kununua "nyama ya Bwana". Aliporudi akatumwa kwa dobi kuchukua "nguo za Bwana". Tena akaenda kununua sanduku la bia akadipeleka kwa Kazija, akamfungulia Bwana mlango wa gari aingie n.k.

Maisha haya ya ulimbwende yadhihirisha kwamba utumwa na ukoloni havijatoweka. Afrika bado twatawaliwa,

lakini twatawaliwa kwa mlango wa nyuma.<sup>23</sup>

Ingawa Maksuudi alikuwa mtetezi mashuhuri wa Chama cha Ukombozi, hakupigania maslahi ya walio wengi. Alipigania maslahi yake mwenyewe na matunda (ya uhuru) aliyoypigania ndiyo anafurahia wakati huu.

Mienendo ya Maksuudi yadhihirisha alivyo sema Freire (1968) kuwa;

Hawapendelei mabadiliko ili kuwafanya watu wawe huru. Wanataka kujinyakulia na kumiliki mashamba, au kwa usahihi zaidi, wawe mabwana wa wafanyikazi wengineo. (Tafsiri <sup>yeku</sup> yangu)<sup>24</sup>

Jambo lingine linaloonyesha kuwa Bw. Maksuudi amejikengeza <sup>sh</sup> na kujitenga na wananchi (ambao katika enzi za ukombozi alidai kuwa anawapigania) ni lile jumba lake la fahari na utukufu. Lilikuwa na heba na uzuri na vile vile lenye ukubwa usio kifani. Jumba hilo lilikuwa na kimo kikubwa kiasi cha kuwa ukigongagonga mlango kwa mkono <sup>a</sup>uitikiwi kwa vile ni muhali kusikika. Inambidi mtu aibonyeze <sup>Kitime</sup> ~~Kitende~~ <sup>obs</sup> swichi ya kengele ili iite ndani - kama alivyo fanya Inspekte Fadhili alipofika nyumbani kwa Bwana Maksuudi kuonana naye. Mandhari ya ukumbi huo inayatia macho nuru, maadam mlikuwemo na;

Sofa seti aina tatu, zote kutoka Ulaya, <sup>R</sup>adio gramu, televisheni <sup>nchi</sup> ishirini na

sita, mapambo, zulia jipyा, picha za mkono  
zilizotoka Ulaya, teprikoda yenye mabomba  
mawili detachable n.k. (uk. 71)

Nyumba hii yaweza kumithilishwa na nyumba za  
wafalme wa Pate katika karne za zamani (K.18) kama  
tuelezwavyo na S. A. Nasir (1939);

Nyumba zao mbake zikinawiri  
Kwa taa za kowa na za Sufuri  
Masiku yakele kama nahari  
Haiba na jaha iwazingiye.

Kumbi za msana zakilivuma  
Na za masturi zikiterema  
Kwa kele na waja na za khudama  
Furaha na nyemi zishitadiye.<sup>25</sup>

"Taa za kowa" katika beti hizi zaweza kufananishwa  
na "taa za thurea" katika Utengano.

Muundo wa namna hii ya maisha wadhihirishwa na  
tabia na mazungumzo yake Bw. Maksuudi. Aongea kwa  
kiburi na fahari na pia majivuno. Maksuudi ni mmoja  
wa watu wachache ambao wameelimika na kupata neema.  
Yeye ni Mkoloni - mamboleo kama alivyo baba Kitaru  
katika Mashetani. Tabia na mienendo yake yajidhihirisha  
kutokana na jinsi anavyozungumza na Bwana Smith kwa  
simu;

Haloo, nani? Aha, Mr. Smith ----- ni wewe. Nilikutarajia. Nilikuwa nakusubiri kwa hamu. Ndiyo ----. Nitafanya kama ulivyoagiza. Nitamlipa, yah, nitamlipa. Lakini kesi yake mbaya ----- kwa kweli taabu kupata fidia lakini nitafix ----. Fifty fifty, okay? Ndiyo -----. Na hii kesi hatari. Polisi wameanza kutia shaka, yaani kuwa nakupeni haki ingawa hamna haki, lakini never mind. Money speaks, money is everything. Okay, tomorrow ----- bye -----. Okay. (uk. 72)

-----Now, now, now ----- tusije huko tena, usinitie kwenye ----- eee, no. (uk. 74)

Maneno mengine yanayoonesha kiburi cha Maksuudi ni yale aliyyoyatamka katika "Uwanja wa Uhuru" alipokuwa akita~~ka~~<sup>Kwenda</sup> kuchaguliwa<sup>Bungeni</sup>. Lakini kabla ya Maksuudi kuianza hotuba yake, mwandishi atueleza;

Zamu ya Maksuudi ilifika. Alisimama kwa heba kubwa, kicheko mdomoni na bashasha zinamfufurika. Alijipa moyo kuona vile alivyozoea midani hii. Jukwa<sup>a</sup> analijua uzuri, kusema anasema kwa furaha, heba yake, utu-uzima wake, uhalisi wake katika chama, yeche muasisi. (uk. 79 - 80)

Katika hotuba alisema;

Mabibi na mabwana ----- Maksuudi si  
mgeni kwenu -----  
Mnahitajia mtetezi kama mimi. (uk. 80)

Mtindo wa aina hii wa kuongea si mgeni kwa watu  
wa tabaka la Maksuudi. Wanahitaji msaada wa raia  
wale wale wanaowanyanya, na vile vile hawataki  
kubadili namna ya kuongea iwe kama wanabembeleza,  
kwa vile kufanya hivyo ni kuiteremsha hadhi yao.

Ni baada ya hotuba aliyoitoa Bwana Maksuudi ambapo  
mhusika mmoja (mkinzani) aitwaye Kazija ameamua  
kumpasulia mbarika bwana huyo. Jambo hili laonyesha  
kuwa wanyonge wamejiandaa barabara na mapambano dhidi  
ya mabepari wanaowanyonya na kuwafyonza damu. Wameamua  
kupigana mpaka warejeshewe haki, usawa na utu uliopotezwa  
na viongozi hao dhalimu. Wanataka (wanyonge) warejeshewe  
mashamba yao na wapate manufaa ya jasho lao. Lazima  
wajikomboe kama asemavyo Freire (1968);

Jukumu kubwa kabisa la kiutu na la kihistoria  
kwa wanaokandamizwa ni kujikomboa wenyewe  
kutokana na ukandamizaji (Tafsiri <sup>yetu</sup> ~~yangu~~).

----- Ukombozi hauna budi utokane na  
wanaokandamizwa wenyewe pamoja na wale  
wanaowaunga mkono kwa dhati ili kuurejesha  
utu wao.<sup>26</sup>

Katika Utengano mwandishi amtumia Kazija kuonyesha

kuwa mahali pasipo haki mapambano hayaishi, kama vile tuelezwapo katika riwaya;

Penye wanyonge mapambano hayeshi, na unapomnyamazisha mnyonge mmoja, ni kama kuwapalilia wengine. (uk. 51)

#### 2:4:2 TABAKA LA MAKABWELA

Kabwela, kama olivyoelezewa na Kamusi ya Kiswahili Sanifu ni;

Mtu wa kawaida asiye na pato kubwa au aliye ~~wa~~ hali ya chini; mwananchi wa kawaida.<sup>27</sup>

Katika jamii ambazo zimegawanyika kitabaka, tabaka hili huwa ni la watu ambao wamenyanyaswa kiuchumi na kisiasa. Baadhi yao ni wale ambao hawana kazi za kuajiriwa au wale ambao wameajiriwa kazi duni. Mapato yao hafifu huwa tu ni ya kijungu <sup>Jins</sup> meko <sup>ai</sup>, Aghalabu watu wa aina hiyo huishi katika hali ya chini kwa namna zote kama vile, mavazi, malazi, chakula, maskani n.k.

Wale ambao hujizatiti ili kuziinua hali zao hujikuta wana vizingiti (vikwazo) mbele yao navyo vikiwa ni wale matajiri. Kudhihirisha haya twaweza kuangalia vitendo <sup>Karin</sup> vya ~~Fuad~~ <sup>Karim</sup> katika Nyota ya Rehema. Huyu <sup>Karim</sup> Fuad alikuwa ni mnyakuaji na mhaini mkubwa. Yeye ni tajiri mwenye mali <sup>Karim</sup> lakini kamwe haridhiki. Anamfuatilia Rehema na

huyn hi Karim bwang mbanga wakanganyika hiro na hata Profes walle hevez kuna. Wote nongwe tu! Sisi wafadhili

Itayoni Kainu  
Adyu Kaunde!  
Chunguze  
Tenzi - Hat  
- 55 -

kumnyang'anya kijishamba chake alichokirithi kutokana  
na jamaa zake.

Fred

Hali hii ya uroho na kutoridhika imeenea sana  
hasa miongoni mwa makabaila na mabepari ambao wanataka  
kujilimbikia kila kitu, ili waweze kuzigharimia starehe <sup>mou</sup>  
na anasa zao. Itaonekana pia kuwa wanyonge wawa hawa  
wanaonyanyaswa na matajiri ndio matajiri hao  
wanaowategemea kuwalisha na vile vile kuwastarehesha.  
Wakulima hulima, lakini mazao hawajui huenda wapi.  
Dhana ya namna hii imejitokeza katika shairi lake Said  
Ahmed Mohamed (1980) liitwalo, "Ajabu". Katika beti  
tatu za shairi hili, mshairi asema;

Ajabu ajabu hii ajabu

Wanaolima hawali

Wasolima wanakula

Hula viso vya halali

Nguvu pia na fadhila

Ajabu ajabu hii ajabu

Wachokao hawalali

Walalao ni wazima

Hulala pema pahali

Na huku wakikoroma

Ajabu ajabu hii ajabu

Watenda si muhimu

Wasotenda watukufu

Wao ni watu adhimu

Kila siku twawasifu. <sup>28</sup>

Beti hizi zinaeleza kinagaubaga kilio cha kundi fulani la watu ambao wanadhulumiwa wazi wazi. Watu wawa hawa ndio ambao walipigana kwa hali na mali nyakati za kikoloni huku wakitumainia kuwa watafika "Jerusalem mpya"<sup>29</sup> ambako watastarehe na kusherehekea matunda ya jasho lao. Lakini matumaini yao yamekuwa kinyume.

Katika jamii ya Utengano, uonevu wa namna hii umekithiri na tunawaona wahusika mbali mbali wakiwasilisha malalamiko na hisia zao kwa njia mbali mbali. Kazija kwa mfano amechoshwa na jamii na basi hana budi kuichukia. "Anaichukia jamii" kwa sababu ya uonevu wake na kutodhamini usawa na haki.

Jamii hiyo ni jamii ya "mwenye nguvu mpishe", jamii ya kikabaila na kibwanyenye. Ni jamii inayo-wakilishwa na watu kama Maksuudi waliojaa uovu na zinaa. Mfumo wa jamii hiyo ndio ulioleta mpangilio wa kitabaka - na hiki ndicho kiini cha mtafaruku katika jamii.

Kwa kuchunguza hali ya maisha ya baadhi ya wahusika katika Utengano, litakuwa baina ya makabaila na makabwela. Kuhusu maskani ya Bi Farashuu, msanii atueleza;

Bi Farashuu anaishi sehemu ya mwisho ya Madongoporomoka. Huu ni mtaa wa makabwela,

ambao unavutuka harufu ya uoza wa kila aina,  
wenye mashimo na makaro yanayoboboja maji  
machafu ovyo, wenyе vibanda vya mgongo  
vyenye kushika tama kwa unyonge ulivyovisibu  
- ndani na nje. (uk. 29)

Mwandishi ametumia neno "Madongoporomoka" kuonyesha  
hali ya nyumba na mazingira alimoishi Bi Farashuu.  
Nyumba ile ilikuwa imekandikizwa kwa udongo ambao  
ungaliweza kuperomoka wakati wo wote, labda kutokana  
na upopo mkali au hata mvua iliyovuja. Isitoshe, msanii  
ametupa mandhari ya unyonge na ultima kwa ujumla. Kwa  
mfano, iliabidi "Makabwela" hawa wazue mbinu za  
kuwawezesha kuishi na kuwapa mahitaji muhimu sana ya  
kila siku. Bi Farashuu aliingilia kibiashara cha  
kusukuma mikate ili aiuze na kupata angalau vitu vichache  
alivyovihiatji kuweza kulisukuma gurudumu la maisha.

*is this  
heading to if  
we intellect  
ing like he goes  
heat!*

*Mwendo*  
*Kunayo*  
*km  
in Sabu*  
*beila wa  
mvi - basi,  
dala Nyati Hesi*  
*siku hino  
Angangu*  
*Aspera  
Kotore  
Bwana Yani*

Hali kama hii ya mtaa wa Madongoporomoka hupatikana  
mahali kwengineko, hasa ambapo wachache walio na uwezo  
wamelijenga tabaka lao na kuwasahau "wasiojiweza"  
kiuchumi. Kunayo mifano maridhawa ya nchi (katika bara  
la Afrika) ambamo hali hii hupatikana. Kwa mfano, nchini Kenya kuna watu ambao huishi katika ukata wa kusikitisha  
hali wengine wanaishi kama miungu wadogo. Sehemu za  
Mathare na Majengo <sup>mji Nairob</sup> <sup>Tubera</sup> nchini Kenya zaweza kunasibishwa na  
Madongoporomoka katika jamii ya Utengano, hali ile ya  
sehemu za Muthaiga, Kileleshwa, Lavington, n.k. yaweza

*Ma Pindu 2/1*  
*- Kenya meoz  
manu ha ku  
wosetu wa  
naki.*

kunasibishwa na "Kasri" ya Bw. Maksuudi. Aghalabu,  
 watu waishio katika magharibi mwa mji wa Nairobi ndio  
 wamemiliki uhondo. Ndio wamekula fungu (kiasi), kubwa  
 la keki ya taifa. Ndio walio na uwezo wa kuishi katika  
 starehe kama vile, magari ghali na yenye fahari kama  
 vile "Benz", "Volvo", "BMW", n.k; vidimbwi vya kuogelea,  
 majumba makubwa makubwa n.k. Nay o baadhi ya mitaa iliyoko mashariki mwa mji wa  
 Nairobi huwa haikaliki kwa vile hali iliyoko yatisha.  
 Uvundo umetapakaa kila mahali kwa sababu ya kutumiwa  
 kwa vitu kama vyoo na watu chungu nzima. Aghalabu  
 kule hutokea maovu ya kijamii, kama vile jinai, unajisi,  
 wizi n.k. Kwa vile watu wamesakamwa na taabu kiasi cha  
 kuwa hawawezi kujizua vitendo kama vite iwapo wataendelea  
 kuishi. → Je, niwaya yeyunyuzi kuhusu Nairobi, hayu muafanui ni half-base

Ingefaa ieleweke kuwa mpangilio na mgawanyiko wa  
 jamii haupo tu nchini Kenya, bali pia katika nchi  
 nyinginezo za Afrika na vite vite katika mataifa  
 "yaliyoendelea" kama vite Amerika na kwengineko.  
 Katika Utengano, twaona jinsi maisha ya watu wa  
 kiwango cha chini yalivyo ya kufadhaisha. Watu hao  
 huishi kwa hofu pasipo kufahamu yatakayowasibu dakika,  
 saa, au siku ijayo. Maisha yao huwa kama ya wakazi wa  
 "Mathare" ambao kila dakika huwa wanahofu kuwa 'moto'  
 utatokea na kuviteketeza vibanda vyao - pamoja na mali

HALUC (1952)

*wana kuna moto*  
zao. Na Askari wa City Council wakibomoa [vioski] vya ambani  
nlio njia moja tu ya kihalali ambayo kwao wanawega  
kuipatia tiziki → MUOROTO (Council?)

Hali ya maisha pia huwafanya wengine kama Kazija  
na Mama Jeni kujishughulisha na biashara ya kuiuza *(concern)*  
miili yao. Mama Jeni amesitawi sana katika biashara  
hiyo mpaka akafikia kiwango cha "kuwaajiri" wasichana  
*(wanawake wachanga na warembo)* kama vile Maimuna *na furaha + dora*  
wawahudumie wanaume, kisha naye Mama Jeni apokee pesa.  
Ukweli wa jambo hili wathibitishwa na jinsi anavyopokea  
pesa kutoka kwa mkware mmoja aitwaye James ili (James)  
amwingilie kimwili Maimuna - mwajiriwa wake Mama Jeni.  
Lakini, Mama Jeni amekula *Huu!* mwande kwa miradi yake maadam  
Maimuna ni limbukeni kwa shughuli kama zile. Mama Jeni  
hafurahi moyoni, lakini vile vile hataki kuonyesha  
hasira yake maadam anajua kwamba "papo kwa papo, kamba  
hukata jiwe". Ana imani kwamba Maimuna atamfunza pole  
pole na atafunzika. Hatimaye anamrudishia James noti  
yake naye James anajiendea huku akilaani moyoni kwa  
kuyakosa mawindo yake.

Mazungumzo baina ya Maimuna na shogaye Dora  
yatonyesha jinsi walivyoteswa na maisha na kukinaishwa  
nayo. Maimuna aona kuwa tayari ameshatumbukia katika  
shimo la dunia, lakini ni muhali kutoka kule maadam  
hawezi kukubalika kwao kwa vile amejisaga na kujilimbika,  
katika malimwengu, na sasa ajihisi "debe bovu lisilo  
na pa kukalia". Dora naye, badala ya kumnsihi shogaye  
na kumshauri kwamba "Ng'ombe akivungu *j* mguu malishoni

hujikokota zizini kusaidiwa", amwambia yafuatayo;

Umenaswa kama wanavyonaswa wengi kama  
wewe bila ya hiyari, ama kwa udanganyifu  
au kwa sababu nyine nisioitambua. Na  
sasa Maimuna uko wapi? Leo wewe nani?  
Na huo ndio uhuru wako ----- too late,  
walioona Wazungu. (uk. 87)

Huko Bobea, alikohamia Maimuna baada ya kufukuzwa  
na Mama Jeni, kulikuwa kwa hali ya chini. Kwa mfano,  
twaelezewa kuwa kijumba cha Biti Sururu kilikuwa  
kidogo na kilijaa dhiki tupu. Kulikuweko na kibao  
kilichoandikwa "KIL MI KWIKI BAA". Kule nyumbani kwa  
Biti Sururu, maisha yameshabihiana na yale ya Bi  
Farashuu na ya Mama Jeni. Shughuli kubwa za kila siku  
ni ubugiaji wa mtindi na uasherati. Maisha ya namna  
hii si mageni hata kidogo kwa watu wa kiwango cha chini  
ambao hawana kazi nyine ya kuwapatia fedha. Wao  
huzihalalisha shughuli kama hizo za kunywa ama kuuza  
pombe isiyo halali na vile vile vitendo vyaa zinaa.

Hali ya maisha ya wanyonge pia yadhihirishwa na  
Shoka, barubaru mmoja anayefanya kazi ya sulubu huko  
bandarini. Baada ya kazi anaingilia tu ulevi bila  
kumjali mkewe Selume na watoto wake. Malalamiko ya  
mkewe yatuonyesha kuwa wanawake wamedhulumiwa na wanaume  
na (wanawake) wana shauku ya kujikomboa kutokana na

dhuluma na utumwa huu.

Bi Selume katika malalamiko yake amwambia mumewe;

Wallahi nitakata pingu za uke mimi 'vyo.

Nitatoka nje. Nitatarazaki. (uk. 111)

Dhuluma kama hizi ndizo alizozibainisha Kazija.  
Wanaume wengi huwa wanaushiriki ulevi wala hawashiki  
wadhifa wa nyumbani. Wanawaachia wake zao kazi zote  
za nyumbani - kuwalea watoto, kupika, kuwapeleka watoto  
shuleni, kuwalisha n.k. Jambo hili laonyesha kuwa  
wanawake wameonewa vikubwa na hawana budi wazue mbinu  
za kujikomboa. Wanawake tunawaweka pia katika kundi  
la wanyonge, maadam, kama makabwela wengine, hawana  
sauti mbele ya wanaume.

Selume, kwa ghadhabu na hasira za mkizi anamfokea  
mumewe Shoka kwa ulaghai wake wa kutegemea kulishwa  
kwa jasho la mkewe. Bi Selume amlaumu;

Nyooo! Hujui unachokila, hujui ulalapo  
wala uamkiapo, wewe mbioni, ti, ti, ti  
-----.

Ewe basi inajuzu hivyo? Huna hata imani.

Nyooo, mjalaana we! Si mjalaana wewe kwa  
hakika, vitendo vyako! Nenda huko vilabuni,  
nami niache na ulimwengu wangu. Niache  
niibebe mizigo nisiyostahili kuibeba. (uk. 112)

Ama kweli, maneno hayo yamesemwa na mwanamke mwenye ghadhabu aliyeswaswa katika "taasubi ya kiume" ambapo wanaume waamini kuwa kazi ya mke ni jikoni, na yeeye (bwana) ni bwana mkubwa mtawala na ana uhuru wa kufanya alipendalo.

Baada ya maneno ya Selume yanayomkashifu mumewe, mwandishi aeleza kuwa;

Ghadhabu ndizo zilizompa aseme maneno hayo; na utumwa, unyonge, na manyanyaso ya mwanamme. Mwisho wa maneno yake daima ulikuwa; "Tumo taabuni wanawake. Huu utumwa kamili".

(uk. 112)

Si jambo la busara iwapo tutamlaumu na kumnakidi Shoka moja kwa moja. Lazima kwanza tuchungue iwapo ayatenda hayo yote kwa maksudi au iwapo kuna sababu zinazompa kuyatenda. Tukitilia maanani kuwa Shoka alifanya kazi ya uchukuzi yenye sulubu, yawezekana kuwa mateso anayoyapata kazini ndiyo anayalowesha kwa pombe. Huenda pia anayakwepa matatizo ya kifedha nyumbani na akatafuta maficho, kimbilio na usalama katika mtindi. Lakini kwa upande mwingine pia lazima akumbuke kuwa wajibu ule wa u-baba nyumbani ni wake wala hastahili kuukwepa. Na iwapo alikabiliwa na matatizo ya kifedha, mbona basi azifuje zile akali alizokuwa nazo kwa kuchapa mtindi vilabuni na chumbani mwa Biti Sururu, na vile.

vile kushiriki katika usherati na Maimuna! *W. 8. 11. 21*

Ingawaje Shoka anaonekana ni mwanamme asiye asili wala fasili mwandishi anamtumia kama chombo cha kutoa hisi za wanyonge;

Wewe unafikiri pesa tuzipatazo sis<sup>i</sup> wachukuzi, au wakulima au wafanyakazi za sulubu ni pesa za mchezo? Mkulima, anachuwana na jembe, nguvu zake huishia wapi? Umerekani, Uingereza, au Japani au ----- wapi? Wao ndio wanaopanga bei za mazao yetu! Na wafanyakazi wa karahana, ukitazama sana wanamfanyia nani kazi - mkoloni mambo leo; na sisi wapagazi bandarini tunampakilia nani bidhaa una ----- unafikiri? Mabeberu. Bado, bado hatuna uhuru kamili hatujaudhibiti uchumi. (uk. 113)

Fikra kama hizi alizozieleza Shoka (kwa kitrevi) zimeelezwa katika shairi la "Ukoloni na Ukoloni Mambo-Leo" katika kitabu ~~hicho~~ hicho, shairi la "Sisimizi sisi" linaelezea kuhusu wanyonge.<sup>30</sup> Katika "Ukoloni na Ukoloni Mambo-Leo" mshairi ameihiusha mifumo hiyo miwili na kuiingiza katika mazungumzo. *dunderi* Ukoloni wajiondoa polepole (kwa amani) na kuuachia Ukoloni Mambo-Leo nafasi ya kutawala. Nao ukoloni mambo-leo wajibu,

Nipe njia, Nikuonyeshe kilinge  
Naingia, nilieneze varange  
Watalia, niwaumapo mi nge  
Nipe njia (S.T. uk. 20).

Katika shairi la "Sisimizi sisi", wanyonge  
wajimithilisha na wadudu dhalili ambao hawana uwezo  
wo wote dhidi ya mwanadamu awakanyangapo (wadudu);

Wanatukanya~~ga~~ binadamu bila ya kuhi~~s~~  
Hutuponda na kutuhujumu, bila ya kisisi  
Maisha yetu ni madhulumu, kipotea basi  
Sababu sisi ni sisimizi (S.K. uk. 19).

Ubeti huu wa shairi la "Sisimizi sisi" wawasilisha  
malalamiko ya wanyonge. Wanahisi kwamba wanadhuluiwa  
kwa vile tu ni wanyonge. Wao ni maskini kama vile  
wakazi wa Madongoporomoka, Bobea n.k. katika Utengano.

Hali nyingine ya maisha ya hali ya chini tunaipata  
katika sehemu ambako Maksuudi, Rashidi na Mussa  
walikopitia walipokuwa wanaenda Bobea kumtafuta Maimuna.  
Huko kulii~~twa~~ "kwa wala tope";

Ni vibanda vibovu vilivyomiliki mazingira  
haya, ambayo yametengwa na mazingira ya  
mjini walikoishi wanadamu kweli. Daima  
huku kulikuwa vumbi, vuke la umaskini na  
uchafu unaothiri maisha ya wanadamu.

----- Vidimbwi vya maji machafu vilikaribisha  
mbu kuzaliana ovyo. Tope, vundo la vyakula

vilivyoza na uchafu mwengine pamoja na  
kupuu la ufukara lilipanda puanī mwa  
jamāa waliokuwa wakiongozana kwa Biti  
Sururu. (uk. 132)

Kwa kweli hiyo ndiyo hali ya wanyonge katika jamii  
anayotuchorea S. A. Mohamed. Matumaini yao yaliambulia  
patupu. Wanaishi katika ulitima, uchungu na sulubu  
isiyo haba, kinyume cha walivyotarajia kama Biti  
Sururu asemavyo;

Mimi nilidhani tutagaiwa majumba -----  
nilifikiri tutakapopata uhuru wetu, sote  
tutakaa kwenye majumba makubwa, yale  
waliokuwa wakikaa wakoloni. Nilidhani  
tutakula pilau kila siku. (uk. 138)

*unaota b' nunda a' n yanayumia  
hao mbwa wa!, nonense*

2:5 KIMALIZIO

Katika sura hii (ya pili) tumeitafiti na kuinakidi  
riwaya ya Utengano, hasa tukielemea katika kipengele  
cha jamii - yaani, jinsi wahusika kadha wanavyojitokeza  
riwayani. Tasnifu kuu katika sura hii ilikuwa ni  
kubainisha wazi jinsi wahusika hao ambao ni viwakilisho  
vya mwandishi wanavyoyatetea maslahi yao.

Tumbainisha makundi mawili makuu, makabaila na  
makabwela na kuonyesha mienendo yao na jinsi  
yanavyohitilafiana.

*matalah*

Katika sehemu hii yafaa kutajwa kuwa si jambo rahisi kuuweka mpaka baina ya ~~tabaka~~ <sup>Watalah</sup> hiso mbili - bwanyenye na ~~proletarii~~ <sup>Watalah</sup>. Matabaka haya hubainika wazi wazi katika jamii kama vile za Kimarikani. Lakini katika jamii ya Utengano, ambayo yalandana sana na jamii katika mataifa ya Kiafrika, kigezo kinachotumiwa kuainisha makundi haya ni uchumi. Ingawa hali ya kiuchumi, kisiasa na kijamii huingiliana vikubwa, tumejaribu kuitafiti Utengano kwa muktadha wa jamii. Twatumainia kulitafiti suala la kiuchumi katika riwaya nyingine ya S. Ahmed Mohamed, ambayo ni Dunia Mti. Mkavu.

Katika Utengano, imedhihirishwa kuwa tatizo kubwa linaloikabili jamii ni uonevu na unyanyasaji wa matajiri dhidi ya maskini. Maskini (wanyonge) nao wanajizatiti ili kuuondolea mbali uonevu huu. Njia ya kipekee ya kuuondoa unyanyasaji na uonevu ni mapambano. Mnyonge hawezи kustarehe na angoje kupewa utu na heshima na anayemdhulumu. Matajiri hawawezи kuwapa wanyonge haki na usawa, maadam usalama na ustawi wao (matajiri) wategemea jinsi watakavyoweza kumkandamiza mnyonge. Kwa rfano, katika kazi za viwandani, bepari atapata tijara iwapo atawafanyiza kazi za sulubu wafanyakazi wao, pamoja na kuwapa mishahara ya chini. Nao wanyonge hawako tayari kuyakubali maonevu na idhilali. Wanadhihirisha hisia za mwamko kuwa wako tayari kuyaendeleza mapambano bila ya kukata tamaa.

Wanyonge wameamua kujikakamua na kujihami ili

kujikomboa. Lakini wanaamini kuwa, ingawaje ukombozi au 'uhuru' hautapatikana mara moja, hatimaye watashinda vita hivyo vikali.

Katika Utengano, mwandishi anatupa ishara ya kufaulu kwa wanyonge kutokana na ule mporomoko wa Maksuudi. Kazija amefaulu katika muradi wake wa kuitenganisha jamii ya Maksuudi. Na hizi ni kama ishara za mwanzo za ushindi wa wanyonge dhidi ya mabepari.

#### 2:6 TANBIHI

1. Nkweria, V. W., Sarufi na Fasihi Sekondari na Vyuo  
Tanzania Publishing House, Dar-es-Salaam 1978. (uk. 85)
2. Said A. Mohamed, "Kupatana na riwaya zangu",  
makala yaliyotolewa katika Mhadhara  
wa Kiswahili wa Kimataifa, Nairobi  
1981. (uk. 3) \*
3. Dkt. Kitsao ni mhadhiri wa somo la "Uchambuzi-mseto" katika idara ya isimu na lugha za Kiafrika,  
Chuo Kikuu cha Nairobi.
4. Maneno haya yamenakiriwa kutoka katika jalada la  
riwaya ya S. A. Mohamed - iitwayo Utengano.
- \*5. Mazrui, A. na Kazungu, E.K., "Maendeleo ya Fasihi ya Kiswahili"  
makala yaliyotolewa katika kongamano  
la kimataifa la chama cha Kiswahili  
cha Kenya, Nairobi, 1981. (uk. 1)

6. Hussein, N. E., Mashetani, Oxford University Press, Nairobi, 1971.
7. Sayyid, A.A. Nasir, Al Inkishafi, Oxford University, Press, Nairobi, 1972 (uk. 56).
8. Muhando, P., Tambueni Haki Zetu, Tanzania Publishing House, Dar-es-Salaam, 1975.
9. Mutiso G. C., Social - Political Thought in African Literature, Macmillan, London, 1974.
10. Kama namba 2 juu. (uk. 7)
11. Kamusi ya Kiswahili Sanifu, Oxford University Press, Dar-es-Salaam, 1981. (uk. 150)
12. Mifano ya viongozi kama vile J. B. Bokassa wa Jamhuri ya Afrika ya Kati na Dikteta Idi Amin wa Uganda.
13. Kezilahabi E., Dunia Uwanja wa Fujo, East African Literature Bureau, Nairobi, 1975.
14. Abdulaziz, M. H., Muyaka, 19th Century Swahili Popular Poetry, Kenya Literature Bureau, Nairobi, 1979. (uk. 63)
15. Mohamed, S. A., Sikate Tamaa, Longman, Nairobi, 1980. (uk. 1)
16. Hussein, E., Wakati Ukuta, E.A.P.H., Nairobi, 1971. (uk. 17)

17. Kama namba 15, juu (uk. 7)
18. Ngugi wa Thiongo, "Literature and Society", katika Eddah Gachukia - Teaching of African Literature in Schools. Kenya Literature Bureau, Nairobi 1978. (uk. 3)
19. Marx K., na Engels F., The Communist Manifesto, Penguin Books, 1978. (uk. 79)
20. Kama namba 6 juu. (uk. 2)
21. Kama namba 20 juu.
22. Armah A., Uchambuzi wa Wema Hawajazaliwa, (uk. 59) katika African Literature Today, Heinemann Nairobi 1975. (uk. 97)
23. S. A. Mohamed, Utengano, Longman, Nairobi, 1980 (uk. 72)
24. Freire, P., Pedagogy of the Oppressed, The Seabury Press, New York, 1968. (uk. 30)
25. Kama namba 7 juu (uk. 70)
26. Kama namba 24 juu (uk. 29).
27. Kama namba 11 juu (uk. 94).
28. Kama namba 15 (uk. 9)

29. Gachukia, E., (Ed.); Teaching of African Literature in Schools, Kenya Literature Bureau, Nairobi, 1978.
30. S. A. Mohamed, Sikate Tamaa, Longman, Nairobi, 1980 (uk. 19).

1 122  
108  
14

## S U R A Y A T A T U

### 3:0 DUNIA MTI MKAVU

### 3:1 UTANGULIZI

*mfupi kuanza kuanza kuanza*  
*Kichwa chake kumkata*  
*U*

Dunia Mti Mkavu ni riwaya aliyoiandika S. A.

Mohamed mwaka mmoja na ile ya Utengano (1980).

Kichwa chake kimetolewa katika shairi moja la Muyaka Bin Haji (1779), mshairi maarufu sana wa ushairi wa "tarbia", aliyeishi na kuyatongoa mashairi katika sehemu ya mwanzo wa karne ya kumi na tisa - baina ya mwaka wa 1776 - 1840.

Shairi hilo laitwa "Dunia Mti Mkavu" na ubeti wake wa kwanza huenda hivi;

Dunia mti mkavu, kiumbe siuemel<sup>e</sup>

Ukaufanya nguvu, kuudhibiti kwa ndole

Mtiwe ni mtakavu, mara ulikwangushile

Usione kwenda mbele, kurudi nyuma si kazi.<sup>1</sup>

Shairi hili ni aina ya waadhi katika jamii, kuwatahadharisha na kuwaonya wale wanaoikiuka mipaka hii na ile kuwa maisha ya dunia hii kamwe hayadumu. Latoa wosia hasa kwa wale walioneemekewa na maisha ya hapa duniani kwa kuupata utajiri, cheo, madaraka, mamlaka na taadhima kuwa vitu hivyo si vya daima dawamu. Mtu anaweza kujitapa leo kwa sababu ya cheo chake, na kesho ashtukie kwamba kile cheo ashakipoteza kutokana

na vitendo vyake viovu. Hujikuta kwamba ashateremshwa chini kule juu alikokuwa amepanda ngazini. Ndiposa mshairi ashauri kuwa; "Usione kwenda mbele, kurudi nyuma si kazi".

Katika riwaya yake, S. A. Mohamed, kwa usarifu na usanifu wake na pia uteuzi wa maneno, amesadifu kutusimulia visa na vituko mbali mbali ili kurutubisha nasaha yake katika jamii.

Maadam wataalam katika somo la mtindo wamesema kwamba "mtindo ni mtu"<sup>2</sup> yatumainiwa kwamba kutakuweko na muumano na kunasibiana katika fani kadha za Dunia Mti Mkavu na riwaya ya Utengano kwa vile zote ni za mwandishi mmoja. Hata hivyo litakuwa jukumu la kazi hii kujitahidi kuchuja yaliyo na uzito zaidi katika kila riwaya na kuyachambua na pia kuyanakidi.

Katika Utengano, tumetilia mkazo mpangilio wa jamii katika fani ya kijamii. Katika Dunia Mti Mkavu, tutaelemea sana katika hali ya kiuchumi na jinsi hali hiyo inavyoendelezwa katika riwaya ili kuyasawirisha maudhui ya tasnifu nzima ambayo ni "wanyonge katika jamii".

S. A. Mohamed katika Dunia Mti Mkavu, kama vile A. Abdalla, Sauti ya Dhiki, Ngugi wa Thiong'o Shetani Msalabani - ameiendeleza mbele zaidi kazi ya

fasihi kwa kuipa lengo la ukombozi. Amefahamu kuwa haiwezekani tena kufuata lile lengo la zamani la kuwafunza watu sera na mienendo ya maisha tu ambapo kila tukiangaza macho twaona idhilali na unyanyasaji ukiendelezwa. Mwandishi huyu pia amefahamu kuwa katika jamii ambamo wanyonyaji wanaendelea kutumiminia fikra zinazotutia katika utumwa wa kuamini mambo yale yale yanayoendeleza dhuluma, haitoshi tena kututanabahisha tu kuwa katika jumuiya yetu kuna unyanyasaji au hakuna demokrasia. Ameitumia fasihi kama chombo cha kumkomboa binadamu na utumwa wa imani na mawazo yanayoendeleza unyanyasaji wake na kulinufaisha tabaka la wanyonyaji wake tu.

Itaonekana kuwa wahusika katika Dunia Mti Mkavu wameupata mwamko zaidi juu ya unyanyasaji kuliko wale wa Utengano.

### 3:2 MAUDHUI

Maudhui kuu inayojitokeza katika riwaya hii ni jinsi jamii fulani ya waswahili inavyojizatiti na kujihami ili kuupinga utawala wa dhuluma wa wakoloni. Utawala huo wa kikoloni unajiimarisha katika dhuluma na ukandamizaji katika mfumo wa ubepari. Ubepari unaendelezwa sio tu katika utawala bali pia katika uchumi, hali ambayo inasababisha kuweko kwa kundi la upinzani linaloupinga uonevu na dhuluma za mabepari.

Baadhi ya wapinzani hawa ni watu ambao hawana kazi na wengine ambao wanafanyizwa kazi za sulubu kwa malipo yaliyo haba. Nao watu hawa wanaonyanyashwa waona kuwa ~~ni~~ <sup>neguna</sup> muhali kunyamaza tu na kuukubali uonevu. <sup>↑ Sisi ana potoka Katika Luko rect "si muhali" na ana walikus, dhuuma nimewa ni muhali</sup> Aghalabu, wanajitokeza wazi wazi na ~~ku~~ upinga ukoloni na utumwa. Takriban kila "mnyonge" anaonyesha kuwa anafahamu uonevu upo katika jamii. Baadhi yao kama vile itakavyodhihirika katika riwaya wameyakolea mateso, na kutokana na tajriba yao ya maisha wanaelewa jinsi ya kukabiliana nayo.

Baadhi ya maudhui nyingine zitabainika tutakapo-endelea na utafiti. — *you are just  
on escapist  
play boy!  
scoundrel*

### 3:3 UFUPISHO

Sura za mwanzo nne hututanguliza kwa wavulana wanne - Fumu, Bakari, Pandu na Kibwana (Farouk) wa jamii ya Mzee Jaku. Katika sehemu hii inadhihirini migogoro kati ya watu wa jamii moja - baina ya Kibwana (Farouk) na wengineo. Migogoro hii zaidi yadhihirisha kuwa uhusiano wa jamii hiyo ni wa kitabaka.

Sura ya kwanza yamtanguliza ndugu wa kwanza Fumu Jaku anayewakilisha tabaka la "wakulima" katika mazingira ya kibwanyenye. Vile vile unadhihiriri ukinzani baina ya Fauz (mtoto wa bwanyenye) na Fumu. Ukinzani huu unadhihirisha jinsi wanyonge walivyodhalilishwa na mabwanyenye, na wanavyoweza kuingizwa hatarini na

*Ubageni - Capital  
Wanyonge - Feudalist*

mabwanyenye. Dhuluma hizi zinaendelezwa zaidi wakati

Masika (mpenzi wa Fumu) anapouzwa kwa Fauz. *Malikene ndiyo  
babave Moshka-siyu  
Fauza anamuzaje  
mzelereza ne  
wylha ucinu*

Mzee Gae naye ametumiwa riwayani ili kuwakilisha  
dhuluma na vile vile mwamko wa siasa wa wanyonge.

Yeye ni mwakilishi halisi wa wafanyakazi. *wafanyakazi  
na-yeje ang walete Pandu jin watobane ndio*

Sura ya kwanza yaishia kwa wazo kuwa wafanyakazi  
wanapingana na dhuluma za ukandamizaji na unyanyasaji.

Sura ya pili yammulika ndugu mwingine aitwaye  
Bakari Jaku. Huyu yuko katika tabaka la proletarii  
na vile vile anaonyesha mwamko wa kitabaka. *ngalana*

*Kumba wa  
wala wala*  
Proletarii huonyeshwa kama tabaka linalosisitiza  
mabadiliko (mapinduzi). Kwa mfano, mhusika mmoja  
aitwaye Kumba anaonyesha kuwa amepevuka kuliko Mzee  
Gae, ambaye ni mkulima wa kawaida. Kwa hivyo, katika  
Kumba, twaliona tabaka la proletarii likipingana na  
ukandamizaji wa kibepari.

Katika sura ya tatu, twakumbana na ndugu mwingine  
- Pandu Jaku. Tabaka la Pandu ni tabaka ambalo laweza  
kushawishiwa kwa urahisi na watawala kwa manufaa yao.

Kundi kama hili ndilo aghalabu huwa la wasaliti, kama  
vile Karanja katika riwaya ya Ngugi, A Grain of Wheat.<sup>3</sup>

*Pandu Jaku*  
Sura ya nne hulidhihirisha tabaka la wanyonyaji -  
maadui wa wanyonge. Farouk Hilal ndiye anayewakilisha  
tabaka hili. Kule kulibadili jina lake kutoka Kibwana

Jaku hadi Farouk Hilal huonyesha kupanda kwake kitabaka. Farouk hushirikiana na ukoloni na ubeberu kuwakandamiza watu wa tabaka la chini. Hivyo, neema za tabaka hili za kiuchumi hutokana na ukandamizwaji wa watu wa tabaka la chini.

Kuanzia sura ya tano na kuendelea twaonyeshwa mgongano baina ya matabaka. Wanaonyanyashwa wanaungana chini ya usimamizi wa viongozi wao na wanakutana katika kibanda cha Fumu na kuamua washirikiane na kuyatoa malalamiko yao kwa tabaka la kibepari - kwa njia itakayoleta mapinduzi.

Madhumuni ya muungano ~~huu~~ ni kuitisha mgomo wa wafanya kazi ukiwa na nia ya kuubomoa uchumi wa kikoloni/kibepari. Pia, wana lengo la kuudhoofisha muundo wa kisiasa wa kibepari.

Imani ya S. A. Mohamed ni kuwa hii ndiyo njia ya pekee ya kuwaokoa wafanya kazi.

#### 3:4 WAHUSIKA

Ili kubainisha uhusiano ulioko baina ya tabaka la "wanyonge" na tabaka la "mabepari", itatubidi tuwachambue na kuwanakidi baadhi ya wahusika katika riwaya. Mienendo yao na hali yao ya maisha kwa jumla itatupa ~~ihibati~~ kuhusu tabaka analoliwakilisha kila mmoja wao.

Kwa madhumuni ya kazi hii, tutaigawa jamii iliyochorwa katika Dunia Mti Mkavu katika makundi mawili, wanaoonewa na wanaoneea - panga bwane mabepari na wafanya-kazi. Kwa mfano, Fauz na Farouk Hilal watakuwa katika kambi moja - ya mabepari hali wahusika wengine kama vile akina Mzee Gae, Fumu Jaku, Bakari Jaku, Pandu <sup>coorie</sup> <sup>?</sup> <sup>?</sup> Jaku, n.k. <sup>Andika verufi doyo. pl. w' nas. w'</sup> Watakuwa katika kambi ya wakulima. Lengo kuu hasa litakuwa ni kuzichunguza hisia na malalamiko ya "wanyonge".

3:4:1 FUMU JAKU, MZEE GAE

Wahusika hawa wawili wamechorwa kama wawakilishi wa kundi la watu walioonewa katika jamii. Fumu amekolea na kustahimili machungu na idhilali kiasi cha kuwa ametumbukia katika hali ya uchofu inayojisawiri yenye;

Mosi, mwili wake ulikuwa na malimbiko ya uchofu na mavune, ingawa hilo si la kuhesabiwa, maana mwili wake umehimili sulubu na mateso toka mja yeye kutumbukia katika shimo hili la dunia. Ni shimo hii dunia: na kama dhiki huzoeleka, basi mwili wa Fumu ungalizoea. (uk. 1)

Ingawaje hapa mwandishi hatupi sababu za Fumu kuwa katika hali ya namna ile lakini maneno yake yatupa taswira ya dunia ambayo haina haki. Vile vile

maneno hayo yatupa wazo kuwa duniani ni mahali pa  
mateso na hapana starehe. Lakini msomaji aeleva  
kuwa mwandishi anaitumia mbinu ya jazanda kumaanisha  
kuwa jamii ndiyo imeenda kombo wala si dunia kama  
tuijuavyo. Vile vile twalipata wazo lililoelezwa  
katika riwaya kuwa dunia ni "mti mkavu".

Hujaheze  
chochote.  
Unahapa ku!

Maisha ya Fumu yanashabihiana na yale ya Mzee Gae  
kwa kiasi kikubwa maadam wote wawili wanaishi katika  
ulitima na ghadhabu, hasa kutokana na tajriba ya  
maisha na yaliyowakumba zamani. Mzee Gae ndiye  
aliyeteswa zaidi, na kutokana na "kuishi kwingi na  
kuona mengi", ameamua kunyamaza tu na kuyaangalia  
mambo kama baridhuli. <sup>a</sup> Maneno ya Mzee Gae kila siku  
yalikuwa;

Waliniunja kichwa changu kwa nyundo -----  
Nyundo ----- yah, nyundo; yah,  
waliniuruga, walikivuruga kichwa changu.  
----- Waliniita mbwa (dog), yah, mimi  
mbwa. Na mara nyingine waliniita Mswahili  
mwenda wazimu. Walinitesa kama mnyama.  
Kwa sababu ----- Kwa sababu nilithubutu  
kuwaambia ukweli. ----- Lazima muulize,  
kwa nini, kwa vipi, kwa sababu gani. (uk. 2-3)

Mzee Gae, kama <sup>mig, j sema bwene</sup> ilivyosemwa hapo juu ameamua  
kunyamaza kwa vile anayufahamu na ashayaona mengi hasa

yaliyo machungu. Msanii amtumia Mzee Gae kama chombo cha kuwatia wanyonge hamasa na kani ya ukombozi.

Anawahimiza wasiwe waoga hasa wateteapo haki na ukweli.

Maneno ya kuzindua ya Mzee Gae yanayapiga mwangwi maneno ya A. Abdalla katika Sauti ya Dhiki ambapo anawahimiza watu waseme haki na ukweli hadharani ingawa ukweli waumiza.<sup>4</sup> Mzee Gae anawakejeli waoga kwa kuwaita "majimbi wala si majogoo". Majogoo ni wale watu wanaousema ukweli wazi bila kuchelea kuwa wanajipalia makaa. Na huu ndio ukombozi kamili.

Huwezi kusinachukua  
Kisima kuna hali kifaa  
ni kujidhera kuna ni kosa  
kuwa sana mto kama mwele  
unzelikanya. F

Liongo! hakisifungwa Alijugwa lila?

Fumu Jaku alipotoka jela aliishi kibandani mwake kwa unyonge na umaskini. Alianza kulima katika kijishamba chake kidogo ili ajipatie angalau chakula cha kila siku. Lakini Fauz alikuwa kikwazo cha maendeleo yake. Kudhulumiwa kwa Fumu na Fauz kunamfanya Fumu akitoe "kilio" chake cha simanzi kwa Mungu;

Mungu tupe nasi, angalau nguvu za jasho letu kama ulivyowapa ----- (uk. 5)

Maneno haya yaonyesha kuwa Fumu ananyanyaswa kwa mazao anayoyapata shambani mwake. Aomba dua kwa Mungu ili wanyonge waweze kupata nguvu za kujikomboa na wanawitawala nguvu na maezo ta hanejetawala, kuweza kuzitawala nguvu zao na vile vile mazao yao.

Fumu hana uwezo wa kulitawala shamba lake kwa vile limefilisiwa na Fauz na ni lazima Fumu ampelekee "zawadi" kutokana na anachovuna.

✓ Prof. Abdullaiz  
me mleki alipotoka  
intahim huyu.  
anayofu?

↗ Nitemba wapi wago hili?  
Chambua Kitabu kena kiliyo. Unajipanya maradhi  
kina kuongezza mendo yako Ki-vi-pi!

Udhalimu wa Fauzi unaonekana katika maovu  
anayomtendea Fumu. Kwanza, anamtesa Fumu kinyama  
kwa kumwachilia mbwa wake Roket amshambulie Fumu.  
Pili anamnyang'anya kwa nguvu mpenzi wake Masika na  
tatu anataka kumpokonya shamba lake kwa hila. Baada  
ya Fauz kumtisha Fumu kuwa atamnyang'anya shamba lake.  
Fumu amfokea Fauz;

Mi la mabwana,  
yeze akodishwa tu.

Sikiliza ----- Niambie ulilolijia  
nilijue. Sio kunijia kifua moto -----  
anayenilisha mimi ndiye anayekulisha  
wewe; Mungu mmoja, aliyekupa wewe kiti  
akanipa nami kumbi, sasa? Na kama ni  
ardhi yako, mimi natoa nguvu zangu bwana.  
Anilishe nani Fauz, kama si nguvu zangu.  
(uk. 8)

Kule kuitetea haki yake ni dhihirisho kuwa Fumu  
kamwe hakubali maonevu ya Fauz. Uonevu huu wa  
kafilisiwa na kunyang'anya mashamba na watu wenye  
uwezo umeenea pia katika riwaya ya Nyota ya Rehema,  
~~KARIM Faud~~ ambapo ~~had~~ anafanya njama za kumnyang'anya Rehema  
shamba la wazee wake na baadaye kumuuzia shamba lile ~~X~~?  
lile.? Aghalabu, mabwanyenye hawa wanawadhulumu  
wanyonge kwa kudai kuwa maisha yao (wanyonge) yamo  
mikononi mwa mabwanyenye kwa vile ndio "wanaowapa"  
mashamba ya kulima na kuwalinda kwa ujumla. Jambo

if this is the first &  
greatest our progressors  
open, then I am afraid  
I won't come for my  
ma here, I will  
fly to Massachusetts  
us.

Ulipita  
K.C.E?

Ulipita  
K.C.E?  
D.U.Yings  
Indonesia  
or Europe

hili ni la kinaya kikubwa. Maisha ya mabepari ndiyo yamo mikononi mwa wakulima, maadam hawa wa pili ndio wanaowalisha, kuwalisha n.k. Hata zile starehe wanazopata kama vile magari, majumba na kadhalika zatokana na jasho la watu kama Fumu.

Wajibu wa Mzee Gae katika riwaya hii ni kuwapa wanyonge ujasiri. Kutokana na maarifa na falsafa yake amejifunza kuwa njia ya pekee ya kujikomboa kutokana na unyanyasaji ni kujasiri na kukabiliana na "maadui" kishujaa, pasipo kuufyata mkia. Anawahimiza wanyonge waupinge uonevu kwa hali na mali ili mnyonge aweze kuupata utu na vikomeshwe vitendo kama vile vya Fumu kunyang'anywa mpenziwe Masika na Fauz. Huu unyang'anyi waonyesha kuwa jamii ya Dunia Mti Mkavu ni jamii ya "mwenye nguvu mpishe". Hata hivyo, wanyonge hawakubali tu kumpisha mwenye nguvu pasipo upinzani wa aina fulani. Stashahada iliyotumiwa ya Kipele (ng'ombe wa Fumu aliyemfunga) Fumu na Masika (uk. 22-23) yaonyesha kuwa Fumu alijitahidi avezavyo kupigania Masika asiende, lakini wapi ----- "Mpiga ngumi ukuyta huumiza mkonowe". Kama tuelezwavyo na mwandishi, nguvu, utajiri na uwezo umekata uhusiano baina ya Masika na Fumu.

Fumu na wanyonge wenzake wametambua kuwa mtu mmoja hawezi kuuleta ukombozi. Ukombozi utaletwa na bidii

za watu wengi pamoja. Wazo hili limewasilishwa katika stashahada ya ung'oaji wa mti - Fumu anaposema;

Mkono mmoja hauwezi kuutikisa mti huu;  
mtu mmoja asingaliweza kung'oa shina<sup>la</sup>  
mti huu. (uk. 25)

*Ran*  
*Par*

Maneno haya ni kama mwitikio wa maneno ya Mzee Gae kuwa lazima watu wawe na ukakamavu katika kulitenda jambo. Aidha, yanamaanisha kuwa wanyonge wakiungana pamoja wanaweza kuung'oa uonevu na dhuluma za wenye nguvu.

Wahusika hawa wawili, Mzee Gae na Fumu Jaku wana changizo muhimu katika maudhui ya mwendelezo wa ukombozi wa wanyonge kutoka mikononi ya dhuluma za mabepari.

### 3:4:2 BAKARI JAKU

Katika sehemu ambayo tumeelezewa kuhusu sifa za Bakari Jaku, mwandishi pia ameubainisha utumwa na uonevu unaoendelezwa katika jamii. Mambo yanayodhihiri ni kama vile; udhalilishaji wa uke, kama inavyoonyeshwa katika uhusiano baina ya Mashaka na mkewe Bi-Mtumwa, uonevu, hasa dhidi ya watu wenye hali ya chini ya maisha - hili laonyeshwa na jinsi aghalabu serikali inawavamia watu wanaouza na kunywa pombe na vile vile Muvoko? kuvuta bangi n.k. Vile vile, twachorewa mandhari ya hali ya chini kama vile watu kuwachotea wengine maji

*Raoed Raoed  
Raoed Raoed  
Mwishi*  
kwa malipo, kwenda mjini kutafuta kazi, wafanya  
biashara kufungiwa vibanda, n.k. Kwa hivyo, ingawa  
sehemu hii inataja machache kuhusu Bakari Jaku, yeye  
ni wakilisho la watu wa hali ya chini kama vile,  
Shomari, Mosi, Mjaka, Bi-Zaina, Bi-Mtumwa n.k.

Watu wa tabaka la Bakari Jaku ni watu wanaoishi  
katika hali ya umaskini na ambao mara kwa mara  
wanagombanishwa na umaskini wao. Wengi wao kama vile  
Shoka katika Utengano wamegeukia ulevi wa kupindukia  
ili kujisahaulisha matatizo yao. Haya yaweza  
kudhihirishwa na ugomvi baina ya Mashaka na mkewe. *(Bi mtumwa)*  
*(bi) zin Heji*  
*(bi) pili*  
*(bi) mashaka*  
Ugomvi huu kama tuelezwavyo ni wa kawaida wala si wa  
siku moja tu.

Mwanamke huyu (Bi-Mtumwa) anapigania haki yake  
kutoka kwa mumewe ambaye ana tabia za kumwibia pesa  
zake na kwenda kulewa nje. Uonevu huu waweza  
kumithilishwa na uonevu wa wakulima au watu wa kawaida  
na wakoloni au wabeberu. Katika jamii aliyoichora  
S. A. Mohamed, mwanamke pia amepambwa na kupewa sifa  
za mnyonge - asiye na nguvu wala uwezo mbele ya  
mwanaume. Kule kupigana kwa Bi-Mtumwa na mumewe kwa  
kani kwatuonyesha kuwa wanyonge hawachelei nguvu za  
*Bwishi! Can't you understand that my husband (husband)  
is being beaten by the wife?*  
*husband*  
*chechel*  
*Sema went*

Ukata ulikithiri katika sehemu walimoishi akina  
Bakari - ingawaje wao wenyewe hawakutaka kuwa katika

hali ile. Mwandishi atueleza kuwa;

Wakati huu alitokea Haji, kijana mvuta  
bangi aliyechongwa vibaya na mazingira  
yake na kupuuzwa na wale<sup>z</sup>i wake. -----

Bakari aliwaza juu yake;

Maskini si kosa lake. (uk. 33)

Bakari atumika kama chombo muhimu cha kuwapa  
wenzake mwamko wa kimapinduzi. Anawatia shime kuwa  
si faradhi yao kuishi katika umaskini, ila hali hiyo  
imesababishwa na mabepari wachache wenye kuzijali tu  
nafsi zao.

Mabepari hawa ndio wamewafanya watu wengine  
waishike kazi ya uzegazega. Kazi hii yasababisha  
kisirani baina ya Mzee Fuko na Biti Kondo, kwa vile,  
kila mmoja anataka kuyachota maji.

Bakari, Kumba, Shomari, amba ni makuli bandarini  
wana hisia kuwa wao ni wanyonge, wafanya kazi ya  
sulubu kama inavyodhahirika katika maneno ya Kumba;

Jifunze kutokata tamaa, ndipo ulimwengu  
utakapouweza. Kumbuka wanatujaza unyonge  
tuwanyenyeknee. Wanavunja nyoyo zetu ili  
tusiwe watu. Binadamu asiye na moyo si  
mtu. Ndio maana hatuna hisia ingawa

tunakandamizwa, tunateswa. Kwa nini  
tuwe katika amri yao maisha? Kwa nini  
tutiwe shimiri kama Ng'ombe? (uk. 38)

Hizi ni ishara kutoka kwa tabaka la wafanyakazi  
kuwa hawakubali mbinu zinazotumiwa na wabeberu  
kuwakandamiza (wafanyakazi). Katika kiwango cha mwamko  
huu ndipo watu wanapoungana pamoja dhidi ya wanyonyaji.

Bakari naye ayatilia nguvu maneno ya Kumba kwa  
kusema;

Katika ulimwengu huu mwanadamu kila kitu  
amekifanya chake. Hata hewa wangaliweza  
kuitenga na kuidhibiti wangalinyang'anyana,  
kila mmoja akadai ni yake. Na hiyo ndiyo — *Hewa  
nauha*  
nusura yetu sisi maskini, angalau tuko huru  
kuvuta hewa; ingawa sisi huvuta chafu, wao  
wakavuta safi. (uk. 39)

Kila alipoiwaza hali hii, Bakari aliikumbuka hali  
ya ultima na uyatima alimoachwa na wazazi wake (*Uyego*)  
*hali hali*  
A walipofariki dunia wakati (Bakari) alipokuwa mtoto  
wa miaka mitano. Kisha, aliachiwa dhiki na maonevu  
ya dunia. Alielekea mjini kutafuta kazi ndipo akapata  
kazi ya ukuli - bandarini. *Hata ingawa ukuuwa ulifaraya MA,*  
*yaonekana hukukusano katabu hiki*  
*kua makini!! Mwongo wa mwele.*

Wanapowaza juu ya hali ya ulimwengu, Bakari na  
Shomari wanauona ulimwengu huo uliojaa mtafaruku, kama  
asemavyo Bakari;

Nikiwaza juu ya huu mtafaruku tulionao.

Huu ulimwengu, ulimwengu wa chuki,

ufedhuli, ujeuri, kiburi, ushupavu,

matusi. (uk. 43)

----- Huu natuuite ulimwengu wa mnyonge -  
msonge, basi haustaa jabiwi. Tabia za watu  
zimebadilishwa. ----- Ndiyo zimebadilishwa,  
hazikubadilika. (uk. 44)

Ingawa wafanyikazi wote wanaonewa na adui mmoja  
(ubepari) wengine wanazozana mionganii mwao na kuziona  
kazi zao ni bora kuliko za wengine. Mathalani,  
wafanyikazi katika kiwanda cha mafuta wanajiona bora  
kuliko wafanyakazi katika bandari. Hawafahamu kuwa  
wao wamo katika chombo kimoja, wakiopoka, wameopoka  
wote, wakizama, wamezama wote.

Shauri hili la kuungana pamoja ili kumpinga  
adui mmoja limesisitizwa sana hata na Jemadari Kimathi  
katika tamthilia ya Mzalendo Kimathi.<sup>5</sup> Katika nyakati  
za kikoloni, Kimathi alisafiri huku na huko nchini  
Kenya akiwahubiria watu wa makabila, dini au viwango  
tofauti waungane pamoja maadam "umoja ni nguvu,  
utengano ni udhaifu".

Wafanyakazi wa Dunia Mti Mkavu pia hawana budi  
waungane pamoja, kama vile Marx anavyohimiza;

Wafanyakazi wa ulimwengu unganeni pamoja.

\* Hamna cha kupoteza isipokuwa ~~maisha~~ (miyo) <sup>mnyonyo</sup>  
~~wawu waona wanayangu ya kupoteza maisha~~ - ni chao <sup>6ns!</sup>  
yenu. Mna ~~ulimwengu~~ mnaotarajia kuurithi.

(Tafsiri yangu)

~~Bla ghaaka mbora Sana!~~

Baada ya kuusema ukweli, Mfaka Bakari amejichimbia kaburi lake mwenyewe. Amefukuzwa kazini kwa madai kuwa

Ninachochea watu kwamba malipo hayatoshi,

na hali zetu zinakuwa mbaya kila siku. (uk. 48)

Lakini kama alivyosema S. A. Mohamed, katika Utengano, kumnyamazisha mnyonge mmoja ni sawa na kuwapalilia wengine, Kimathi (Ngugi na Micere 1978), pia aliquawa na wazo kuwa akiaga dunia wazalendo wengine wengi watayaendeleza mapambano.<sup>7</sup>

Kutokana na malalamiko ya wafanyakazi, ambayo wadhalimu wanayatilia masikio komango, wafanyakazi hawa wanawaza juu ya mgomo, lakini mmoja wao anatanabahisha;

Lakini sisi makuli hatutoshi kufanya mgomo, lazima wachukuzi washirikiane nasi; pia wazururaji wasio kazi wafahamishwe maslahi ya wanyonge ili wasije wakatumia kujaza nafasi zetu; pia wakulima na wafugaji lazima tuwashirikishe. (uk. 53)

Bakari ndiye amejasiri kuuongoza mgomo huu. Ama kweli, kama nduguye Fumu Jaku, ye ye pia ameitikia maneno

ya Mzee Gae kuwa uoga haufai kwa mwanadamu. Hatua hii ya mgomo inatilia nguvu imani ya msanii wa riwaya hii kuwa penye udhalimu na uonevu, mtafaruku hauishi.

*See  
Kinewii*

3:4:3 PANDU JAKU

Pandu Jaku huishi katika hali ya jitimai. Yeye ni fukara *hoe hae* na ana sifa mbaya - za wizi.

Kumba rafikiye pia ana sifa zizo hiso za wizi,  
lakini anauhalalisha wizi kwa kusema;

Kwanza wewe unajijua unaiba, lakini kinyume cha matakwa yako. Ni hali ya mambo inayokufanya hivyo. Umetamba kutafuta ardhi ya kulima, huna. Umetamba kutafuta kazi hukupata. Unataka kuishi, utakula upepo? Na kuishi sio kula, kula majani kama ng'ombe. Unataka ule vizuri, ulale pazuri, upate pumziko. Na si wewe tu bali una watu nyuma yako. (uk. 58)

Ingawa watu hawa wawili wana sifa za wizi, mmoja wao (Kumba) ameajiriwa kama kuli huko bandarini, hali Pandu ni kabwela mzururaji.

Lakini, wahusika hawa wawili wamebanwa na hali ya maisha hivi kwamba hakuna ajionaye bora kuliko mwingine. Sifa zao za jinai zimezagaa sana katika jamii za kibepari. Hali huwa hivyo kwa mabwanyenye

hao ndio wamemiliki njia za uzalishaji, na vile vile  
wanawamiliki wafanyakazi ambao hawana mali yo yote.  
Kitu walicho nacho ni zile tu nguvu (jasho) zao ambazo <sup>utisena ulelewa ogrewe zao in huse</sup>  
<sup>utisena ulelewa ogrewe zao in huse</sup>  
wanaziwa kwa dhamana ndogo kabisa. Tabaka dogo la  
mabwanyenye ndilo linalosababisha mzozo wa kiuchumi  
kwa vile huwanyanya wakulima na kuwaacha bila cho  
chote. Hali hii nayo huwapa wanyonge wazo la kuungana  
pamoja ili waung'oe utawala dhalimu. Jambo hili ndilo  
lililomfanya Kumba afike kuonana na Pandu kwa vile  
anataka makabwela na wazururaji wawaunge mkono makuli  
ili kuuimarisha mgomo, na hatimaye vita vyta ukombozi.

Bi-Pili, kama vile Bi-Mtumwa amueleza Pandu jinsi  
mumewe (aliye marehemu sasa) alivyomtesa;

----- Sijapata kuona furaa ha katika  
ndo ya aangu ----- alinipiga, alinitesa,  
hakunishughulikia; akanitwiisha mziiigo  
wa maisha ----- alikuwa mleeeevi kuliko  
ee miii. (uk. 61)

Malalamiko ya bi huyu, kama mabibi wengine  
tuliowaona yanapinga "taasubi ya kiume". Wanawake pia <sup>bijondyo lew s- wa</sup>  
wana hamu ya kujikombua kutoka katika "utawala dhalimu"  
<sup>vicohoni asilia</sup>  
<sup>hago nelipo mebha weym'</sup>  
<sup>Laiti ungentobolea boksa</sup>  
<sup>walo-Vita. Vita-hali na Boot</sup>

Bibi huyu aendelea kuonyesha jitimai iliyomkumba  
baada ya mumewe kufia kazini ya wakoloni;

----- halafu wananiitukaaana, wananiita  
afriiiti, mleeevi, hayawaaaani, ha, ndiyo  
miii mlevi, sitowacha ulevi. Bila ya  
ulevi kwangu jitimai, ulevi hunichangamsha,  
hufifiza mawazo yaaaangu; husahau angalau  
----- (uk. 62)

Bibi huyu ndiye ametufunulia wazi wazi sababu ya  
baadhi ya maskini hujitosa katika pombe - ili "kufifiza  
mawazo". Twaona kuwa watu hawa huishi katika simanzi  
na jitimai na aghalabu huangukia katika mambo  
yasiyopendekezwa na kaida za jamii. Lakini, maadam  
wameponzwa wakaponzeka, hawana budi kujiingiza katika  
baadhi ya mambo (maovu) yale.

Mabepari wana dhuluma zisizo kifani. Walikuwa  
karibu kukivunja kibanda cha Pandu ili wapitishie  
barabara hapo kilipokuwa. Cha Bi-Kijakazi tayari  
kishavunjwa. Dhuluma hizi zadhihirisha jinsi haki  
za kibinadamu zinavunjwa. Mwenye nguvu amedhamiria  
kumuangamiza mnyonge kabisa - kwa kumnyang'anya cho  
chote alicho nacho.

Kwa kumalizia twaweza kusema kuwa Pandu Jaku  
ametumiwa na mwandishi kuwakilisha tabaka la chini  
kabisa la makabwela. Yeye hana kazi na autegemea  
mkono wake mrefu, ili kuyapata mahitaji yake muhimu -  
kama amwambiaavyo Kumba kuwa ukiwa na kazi au usiwe

nayo, utahitaji kula, kuva, kulisha watoto wako n.k.

Ameachwa na wazazi wake katika kaburi la simanzi na jitimai na mfadhili mmoja tu aliye kuwa naye Bi Kizee Staghafiru ametumbukia maradhi mabaya sana - T.B. na hatimaye anafariki. Hivyo Pandu aachwa bila mtunzi ye yote. Anadaiwa kope si zake. Mzee Siwa amemwandama vikali ili amlipe deni lake analomdai.

Katika kumchora Pandu Jaku na kumpa sifa za maskini hoe hae - asiye asili wala fasili, ~~msanii~~ amedhamiria kutueleza kinaganaga jinsi muundo wa jamii ile ulivyowaangamiza wanyonge. Wao wametengwa na kundi dogo la mabepari na wameachiwa waibe, ~~wau~~gue, wapigane, wale chungu na hatimaye wafe. Hali hii yatudhihirishia jinsi jamii za kibepari zinavyodhulumu nguvu na jasho la watu wa tabaka la chini.

Lakini wanyonge nao aghalabu wanaonyesha hisia za kuupinga utawala dhalimu. Wanachohitaji ni kuungana pamoja ili wachukue ala na kumuangamizia mbali <sup>Dhalim</sup> mdhalimu.

Ingawa mwandishi ameitunga riwaya yake kwa kuichora jamii ya Waswahili walio chini ya udhalimu wa Waingereza na unaizi wa Waarabu, hali iliyoko pia yaweza kunasibishwa na nchi zilizojinyakulia "uhuru wa bendera" ambapo dhuluma huendelezwa kwa mlango wa nyuma chini ya mfumo mpya uitwao ukoloni-mambo-leo.

3:4:4 FAUZ, FAROUK HILAL

Fauz na Farouk Hilal (Kibwana Jaku) ndio wanaowakilisha mfumo wa kibepari katika jamii - kama ulivyowasilishwa na mtunzi wa Dunia Mti Mkavu.

Hawa wanaliimarisha tabaka lao kwa kuwadhulumu wengine ili kuweza kuyalinda maslahi yao. Watu wa tabaka hili aghalabu ni makatili ambao hawana hata chembe cha huruma kwa wenzi wanaodidimia katika lindi la taabu na umaskini.

Ingawa Kibwana amejigeuza na kujikengeuza kuwa mzungu-mweusi - kwa mienendo na tabia zake, mathalani kubadili jina, yeye anatokana na familia maskini ya Mzee Jaku, mamake akiwa ni Bi-Pole. Lakini sasa, amegeuka kuwa msaliti, kibaraka na muuza haki za Waafrika maskini wenzake. Anaweza kumithilishwa na Karanja <sup>Tophet</sup> <sup>Yerath za kufa</sup> katika A Grain of Wheat,<sup>8</sup> ambaye kwa kuraiwaraiwa na Wazungu na kupewa vitamu na vinono, alikuwa tayari kuisaliti nchi yake na kuwauza watu wake.

Maisha ya Kibwana ya utotoni ni ya kusikitisha. Yeye aliuzwa na mamaye kwa Bi-wa-Minarani, kwa vile alikuwa amekose<sup>sh</sup>wa uzazi na Mungu. Kwa sasa, baada ya kukulia kwa Bi-wa-Mnarani, Kibwana ameshakuwa na madaraka ya 'Inspekte wa Polisi' baada ya kutoka Ulaya <sup>Sandhu</sup> kusoma. Lakini analichukia jina la Kibwana. Anajiita Inspekte Farouk Hilal.

Maisha yake Farouk ni tofauti na ya wale ndugu zake wengine, maadam hao wengine hawakushirikiana na wakoloni kuwatesa wenzao. Wao wanaukubali uhalisi wa maisha wala hawaукwepo wajibu wao wa kuupigania utu na maslahi ya wanyonge.

Nyumbani mwa Farouk mlikuwemo vitu kama vile "dressing table", kabati zilizong'aa kwa "yanishi" n.k. Yeye huenda kustarehe katika "mabichi" kama vile Alhashmin Beach. Farouk ni mtu mwenye kiburi na majivuno, na mara nyingi hupenda kuongea kizungu na kuwadharau watu wa taifa lake. Kwa mfano, alipomfungisha babake (Jaku) jela alisema;

It was quite clear. Oh yes, quite clear. It was murder. (uk. 76)

Anawapuuza ndugu zake na kuwaona wachafu, washenzi na watu wasiostaarabika. Tabia hii ya Farouk hupatikana sana hata katika mataifa mengine ambapo waliopata bahati ya kutajirika na kuwaelimisha wanao huwaona wenzio wasiobahatika kama washenzi. Wanaitumia elimu kama kigezo cha kuwaainisha watu kitabaka.

Kutokana na madaraka aliyonayo Farouk, anaishi maisha ya ulimbwende akistarehe hasa bandarini.

Inafaa ifahamike kuwa starehe zote za tabaka la akina Farouk zaghari miwa kutokana na jasho la watu kama vile Bakari Jaku, Kumba, Fumu Jaku n.k. Na huu ni

ubatilishaji wa haki na uendelezaji wa unyanyasaji.

Farouk amejiingiza katika ulaji rushwa, kama alivyomwambia Sakina wakati alipokuwa akihojiwa ili apewe kazi;

Kupeana ni kikoa, toa nawe upewe. Bila ya hivyo hakuna kazi. (uk. 84)

Alikuwa akitumia cheo chake kazini sio tu kujitajirisha bali pia kuiuza haki. Mazoea yake ya kula mrungula kama alivyomwambia mhindi mmoja;

How come ----- how can I buy him? How can I bribe him? A complete change; very wild he is, can't be tamed. (uk. 84)

Mwandishi pia anatueleza juu ya ubatilishaji wa haki baada ya wahalifu kumhonga inspeka;

Kwa pupa alichakura ripoti zilizokuwemo; ya kwanza, ya pili, ya tatu, hadi ya kumi na mbili ambayo ilikuwa juu. Hawa wote ni wahalifu ambao walikwisha toa mrungula kesi zao zififizwe; lakini wale kumi na moja hawakumshughulisha. (uk. 85)

Vile vile amemnyang'anya Bi Mwanaali kikataa chake alichorithi kutoka kwa wazazi wake. Anamsingizia kuwa ni mwizi na hatimaye anamlazimisha kutia sahihi

kwenye warka unaoonyesha kuwa yeye Mwanaali amefilisiwa kikataa chake kwa sababu ya deni ya shilingi mia tano aliyokuwa nayo kutoka kwa Bwana Subhash. *m Karim*

Vitendo vya Farouk vinaoana na vile vya Maksuudi katika Utengano, na vya Fuad <sup>KARIM</sup> *What type of man?* katika Nyota ya Rehema.

Rehema alipokonywa kijishamba chake kwa hila kama hizo alizozitumia Farouk kumpokonya Bi Mwanaali. Ama kweli, wanyonge wamo mashakani. Wao hawana mtetezi, maadam wanaowanyanyasha <sup>ndio</sup> ambao wamesimamia sheria, na sheria hizo zimetungwa ili kuyalinda maslahi ya <sup>ref</sup> *Haki* mabepari. Lakini, ukombozi hauna budi utokane na hao hao wanaonyanyaswa.

Fauz alikuwa mkoloni mwenye kuusimamia utawala wa kikoloni. Aliwatawala watu kwa 'ufito wa chuma' <sup>ina benaf</sup> wala hakujali maslahi ya wanyonge.

Alilolishughulikia zaidi ni kuona kwamba tabaka lake limehodhi mali bila kujali iwapo mali ile ilihodhiwa kwa njia halali au haramu.

Katika riwaya amechorwa kama katili mwenye moyo mgumu na asiyeona karaha kulitenda baya lo lote. Aghalabu watu wa tabaka la juu linalotawala na lenye uwezo usio <sup>na</sup> kifani hupumbazwa na mali na starehe mpaka haki wakaigeuza haramu, na haramu ikawa ndiyo haki kwoo.

Hisia za Fauz ni kama za madhalimu wengine, Farouk,

Maksuudi (Utengano), Zuberi (Asali Chungu), Fuadi  
(Nyota ya Rehema) n.k.

Karim  
nuru  
kati ug  
watu  
jua

Mienendo ya Fauz yatiwa nuru na jinsi anavyomtesa Fumu. Amemhini Fumu haki zake zote na kumuachia ukata na ghamu maishani mwake. Amnyang'anya mali (shamba), mazao na hata mpenziwe Masika.

Katika fani ya mbinu - rejeshi S. A. Mohamed anatudhihirishia unyama wa Fauz uliomfanya aliunguze moto shamba la Fumu lenye kipimo cha eka tatu za mahindi.

Kitwana ndiye anayemletea Fumu habari ya kuunguzwa moto konde lake, habari ambayo inamtia ghamu na kiherehere. Kitwana ameleta habari kuwa;

Konde yako imeunguzwa moto ----- imechomwa; imetiwa moto, hivi sasa watu wanamaliza kuizima, nimetumwa nije nikuite. (uk. 91)

Fumu naye, kwa hamaki iliyomjaa na kitetemeshi cha kilio alibwabwaja maneno ya ukali;

Fauz ----- umenichoma mkuki kwenye chembe cha moyo ----- Umenichoma kwa mara ya pili ----- mara mbili. Ardhi hii ya Mungu, ardhi hii niloipatia ta ----- ta ----- taabu -----.

Baada ya maneno haya, Fumu ametangaza vita dhidi

ya Fauz. Ama kweli uhalifu huu (wa shamba) umechochea chuki mionganini mwa wanaoonewa na kudhalilishwa. Hawachelei kifo, maadam wanafahamu kuwa kifo ni jambo la faradhi - hakiepukiki.

Mkabiliano baina ya Fumu na Fauz ni ukinzani baina ya mabwanyenye na <sup>matalake</sup> proletarii. Nao umati unaomwandama watuashiria ukakamavu na udhati wa wanyonge kuzipigania haki zao. Kuhusu kukabiliana kwa hawa wawili - mnyonge (Fumu) akiwa na mndu na mwenye nguvu (Fauz) akiwa na bunduki, mwandishi atueleza;

Nani asiyejua kwamba mbele ya bunduki mndu hausimami? Lakini huu ulikuwa wakati ambao kwamba maovu yalifika ukingoni na unyonge ukamshajiisha mwanadamu ayasukume maovu yaporomoke na kutokomea moja kwa moja - ingawaje yanatisha kama kuishi kuchungu, kifo huwa ni kitamu. (uk. 95) - <sup>Sikata tamaa napojin'</sup>

Fauz, kama ilivyosemwa awali anawakilisha nguvu za ubeberu na ubepari. Analitekete <sup>sho</sup> moto konde la Fumu kwa vile anafahamu dhahiri shahiri kuwa tabaka lake ndilo lenye nguvu. Bunduki yaonyesha ishara ya nguvu zake. Lakini hata hivyo, walioonewa wameamua kulipiza kisasi ijapokuwa ala zao ni hafifu. Lakini wana imani thabiti kuwa hatimaye watashinda.

3:5 HALI YA UCHUMI NA HISIA

ZA MWAMKO ZA WANYONGE

Glicksberg (1976) ametoa maoni kuwa;

*Ki-muz  
kinak.*

Uhakiki wa kifasihi wa Ki-Marx huchungua athari za kiuchumi katika wakati fulani ki-historia na husisitiza mtafaruku wa kitabaka ambao hujitokeza kutohana na siasa hizo za uchumi.<sup>9</sup> (Tafsiri yangu)

Maoni haya ya mtaalam huyu ni muhimu sana na yatatuzaa sana katika kuitafiti na kuinakidi hali ya uchumi na jamii ya wanyonge katika Dunia Mti Mkavu.

Ukinzani wa kitabaka unaletwa na usimamizi mbaya wa uchumi - ambapo tabaka la wachache huhodhi sekte (*nyenye nyanya*) za kuzalisha rasilmali na kulitumia tabaka la chini kama vyombo vyaa uzalishaji kwa urahisi. Hilo tabaka la chini nalo bila shaka unafika wakati ambapo linatambua kuwa linanyonywa nguvu kwa faida ambayo halipati. Ni katika kujinyakulia uhuru wa kiuchumi na kisisasa na kiutamaduni ambapo mtafaruku unazuka. Aidha, wanaoumiliki uchumi wanaona kuwa kuwatenda haki wakulima ni sawa na kuhatarisha maslahi yao - pamoja na faida wazipatazo. Vile vile ni kuhatarisha maisha yao ya starehe na anasa, Hii ndiyo sababu tunaona kuwa kila mmoja amepashikilia pake kwa nguvu. Mabwanyenye washikilia dhuluma dhidi ya wanyonge, wanyonge nao washikilia kuwa lazima waundoe utumwa na unyanyasaji

ili wawe huru na waweze kuutambua utu wao.

Katika Dunia Mti Mkavu, uonevu wa dhahiri ndio unaozusha migongano baina ya matabaka. Mzozo wa kiuchumi unawapiga watu, mithili ya dhoruba kali, na kuwaacha katika hali ya mashaka na ya kutamauka. Hali hii ndiyo iliyowakumba, Mzee Gae na Fumu Jaku, Imewapa tajriba kwamba ukombozi hauwezi kupeanwa kama zawadi. Ni lazima upiganiwe. Wametambua pia kuwa, "amani haiji ila kwa ncha ya upanga". wazo la namna hii pia limeshikiliwa na Paul Freire (1968), aliyesema kuwa;

Uhuru hupatikana kwa kupiganiwa wala si  
kwa kutolewa kama hedaya.<sup>10</sup>

Freire pia ameyaendeleza maoni kuwa hakuna mtu mwingine awezaye kuuelewa umunimu wa ukombozi isipokuwa yule anayetawaliwa, hivyo, ukombozi hauna budi utokane na hao hao walionyanyaswa.

Katika riwaya tunayoitafiti, hisia za wanaodhulumiwa zimebainishwa kinaganaga kwa mfano, katika mifano ya maneno yafuatayo;

"Mwili wake umehimili sulubu na mateso toka mja yeye kutumbukia katika shimo hili la dunia!" (uk. 1) (Fumu)

"Mungu tupe nasi, angalau nguvu za jasho letu \_\_\_\_\_. " (uk. 5) (Fumu)

"Mimi nakula jasho na nguvu zangu bwana."  
(uk. 9)

"Kero, Kero. Nipe nini sijui; mara  
matapishi, mara mate, mara madenda, mara  
mkojo, mara <sup>Lingai, Verle</sup> ~~-----~~. "(uk. 28) <sup>bi ntumwa</sup>

"Mmoja alikuwa mkulima hodari, lakini  
amefukuzwa kwenye ardhi ya watu." (uk. 43)

"Mwenye nacho na asonacho huwaje sawa?"  
(uk. 59)

"Maonevu; alisema kimoyomoyo." (uk. 86)

"Leo imefika kikomo cha kuwaonyesha hawa  
madhalimu, mwacheni Fumu ende, na sisi tuko  
nyuma yake, na atuue sote." (uk. 94)

Hali mbaya ya uchumi iliyowasakama wanyonge  
yaonyeshwa na jinsi watu hao walivyoishi. Kwa mfano,  
kibanda cha Fumu kilikuwa na;

Kitanda cha kamba alichokikalia chenye <sup>mwakim</sup>  
tendegu moja lililoteguka, kiti cha marimba  
kilicholalia yombo, jembe lililolika bapa  
kwa kuchuana na ardhi limesimama wima  
kipembeni ~~-----~~. (uk. 3-4)

Mlikuwemo na vitu kadha vilivyoonyesha hali yake  
ya chini ya maisha kama vile - majifya matatu, gunia

bovu, mararu ya shati na shuka n.k. Hali hii ya kibanda  
cha Fumu <sup>Sq 56</sup> yanasisibishwa na hali yake mwenyewe ya uchofu,  
udhaifu na upweke - yote yanayotokana na mfumo wa  
utawala na vile vile wa uchumi. Fumu anadhalilishwa  
zaidi pale anapopokonywa kishamba chake na Fauz.

Fauz asema;

Tokea leo, vipando hivi ulivyopanda ardhini  
petu si vyako. Na kuanzia sasa, huruhusiwi  
kulima katika shamba hili la Hamoud bin  
Said. Huruhusiwi kulima wala kupanda cho  
chote - kwa heri. (uk. 9)

Kupokonywa huku kwa shamba bila haki yo yote  
kwamuweka kabwela taabani kiuchumi. Baada ya  
kunyang'anywa kijishamba chake, ambacho kilikuwa  
tegemo lake la pekee, Fumu ameachwa aangamie duniani  
bila cho chote.

Ingawa wafanyakazi ndio wanauinua uchumi wa nchi,  
uchumi huo umesimamiwa na makabaila wachache. Mzee  
Gae anamuuliza Fumu;

Hebu jiulize swala rahisi hili: Kwa nini  
unashindwa kupata kijiti cha kibiriti  
kuwashia moto? Na wewe unalima, unafuga  
wanyama ----- (uk. 12)

Swali hili la Mzee Gae ni muhimu sana. Ni swalii

linalompa mkulima motisha ili atafakari jasho lake linakokwenda iwapo yeye hufanya kazi katika viwanda vinavyotoa bidhaa nyingi na zenyenye thamani kubwa lakini yeye hawezizupata bidhaa ndogo ndogo muhimu. Hivi ni kuonyesha kuwa alimaye siye anayekula, na anayechoka halali, hulala aliye mzima.

Hali mbaya ya kiuchumi imewaangamiza watu wengi katika Dunia Mti Mkavu. Wengine wametumbukia maradhi mabaya, wengine wamegeukia wizi, wengine wameshiriki ulevi ili kujisahaulisha dhiki na wengine nao wanawauza watoto wao kwa matajiri ili wajipatie riziki n.k. Ili kuziondoa hali hizi, wanyonge wamemaizi kuwa hakuna njia nyingine ya kuepukana nazo ila kwa kuung'oa udhalimu; na hapa ndipo watu wanapata hisia za kuwazindua ili kuyaleta mapinduzi, sio tu ya kiuchumi, bali pia <sup>Political      Social      traditional      falan</sup> ya kisiasa, kijamii na <sup>cultural</sup> kiutamaduni. Juhudi hizi zadhihirishwa na harakati za ukombozi zinazopatikana katika mgomo.

Dhuluma zilizowachochea watu chuki na kuzusha zahama ni kama vile - kunyang'anywa na kuteketezewa mashamba, malipo duni kwa kazi ya sulubu, kufungwa jela bila hatia (kama Mzee Jaku Shonge), na kunyimwa haki kwa jumla

Hisia za wakulima, wafanyakazi, makabwela na wengineo zawachochea waitishe mgomo - kwa imani kuwa;

Mgomo wetu hata kama hautafuzu, utasaidia  
kuona matokeo, maana wazee wetu wamesema,  
gonga gogo usikilize mlio -----

Mgomo huu ni mwanzo wa kuwajulisha kwamba  
wakati wa mtu mweusi kujua haki yake  
umefika, mwanzo wa kutetea haki zetu.

(uk. 102)

Imani ya watu hawa ni kama ile ya Wamatumbi  
katika tamthilia ya Kinjeketile.<sup>11</sup> Kinjeketile alizua  
'neno' ambalo aliamini lingekuwa mbegu ya uzalendo na  
umoja katika kumpinga Mjerumani. Kwa hivyo, ingawa  
wanyonge hawana nguvu, wana imani kuwa safari ni hatua.

Mgomo unaendelea na ingawa watu wengi wamekamatwa,  
ngomo huo hauishi.

Maneno ya Mzee Gae anapo jitetea mahakamani  
yafanana na ya Dedan Kimathi /na Steve ~~Forko~~ <sup>Freedom</sup>  
mahakama ya kikoloni. Mzee Gae auliza;

*Nyoka tokea lini kumpa chura nafasi*  
*ajitetee? Ni udangamifu tu; sisi tuko*  
*hapa na nyinyi mko huko, tumezeni kama*  
*mlivyo zoea kumeza, tumezeni, tumezeni,*  
*sisi tumo kinywani mwenu.* (uk. 113)

Kimathi naye katika Mzalendo Kimathi anaikejeli  
mahakama ya kikoloni;

Wanasheria waongo, wenyе benki, wenyе  
mali -----.

KIMATHI: Katika mahakama ya kibeberu! Hamjakuwa na hamtakuwa na haki sawa kwa wananchi walio chini ya ubwana huo. Haki na usawa vinaundwa kutokana na mapambano ya mapinduzi. Kupinga uonevu wote na ubwana.  
Mapambano yetu kwa hivyo yataendelea.<sup>12</sup>

Kimathi, kama vile Mzee Gae anawatia watu shime na kani kuwa mapambano yataendelea.

Katika Dunia Mti Mkavu, ingawaje baadhi ya wapinzani wameuawa, wengine wayaendeleza mapinduzi na hatimaye mvua kubwa inanyesha - ishara ya maisha na mapambano mapya.

### 3:6 KIMALIZIO

Kwa utafiti uliofanyiwa kipengele cha "Uchumi" katika sura hii, tumejaribu kubainisha uhusiano ulioko baina ya wanyonge na uchumi. Tumejizatiti kudhihirisha kuwa usimamizi mbaya wa uchumi na muundo wake katika jamii husababisha mtafaruku na ukinzani baina ya mabepari na makabwela. Jambo muhimu la kuzingatia ni kuwa ukombozi wa kundi lo lote linalonyanyaswa hutokana na watu hao wenyewe, wala hautoki nje ya kundi hilo. Wamesema Waswahili kuwa "kitanda usichokilalia hujui kunguni wake". Licha ya hayo, wakasema kuwa "Adhabu

ya kaburi aijua maiti".

Kwa kuwatumia wahusika kama viwakilisho vya jamii, tumejadili maudhui mbali mbali katika riwaya - hasa ile itikadi ya msanii kuwa bila haki, mtafaruku hauishi. Itikadi hii pia ndiyo wameishikilia wanyonge. Wanaamini kuwa hata wakipata idhilali na jitimai jinsi gani, hawana budi washirikiane kwa umoja na stakiri na hatimaye watashinda.

Tumeona kuwa ni muhali kumnyamazisha mnyonge milele maadam yeye anahisi kuwa jambo fulani limeenda kombo. Amepata hisi kuwa si mkadara wake kuteseka katika udhalimu wa makabaila wachache. Yeye ni binadamu kama wengine, anahisi, anaona, anasikia, anafurahi, anahuzunika n.k. Kwa hivyo, hawezi kuukubali uonevu unaosababishwa na walafi wachache wenye inda na ubinafsi.

Wanyonge wanaupinga udhalimu kwa hali na mali na haionekani kuwa watakata tamaa, maadam wanapigania haki na utu wao.

Katika sura hii, mashauri anayotoa mwandishi katika jamii ni kuwa wale wanaoendezea dhuluma wanajichimbia makaburi yao. Anawatahadharisha kuwa "hakuna refu lisilokuwa na ncha". Kwa hivyo, ni muhimu wadhalimu hao wafahamu kuwa starehe na anasa zao kutokana

na jasho la wanyonge haziwezi kuishi milele maadam  
wanyonge wamepevuka na kupata hisia za mwamko kwamba  
wanaonewa.

3:7 TANBIHI

1. Abdulazizi, M. H., Muyaka, 19th Century Swahili Popular Poetry. K.L.B. Nairobi, 1978 (uk. 67).
2. Crystal & Davy, Investigating English Style, Longman Group, 1969.
3. Ngugi wa Thiongo, A Grain of Wheat, Heinemann, London, 1968.
4. Abdalla, A., Sauti ya Dhiki, O.U.P. Nairobi, 1973
5. Ngugi & Mugo, M., Mzalendo Kimathi, Heinemann, Nairobi, 1978.
6. Marx, K. & Engels F., The Communist Manifesto, Penguin Books, 1968.
7. Kama namba 5, juu (uk. 74).
8. Kama namba 3, juu.
9. C. I. Glickberg, The Literature of Commitment, London Associated Press (uk. 70).

10. Freire, P., Pedagogy of the Oppressed, The Seabury Press, New York, 1968, (uk. 31).
11. Hussein E., Kinjeketile, O.U.P. Nairobi, 1969.
12. Kama namba 7, juu.  
*use the correct  
footnoting format*

## S U R A Y A N N E

4:0 ASALI CHUNGU

4:1 UTANGULIZI

Asali Chungu ndiyo riwaya ya kwanza aliyoianika Said Ahmed Mohamed. Aliandika mnamo mwaka 1978 - mwaka ambao pia alihitimu masomo yake ya chuo kikuu cha Dar-es-Salaam na kupata shahada ya B.A.

S. A. Mohamed anakiri kwamba hakuisawirisha riwaya ya Asali Chungu kama vile alivyofanya katika Utengano au hata Dunia Mti Mkavu. Anasema kuwa aliipanga Dunia Mti Mkavu ipasavyo; lakini amejusurisha katika kuiandika Asali Chungu. Hata hivyo, hamaanishi kuwa Asali Chungu ina makosa na Dunia Mti Mkavu haina. Anavyosema ni kuwa ploti katika Dunia Mti Mkavu inajitokeza kwa wema zaidi kuliko katika Asali Chungu.

Maadam riwaya hizi zote tatu - Asali Chungu, Dunia Mti Mkavu na Utengano ni za mwandishi mmoja, sura hii itatafiti Asali Chungu kwa ujumla. Sababu yake ni kujiepusha na kuyarudia yale ambayo tayari yamekwishatajwa katika sura zilizotangulia. Tutaitafiti maudhui ya riwaya hiyo, hasa tukitilia mkazo hali ya kisiasa katika jamii tuliyopewa na mwandishi.

Lengo ~~letu~~, kama ilivyo madhumuni ya jumla ni kueleza jinsi wanyonge wanavyojitokeza riwayani.

4:2 MAUDHUI

Kichwa cha riwaya hii "Asali Chungu" kimekita  
katika kinaya. Ni jambo lisilowahi kutokea asali  
ikawa chungu. Sifa tuzijuazo za asali ni kuwa ni tamu  
kupita kiasi. Katika Kiswahili, zimetokea methali  
kadha zinazoisifu asali kwa utamu wake. Methali hizo  
ni kama vile; "Chovya chovya humaliza buyu la asali",  
"Mchovya asali huchonga mzinga", "Mchonga mzinga  
hakatazwi asali", "Mchovya asali hachovi mara moja",  
n.k.

S. A. Mohamed ameitumia jazanda ya asali ili  
kuubainisha uovu unaoendelezwa katika jamii.

Anatueleza kuhusu jamii moja ya kinaizi ambayo  
iliishi katika ulimbwende huku wengine wakiungulika  
katika umaskini. Ametuonyeshä kuwa starehe na anasa  
ndicho kiini cha uovu katika jamii.

Kama alivyofanya katika riwaya zake nyingine,  
wahusika wake amewachora katika matabaka. Tabaka la  
mabwanyenye na tabaka la mafukara. Zuberi ndiye  
anayewakilisha tabaka la mabwanyenye hali wahusika  
wengine duni kama vile Dude, Semeni n.k. wanawakilisha  
tabaka la makabwela.

Tabaka la mabwanyenye ndilo linalotawala na ndilo  
lenye mali. Kwa hivyo, maisha ya maskini yategemea

hilo kundi la wachache ambao ndio wamemiliki kila  
kitu - mali, mashamba, kazi, haki n.k. Ndio wenye  
majumba ya ~~kukoo~~<sup>Kukoo(Bsh)</sup> desha, maduka n.k.  
*Silly*  
*ba'otong'*?

Jambo moja linalojitokeza katika tabaka hili  
la juu ni kuwa ni tabaka linaloendeleza ujisadi,  
uonevu, udhalimu, mateso na maovu mengine ya kijamii.  
Siasa na mali zinampa mtu uwezo na mamlaka yasiyo  
kifani - ambayo yanatumiwa kuwadhalilisha wanyonge.

Kwa jumla, maudhui ya riwaya ya Asali Chungu ni  
uonevu ulioko katika jamii - unaoendelezwa na tabaka  
dogo la wachache ambalo ni lenye nguvu, na uwezo wa  
kisiasa na kiuchumi.

Watu hawa wachache wanaingilia maisha ya starehe  
na kuwasahau wale wanyonge wanaozichumia hizo starehe  
zao. Mwandishi anatueleza kuwa starehe kama hizo zina  
mwisho wake, kama tunavyoona kuhusu maisha ya Bw. Zuberi  
na jamaa zake.

#### \* 4:3 HALI YA KISIASA KATIKA ASALI CHUNGU

Hali ya kisiasa katika riwaya hii hudnihirisha  
kuwa wanaopewa madaraka ya kuwaongoza wengine huyatumia  
vibaya mamlaka yao. Haya yaonyeshwa na Zuberi. Yeye  
ni mkuu wa wilaya, lakini hautekelezi wajibu wake  
ipasavyo. Jambo linalotuonyesha kuwa ameshindwa kutekeleza  
jukumu lake ni makundi ya watu wanaofika ofisini mwake

kila asubuhi kuwasilisha malalamiko yao. Wote hawa waonyesha jitimai katika nyuso zao, na kila mmoja amekuja kumuona Bw. D.C. kwa tatizo au matatizo fulani. Wengine wamesubiri kwa muda mrefu sana - karibu wakate tamaa, kama tuelezwavyo;

Bi Pili, stahamala zinemwisha. Anachacharika baoni tayari kumvunjia mbarika Bw. D.C. (uk. 1)

Kuna pia vikongwe, wanawake wa makamo, na vile vile wasichana au "maspoti" kama wanavyoitwa na mwandishi. Baadhi yao walifika ofisini kabla ya ofisi kufunguliwa, asubuhi na mpaka saa nane hivi mchana hawajaonana na Bw. D.C.

Kila mmoja kati ya wanawake wale ana taabu yake. Wengine wamekuja kudai walipwe fidia baada ya kuharibiwa mashamba yao na ng'ombe wa Bw. D.C., wengine mashamba ~~yao yamefyekwa kwa amri za Bw. D.C.~~

Malalamiko haya na mengine mengi yanatuonyesha jinsi katika jamii za kinaizi viongozi kujipatia nguvu na uwezo mwingi wa kisiasa. Bwana D.C. achukuliwa kama ndiye mwokozi wa wanyonge. Naye, anayatumia mamlaka yake kuwadhalilisha wanyonge hao - badala ya kuwashudumia na kuwasaidia ipasavyo.

Wanyonge wanawasilisha malalamiko yao kwa mfano wanaposema;

Bahati ni ya warembo na wenyе sura zao!

Mwenzetu katupita hapa! Katuona sisi  
vyuma, hatugunyuki na bao. (uk. 2)

Haya ni malalamiko ya wanyonge kulaani mapendeleo  
ya Bw. Zuberi. Anawapendelea warembo labda ambao hata  
hawana malalamiko yo yote - na kuwapuza wenyе shida  
za dhati.

Ufisadi wa namna hii umeenea kwa mapana na mafuru,  
sio tu katika Asali Chungu bali pia katika jamii  
zingine.<sup>1</sup> Baadhi ya maofisa wamezifanya ofisi za  
serikali kama nyumba zao. Mle ofisini wanapanga  
shughuli za magendo, ufisadi na uhaini. Wanapouendeaza  
uovu huu, wanyonge wanalia kwa kuonewa bila la kufanya  
kama asemavyo mmoja wao katika riwaya;

Tutafanya je dada na sisi hatuna sauti? (uk. 3)

Huku kukosa sauti kwa wanyonge kunawapa wakubwa  
fursa ya kuyaendeleza maovu yao. Kwa mfano, Zuberi  
anamnajisi mtumishi wake wa nyumbani (semeni), wala  
(Zuberi) hafuatiliwi na sheria maadam yeye ni sheria  
na sheria ni yeye, kama tuelezwavyo na Hussein (1971); 32

Mimi ni nguvu na nguvu ni mimi. Mimi ni  
uwezo na uwezo ni mimi.<sup>2</sup>

Tarishi wa Bw. D.C. amechorwa kama mwakilishi  
wake. Huyu ni mfano wa watu katika jamii ambao huitwa

*Storage*  
zuge. Bw. D.C. amenzuga akili kiasi cha kuwa yeye

huandama tu anayeamrishwa bila kutafakari sababu.

*10 a.m.  
Dred Mor*

Yeye anashuhudia udhalimu wa Zuberi lakini hajiulizi  
*Police na  
chuo libumu  
boot riders*

Bi Pili ametumiwa kama sauti ya wanyonge ya  
kuupinga uonevu wa Bw. D.C. Yeye anampasulia mbarika  
kwa kusema;

Bwana wewe, mtukufu wa jina na tajiri  
mwenye uwezo ----- Mungu kakupa mengi,  
lakini kakunyima akili na maarifa.

Nakwenda zangu, lakini nakwambia: umekula  
wa mwenzako, miguu itakwelekea. Mungu si  
Athumanani. (uk. 6)

Maneno haya yaonyesha laana za wanyonge dhidi ya  
wanaowadhulumu. Wanateswa bila hatia

4:4 MAISHA YA JAMII KATIKA ASALI CHUNGU

Jamii aliyoichora S. A. Mohamed katika riwaya hii  
ni ya kibwanyenye na kibepari. Kama jamii nyingine  
zinazoifata mifumo hiyo, jamii hii ina kundi dogo la  
watu ambao hujitajirisha binafsi bila kujali maslahi  
ya walio wengi. Katika jamii ya namna hii pia hutokea  
tabaka mbili zinazopingana - tabaka la watawala na  
watawaliwa, mabwana na watumwa.

watu wa hali ya chini huishi katika umaskini

usiokwisha maadam sidha wameajiriwa kazi ndogo ndogo  
na za sulubu au <sup>Neno naisibul. no nge ajutaka</sup> hawana kazi kabisa. Baadhi ya <sup>Kungo</sup> <sup>"other" ??</sup>

walioha kazi ni kama vile; wapishi, watumishi wa nyumbani, walinzi n.k. Kazi zile kubwa kubwa hunyakuliwa na jamaa za mabwana wakubwa. Wanapofanya hivyo huwa wanaliendeleza tabaka lao. Kwa hivyo maskini huzidi <sup>? ?</sup> kumaskini<sup>ka</sup> na tajiri huzidi kutajirika.

<sup>Utenago</sup> <sup>not even a verb</sup> <sup>Kasri</sup>  
Tukiangalia hali ya chumba cha Bw. Zuberi twaweza kuelewa tofauti iliyoko baina ya mifumo miili ya ubwanyenye na <sup>nhasabi</sup> <sup>Jumba laido</sup> <sup>Chumba hicho</sup> <sup>lina ucan</sup> <sup>ya room</sup> <sup>wala sio</sup> proletarii. Chumba hicho kimeelezewa <sup>understatement</sup> <sup>How?</sup> <sup>red you want me</sup> <sup>One like you</sup> <sup>lina vole</sup> <sup>in my vole</sup> <sup>Na</sup> <sup>lina vole</sup> <sup>in my vole</sup> kuwa;

Taa zake za therea zilizokuwa zikininginia, zilimwitikia pamoja, zikamwaya anga la kupendeza kwa matungi yake ya feruzi yaliyosanifiwa kwa muundo wa mikonga ya tembo. Kwa mwanga wa feruzi uliostawisha kuta za maziwa, uzuri wa ukumbi ukaanza kujifaragua. (uk. 8)

<sup>Kasi la</sup>  
Ama kweli, Zuberi aliishi katika chumba cha fahari kama kile cha Maksuudi katika Utengano. <sup>I</sup> Chumba <sup>chake</sup> <sup>kinao-ana na dhima na mamlaka yake. Ingawa anaishi</sup> kwa raha mustarehe, Zuberi hatosheki. Anaendelea kuwanyang'anya maskini rasilmali yao iliyo haba. Kwa mfano, anataka Mzee /Omari awe akitoa sehemu ya mazao

Banya

yake na kumpa yeze Zuberi. Ingawa anadhulumiwa haki  
yake, Mzee Omari hajakata tamaa. Msanii anatueleza  
kuhusu Mzee Omari;

Boqa

Hata hivyo, Mzee Omari alikataa kufa moyo,  
na kama alivyo, muumini wa Mungu, alitaraji  
kwamba itakuja siku ambayo Mungu atawafungulia  
milango ya rehema. Aliomba tu siku hiyo  
ifike hima, ama si hivyo, itafika siku  
ambayo mtu ataambiwa amtoe mame chanje ikiwa  
leo anaambiwa amtoe binti yake. (uk. 23)

Umo hukuka?  
(uk. 20)

Mapinduzi si lele Mama, ya hifiji kusitua Mhang'z

Mzee Omari anayakubali mateso ya Zuberi kwa vile

huyu wa kwanza ni mnyonge, hali wa pili ni mwenye  
nguvu. Lakini ana imani thabiti kuwa siku moja Mungu  
atawahurumia wanyonge na uonevu utafikia kikomo. Na  
hii itakuwa ni siku ya mapinduzi. *bebwa*

Thabiti  
atakubali

No way!

Zuberi anashiriki katika mambo mengi ya ufisadi.  
Anatumia uwezo na mali yake kumfisidi na kumpumbaza  
Biti Daudi ili amshwishie <sup>binti</sup> wasichana wa watu aweze  
kukinaisha uchu wake. *asenki / Nyoge yake! - utariboo wote!*  
*Vakaa aselele* *Ache Kikwemba*

wakati Zuberi anajisaga katika ulimbwende, watu  
wengine kama Dude wanaangamia katika umaskini. Dude  
aliachwa katika hali ya jitimai na mamake Semeni  
alipofariki. Alipoona hana njia ya kujikomboa kutoka  
katika umaskini, yeze na wenziwe walijiingiza katika  
ulevi *usiokuwa na kipimo*. Yeye (Dude) na wenzake

*Kipimo cha ulevi  
ni kipi jumani?*

kama vile Bushiri hawana kazi bali wataraji kuishi katika ulimwengu uliojaa uhaini. Twaelezwa kuhusu hali ya maisha;

Kukosa kazi kulikuwa kwingi kuliko kupata;  
na hata kama kijana mmoja alipata, ilikuwa  
*Vlsls* kazi ya kuosha vyombo, kupika au kufagia-  
*Vlsls* fagia kwa wahindi; au pengine iliwabidi  
wawe wapagazi au wapara samaki Forodha ya  
Papa ----- Kazi njema zikawa za mabwana  
na matajiri. (uk. 77)

Hali ya umaskini yamfanya Dude aikose tamaa ya kuishi - kwa vile kazi zapeanwa kutegemea uhusiano baina ya mwajiri na mwajiriwa. Jambo muhimu analotufunza mwandishi ni kuwa, "aliyekupa wewe kiti ndiye aliyenipa mimi kumbi". Zuberi ametumbukia \*

maradhi ya moyo, na hapo ndipo (Dude) anapopata

nafasi ya kujilipizia kisasi. Anamhaini Zuberi kwa

D. *Anlingali omjua* *Z. Yomo mwajiriwave-basi!* *Anongi* *wie* *ndiye* *zuberi* *na* *mkewe* *Zuberi* - Bi Amina. *ni* *sadda* *wala*

? *Sadki* *ku.* ? *\*Modulazis* *na* *Vitaa* *Zuberi* *na* *mkewe* *zuberi* *na* *mkewe*

Dude anastarehe na mke wa Zuberi - wanaingilia starehe kama vile kukoga mwaka, kusafiri huku na huku wakijisaga katika starehe mbali mbali za kibwanyenye.

Kwa kueleza kwa kirefu kuhusu maisha ya starehe na anasa kisiwani na mashambani, S. A. Mohamed amedhamiria kuukejeli ubwanyenye kwa ulimbwende wake, huku wengine wanateseka katika umaskini.

Anatueleza jinsi Dude na Bi Amina, na baadaye Shemsa waliishi katika majumba ya fahari na yenye <sup>(Bar)</sup> utukufu, huku wengine kama vile Bushiri wanaangamia kwa njaa.

\* Kwanza Dude  
Kuanzita yepo-usuli  
wave mamuli wa taba - iena  
Bushiri si mchode nii! Senya mzga bwe!  
at Sup!

Vile vile anatuonyesha jinsi watu fulani wanavyoweza kuibadili mienendo yao wanapopanda katika tabaka la juu. Dude ni mfano bora wa ubadilishaji huu wa tabia na mienendo. Yeye amekuwa kama afriti. [Anashiriki katika mapenzi na "mamake wa kambo" - Bi Amina.] <sup>Nini? Hakuja kamei ana ulusiano Bi Amina</sup>

Kisha anamuoa Shemsa - bintiye Amina na vile vile <sup>uvu</sup> afanya mapenzi na Latifa - dadaye Shemsa.

\* Simlaumu Sava - ~~Mwiliwa~~ Iwa mda uregu - upalapo vinova maadui Si lolote, simlote - ndio niviotouai!

Vitendo vyake vyatuonyesha uovu unaoambatana na anasa na mali. Vile vile vyatuonyesha jinsi jamii ya matajiri ilivyotapakaa uovu wa kila aina. Bi Amina

Kwa upande mwingine, wanyonge hawawezi kuvumilia dhuluma za mabwanyenye huku wao (wanyonge) wakiangamia katika ultima. Wanaamua kuupinga udhalimu kwa kuteketeza mali za matajiri. Hatua hii yaonyesha kuwa wanyonge wako tayari kujikomboa na kuuangamiza ubwana na unyanyasaji.

#### 4:5 WAHUSIKA

Ni muhimu kuchunguza sifa za wahusika wawili ili tuweze kubainisha hali ya maisha katika jamii iliyojengeka katika matabaka. Wahusika hao ni Zuberi na Dude. Hata

hivyo utafiti wa sifa zao utafanywa kwa kifupi, maadam mengi kuwahuusu yameshatajwa katika sehemu zilizotangulia.

\* 4:5:1 ZUBERI

Zuberi ni mmojawapo wa wale walionufaishwa na mfumo wa kikoloni na kibwanyenye. Labda, kwa kushirikiana na utawala dhalimu, ameweza kupewa madaraka ya kuwa mkuu wa wilaya. Yeye ni mwakilishi na mlinzi wa maslahi ya mabwanyenye wachache katika jamii. Ni mvivu na anaipotosha haki kwa kuyatumia vibaya mamlaka yake. Zuberi ni mzinifu, na vile vile, anakitumia kipawa na cheo chake kufanya hila ili afanye mapenzi na wasichana wa watu.

Hafai kabisa kuwa mkuu wa wilaya maadam utawala wake, badala ya kuongoza, unapotosha.

Uovu wake wajidhihiri wenyewe pale ofisini mwake. Amewatendea watu hiana, na vile vile, badala ya kuwatatulia matatizo yao anawadhili zaidi. Wengine wamefika hapo takribani wiki mbili. Kutokana na anavyolaaniwa na wanawake waliofika pale ofisini, Shahada Matope inaeleweka wazi wazi kuwa Zuberi hapendwi na watu anaowatawala. Hawampendi kwa vile ni mla rushwa, Shahada Matope mnyang'anyi, na vile vile anafurutu ada za kiutu. Anayachoma moto makonde ya watu na vile vile kufanya uharibifu wa kila aina.

Siku alipolala na Semeni (bintiye Bi Pili) ndipo

huyu kappi  
Shahada Matope

Zuberi alipoiramba asali chungu. Alimpachika mimba mtumishi huyo (Semeni) na akamzaa mtoto - Dude. Dude huyu ndiye aliyemwendea kinyume Zuberi na akawa anaingia faraghani na Amina - mkewe Zuberi.

Huu u Sadja tu  
Kusini la Mwanza

Vitendo hivyo vyote vya uzinifu vyatudhihirishia kuhusu maovu yanayoambatana na anasa.

Watw wengi wapatapo mali na madaraka hufikiria tu jinsi wanavyoweza kutumia mali zao kujinufaisha wenyewe. Aghalabu hufanya hivi kwa ubinafsi na uroho wao. Jambo hili ndilo linalomwongoza Zuberi kutaka kumiliki kila kitu duniani. Anataka kumiliki wake, mabinti za watu, majumba, mashamba na vile vile jasho la maskini.

Uovu aliouanzisha ndio unaomwangamiza. Pengine mwandishi amemfanya Zuberi afedheheke ili kutuonyesha kuwa "hakuna refu lisilokuwa na ncha". Yeye aliutamani ulimwengu kupita kiasi, bila kufahamu kuwa utajiri na anasa ni vitu ambavyo mtu ataviwacha hapa duniani.

Ameiacha mali yake ipondwe na Dude - mtoto wa mtumishi wake (Semeni). Kifo cha Zuberi cha fedheha ni funzo kwa wachache ambao hupanda ngazi na kuwasahau walio chini. Ingefaa wafahamu kuwa "aliyekupa wewe kiti ndiye aliyenipa mimi kumbi". Huu ni waadhi aula hasa kwa jamii ambayo yaelekea kuteketea kwa maovu yake.

Mary ya  
ngaoz sasa?

4:5:2 DUDE

Dude ni mtoto haramu aliyezaliwa kutokana na uzinifu wa Zuberi (na Semeni). *fahamu Semeni*  
*Vizuri kihawa maji!*

Dude alikulia katika hali ya umaskini mpaka pale

Bi Amina alipopendekeza kuwa (Dude) aje arithi mali  
ya Zuberi. Kisa cha Dude na mamaye wa kambo - Amina

chakaribiana na kile cha Edipode katika Mfalme Edipode.

\*Oedipus complex - infano mwana! Edipus alivuwa ayalu  
 Tofauti iliyoko ni kuwa Dude hakumuua babaye wala Yose  
Dude wajui unusiano  
hakumuoa mamaye, isipokuwa alizini naye na hatimaye  
akamuoa binti Zuberi - Shemsa. Isitoshe, jililala na  
Laifia (dadaye Shemsa) na akampa mimba. Kutoka hakumuua akandungu mivila  
akampa mimba hakumuua akandungu mivila  
akampa mimba hakumuua akandungu mivila

Uzinifu huu wa Dude waoana na jina lake. Tabia na mienendo ya Dude yafanana na ya mnyama ay punguani.

Pengine hiyo ndiyo sababu mwandishi akampa jina hilo.

Lakelostishwa Akili curious curious curious curious?  
 Baada ya kurithishwa mali, anaanza kuponda raha na Bi Amina. Hapa twafahamikiwa jinsi mnyonge pia  
 akipata nguvu anavyoweza kuwadhulumu wengine. Awali  
 maisha ya Dude yalikuwa ya umaskini. Alikuwa amefungwa jela na akateseka kwa mapana na marefu. Baya na merake, Hakundidhunu  
ye tote, Anasarchea

Lakini hivi leo tunamuona anavyoingilia raha na kujiingiza katika maovu yale yale Zuberi - babake aliyoyatenda. Katika jamii nyingi jambo hili hutokea. Mtu wa hali ya chini apatapo cheo huwasahau kabisa na kuwapuuza aliowaacha chini. Maksuudi pia katika

Utengano alitokana na tabaka la wakulima, lakini alipopata madaraka ya kuwa mkuu wa wilaya, aliwapa kisogo wakulima na kuanza kuwadhulumu kwa kudai hongo kabla ya kuwahudumia.

Jamii ya Asali Chungu siyo tu iliyo na mtindo huu. Hata katika mataifa mengi ya Kiafrika, wamo akina Maksuudi na akina Zuberi wengi. Kuna <sup>Soma Augaine Swan</sup> watu ambao baada ya kuchaguliwa bungeni na kupewa madaraka, labda ya uwaziri, huanza kuwadharau wananchi wale wale <sup>miss</sup> <sup>Wapende Was'pend</sup> waliowawezesha kuyapata madaraka hayo. Lakini hatimaye, (katika kipindi kingine) hunyimwa kura na aghalabu hujuta sana, kwa vile huu sasa huwa ni wakati wao kudharauliwa. Poa <sup>mif</sup> <sup>multe multsyga moi multe parny</sup> <sup>usigote maati?</sup> <sup>→ puni usoni sio</sup> <sup>sasa</sup> <sup>kipicome</sup> Dude pia ameanza maisha ya namna hiyo - ya <sup>I Even</sup> <sup>abana</sup> <sup>utwala</sup>

Dude pia ameanza maisha ya namna hiyo - ya ulimbwende, lakini twatarajia kuwa aliowaacha chini watamtweza na kumtumbukiza katika hali yake ya zamani.

#### 4:5:3 KIMALIZIO

Katika sura hii tumeyaona makundi matatu ya watu. Kuna ~~mabwanyenye~~ ambao wanafanya juu chini kuyalinda maslahi yao - kundi hili lawakilishwa na Zuberi. Hili ni kundi ambalo limesitawi kutokana na jasho la wananchi wa kawaida. Wawakilishi wa kundi hili ni wanyang'anyi kama vile ilivyodhihirishwa kutokana na sifa mbaya za Zuberi. Wana madaraka ambayo wanayatumia kuuendeleza ujisadi na maovu mengine katika jamii.

Jambo muhimu la kutaja kuhusu kundi hili ni kuwa baadhi ya mabwanyenye hao huishia katika maangamizi.

Wanawadhulumu wanyonge vya kutosha, laini laana za wanyonge huwapata na wanaporomoka kutoka walikopanda <sup>Mo i? wache wajige, Mai Thatazivo ve w kwa hieni yale</sup> f kwa kishindo kikubwa. <sup>Na mauti? Katu hatayepa. - mudi a taka ziku gatapenda.</sup>

Kundi la pili ni la watu amba o huwa katika tabaka la makabwela. Kwa bahati nzuri, wanabarikiwa kupata mali au anasa. Baadhi yao wafikapo kwenye <sup>Det. mwepesi wa kusau - ms. mohamed - kia che maflee neema husahau zile hali zao za umaskini na huendeleza</sup> ile mienendo ya kibwanyenye. Kundi hili lawakilishwa na Dude ambaye siku zake za neema alijilimbika katika anasa zisizokuwa na kikomo. "Je, Bi Daudi yuko wapi <sup>h h iki si cisimai</sup>"

Kundi la tatu ni la maskini hoe <sup>h</sup> amba o huzaliwa katika umaskini na hufa katika hali hiyo hiyo. Hawa ni kama vile Bi Pili, <sup>Bushiri</sup>, Mzee Omari n.k. Hawa ni watu amba o hawana sauti, mali wala cho chote. Na hili ndilo kundi ambalo aghalabu, kutokana na hali zao za idhilali na jitimai huzua njia za kujikomboa kutokana na hali yao dhalili. Wao ndio chanzo (kiini) cha mapinduzi ya kisisasa, kiuchumi na kijamii.

#### 4:6 TANBIHI

1. Katika tabaka la kibwanyenye, ufisadi umetapakaa kila mahali, sio tu katika jamii moja. Upo katika mataifa ya Kiafrika na vile vile mataifa mengine yote ulimwenguni.

2. Hussein, E., Mashetani, O.U.P. Nairobi, 1971.  
(uk. 2)
3. Mushi S. S., (transl.) Mfalme Edipode, O.U.P.  
Dar-es-Salaam, 1971.

## S U R A Y A T A N O

### 5:0 HITIMISHO

Uhakiki wa riwaya za Said Ahmed Mohamed umetudhihirishia mambo kadha. Kwanza umetubainishia wajibu wa fasihi katika jamii, na pili umetufunulia ukweli wa maisha halisi ya jamii ki-historia.

Katika riwaya zote tatu, S. A. Mohamed amejizatiti kutubainishia ukweli wa hali ya mambo yalivyo, bila kutuficha hata chembe. Pale ambapo pana uonevu au uovu wowote anaueta na kuuashiria ili uonekane wazi wazi.

Ameeleza kinagaubaga juu ya mifumo itumiwayo kuwadhalilisha wanyonge; mifumo hiyo ikiwa ni siasa, uchumi na ma-sala ya jamii. Basi, twaweza kusema kuwa msanii huyu ameitumia fasihi ipasavyo - kwa kuyamulika maovu katika jamii ili wanaoshiriki katika maovu hayo waweze kujirekebisha, la sivyo, watakumbwa na athari zilizowakumba watangulizi wao walioikiuka mipaka ya maadili.

Jambo lingine muhimu lililodhihirishwa ni kuwa katika jamii ambayo imejigawa katika matabaka, mtafaruku hauishi. Mtafaruku huo huwa ni baina ya tabaka la juu na tabaka la chini. Watu wa tabaka la chini hutia kani na kupigania haki zao ambazo zimekaliwa na watu wa tabaka la juu. Kufuatia utafiti wa riwaya

hizo, pia imeonekana kwamba mnyonge kamwe hawezi kunyamaza mpaka arejeshewe utu na heshima zake alizopokonywa na makabaila. Kwa mfano, katika riwaya zote, tumeuona ukakamavu wa wanyonge katika shauri la kujikomboa kutokana na uonevu na ukandamizwaji. Wana imani isiyo haba kuwa, ingawa hawana nguvu za kutosha kumwondoa mdhalimu mara moja, hatimaye watamuweza. Jambo lililo muhimu kwa wanyonge ni kuupata ule mwamko kuwa wao ni wanyonge. Basi wajue kwamba ukombozi utatokana na wao, wala hauwezi kutoka nje.

Imebainika kuwa kiini cha uovu ulimwenguni ni mali, cheo, madaraka, ubinafsi, uroho, chuki n.k. Hali hii hutokea sana katika jamii ambapo mifumo ya siasa, uchumi, jamii na utamaduni imemilikiwa na watu wachache katika jamii. Watu hao wachache hujihisi kuwa wao ni miungu wadogo. Wanajijaza kiburi, fahari hadhi na majivuno, na kuanza kutambaa huku na kule wakijinyakulia cho chote wanachoweza kukififikia.

Said A. Mohamed aamini kuwa duniani hapatakuwa na amani mpaka tabaka za kijamii zitakapovunjwa na kupondwapondwa na haki zitakapotambuliwa. Bila hivyo, mapinduzi ya mara kwa mara hayataisha.

Imani ya wanyonge juu ya ushindi katika vita vya ukombozi inawapa moyo watu wowote au makundi yo yote ya watu yaliyo chini ya udhalimu huu na ule kuwa

wasikate tamaa. Hasa wafanyakazi wa hali ya chini wanazinduliwa kuwa wasiwe waoga pale wanapoutetea ukweli na haki za kibinadamu. Kwa upande mwingine, S. A. Mohamed anawahimiza wanafasihi kuwa wana wajibu muhimu wa kuiambia jamii ukweli pasipo kuchelea athari hizi na zile. Anaupinga unafiki katika kulitenda jambo, maadam, dhuluma nazitendwe jinsi gani, uonevu nauendelezwe kiasi gani, haki na ukweli ndizo hatimaye zitatawala. Bila hivyo, basi, nguvu za wanyonge katika harakati za kujihami na kujikombua hazitaisha kamwe. Mtafaruku na mapambano yataendelea.

*mpaka lini?*

- Mtahiriwa ne wetahini wa kazi hili ni 'maskaiva' wote.
- Kama nungekwa nimi, nisingempa hata 2%

*Pamje Jhny  
Makosa Chaguo  
Kithini Sabukwa Bims  
Kapi? Jinga!  
Mtahini wa Mtahini wa  
Ulikuwa moja!*

*Amwajoz*

*LSP*

M A R E J E O

- Abdalla, A., Sauti ya Dhiki, O.U.P. Nairobi,  
1973
- Abdulaziz, M.H., Muyaka, 19th Century Swahili  
Popular Poetry, K.L.B. Nairobi  
1978.
- Arvon, H., Marx and Engels on Literature  
and Art. (International General,  
New York, 1923)
- Chacha, N.C., Ushairi wa Abdilatif Abdalla.  
Tasnifu ya M.A. 1980, Chuo Kikuu,  
Nairobi
- Cohen, R., Marxism and Africa: Old and New  
Projected, University of  
Birmingham, 1975.
- Coser, L.A., Sociology Through Literature,  
Prentice Hall, international  
Inc. London, 1963.
- Crystal & Davy, Investigating English Style.  
Longman Group, 1969.
- Eagleton T., Marxism and Literary Criticism,  
Methuen and Co. Ltd. Longon, 1970.

- Freire, P., Pedagogy of the Oppressed,  
The Seabury Press, New York,  
1968.
- Gachukia, E., (Ed.) Teaching of African Literature  
in Schools, K.L.B., Nairobi 1978.
- Hudson, W.H., An Introduction to the Study of  
Literature (George & Co. Ltd.  
1965).
- Hussain, A., Marxism and the Agrarian  
Question (Vol. 2). The Macmillan  
Press Ltd., London, 1981.
- Hussein, E., Kinjeketile, O.U.P., Nairobi,  
1969.
- 
- Mashetani, O.U.P., Nairobi, 1971.
- 
- Wakati Ukuta, E.A.P.H., Nairobi,  
1971.
- 
- Arusi, O.U.P., Nairobi, 1980
- 
- Jackson, J.A., Social Stratification, University  
Press, Cambridge, 1968.
- 
- Jones, E.D., (Ed.) African Literature Today,  
Heinemann, Nairobi, 1975.
- 
- Kamusi ya Kiswahili Sanifu, O.U.P., Dar-es-Salaam, 1981.

- Kazungu, K.E., "Deviation and Foregrounding in Chosen Swahili Literary Texts" Tasnifu ya M.A. 1982 - Chuo Kikuu, Nairobi.
- Kezilahabi, E., Dunia Uwanja wa Fujo, E.A.L.B., Nairobi, 1975.
- Kichomi, Heinemann, Nairobi, 1974.
- Kiswahili: Jarida la Chuo Kikuu Cha Uchunguzi wa Lugha ya Kiswahili, Dar-es-Salaam, Vol. 41, 1971.
- Kitsao, J., "A Stylistic Approach Adopted for the Study of Written Swahili Prose Texts". Tasnifu ya M.A. 1975 - Chuo Kikuu, Nairobi.
- 
- Uasi, O.U.P., Nairobi, 1980
- Lefebre, H., The Sociology of Marx, The Penguin Press, London, 1968.
- LUGHA: (A Journal for Language Teachers in Kenya - Vol. 5, Nov I, 1976).  
(A Journal for Language Teachers in Kenya - Vol. 5 No. I, 1976).

Marx, K., (1818 - 1883), Capital, London, 1946.

Marx K., & Engels F., The Communist Manifesto  
Penguin Books, 1968.

Mazrui, A., Kilio Cha Haki, Longman Kenya  
Ltd., Nairobi, 1981.

---

"Dunia Mti Mkavu, A Literary  
Treatise on Marxism". Makala  
yaliyoandikwa na Mazrui mnamo  
11/6/81.

Mazrui A., "Maendeleo ya Fasihi ya Kiswahili"  
na makala yaliyotolewa katika  
Kazungu K., kongamano la kimataifa la Chama  
cha Kiswahili cha Kenya, Nairobi,  
1981.

Mohamed S.A., "Kupatana na riwaya zangu"  
(KKA) Kongamano ya Kimataifa,  
Kenya Polytechnic, Nairobi,  
Agosti, 1981.

---

Utengano, Longman, Nairobi, 1980.

---

Asali Chungu, Shungwaya Publishers,  
Nairobi, 1978.

Mohamed S.A., Dunia Mti Mkavu, Longman, Nairobi,  
1980.

- 
- Sikate Tamaa, Longman, Nairobi,  
1980.
- Mohamed, S.M.,  
Nyota ya Rehema, O.U.P.,  
Nairobi, 1976.
- Moore, G.,  
Twelve African Writers,  
Hutchinson University Library  
for Africa, London, 1980.
- Mugambi, P.J.,  
Tasnifu ya M.A. 1982.
- Mugo, G.M.,  
Visions of Africa, K.L.B.,  
Nairobi, 1975.
- Muhando, P.,  
Hatia, E.A.P.H., Nairobi, 1972.
- 
- Tambueni Haki Zetu, Tanzania  
Publishing House, Dar-es-Salaam,  
1975.
- Mutiso, G.C.M.,  
Socio-Political Thought in  
African Literature, Macmillan,  
London, 1974.
- Sayyid, A. Nasir,  
Al-Inkishafi, O.U.P., Nairobi,  
1971.
- (  
Ngugi wa Thiongo,  
"Literature and Society" in  
E. Gachukia (Ed.), Teaching of  
African Literature in Schools,  
K.L.B., 1978.

---

A Grain of Wheat, Heinemann,  
London, 1968.

---

Kesho Wakati Kama Huu, E.A.L.B.,  
Nairobi, 1970.

Ngugi wa T., &  
Micere, M.,

Mzalendo Kimathi, Heinemann  
Educational Books, Nairobi, 1978.

Omari, C.,

Usawa wa Binadamu, E.A.L.B.,  
Nairobi, 1976.

Okot P' Bi'tek,

Wimbo wa Lawino, E.A.P.H.,  
Nairobi, 1975.

Sarte, J.P.,

What is Literature?, Methuen  
and Co. Lt., London, 1970.

Sengo, T.,

MULIKA Vol. 8 (Taasisi ya  
Uchunguzi wa Kiswahili wa Chuo  
Kikuu Dar-es-Salaam, 1976).

SWAHILI:

"Jarida la Taasisi ya Uchunguzi  
wa Kiswahili". Toleo I - 1936-  
1970 - Chuo Kikuu - Dar-es-  
Salaam.

Swingewood, A.,

Marx and Modern Social Theory,  
The Macmillan Press Ltd., Great  
Britain, 1975.

Topan, F., (Ed.)

Uchambuzi wa Maandishi ya  
Kiswahili - Vol I, O.U.P.,  
Nairobi, 1971.

Tumin, M.M.,

Social Stratification, Prentice  
Hall, New Jersey, 1967.

---

Readings on Social Stratification,  
Prentice Hall, London, 1970.

UMMA:

"A magazine of original writing  
from the University of Dar-es-  
Salaam, Vol I., 1970.

Wanjala, C.,

Standpoints on African Literature,  
E.A.L.B., Nairobi, 1973.

William, R.,

Marxism and Literature, O.U.P.,  
Oxford, 1977.

Wright, E., (Ed.)

The Critical Evaluation of  
African Literature, Heinemann  
Educational Books, London, 1973.